ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake

29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tisa – Tarehe 29 Januari, 2013

(Kikao kilianza saa 3. 00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujawasilisha Hati Mezani kama kawaida na leo tumepata wageni, tena wagani hawa ni wageni ambao baadhi yao tupo karibu sana huwa tunashirikiana kwa shughuli mbali mbali.

Kwa hivyo wageni wetu wa leo ambao wapo kwenye ukumbi wa juu, kwanza ni ujumbe kutoka jumuiya ya wasaidizi wa sheria, naomba wasimame ili wasalimiane na Waheshimiwa Wajumbe.

Hawa jumla yao ni 22 na wanaongozwa na Katibu wa jumuiya hiyo Ndugu Ahmada Ali Haji.

Waheshimiwa Wajumbe jumuiya hii inajihusisha na utoaji wa msaada wa kisheria katika majimbo yote ya Zanzibar. Kama munavyoelewa ndio ambao tumekuwa tunasaidiana nao katika shughuli yetu muhimu ya elimu ya Katiba. Kwa hivyo hawa wamekuwa wanatusaidia sana kwenye maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

Ndugu wasaidizi wa sheria karibuni sana na tunawashukuru kufika leo. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani taarifa ya utekelezaji ya mapendekezo ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar.

Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kuweka utekelezaji wa majukumu na uwezo na mambo yanayohusiana na hayo na ninaomba usomwe kwa mara ya mwanzo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba usomwe kwa mara ya mwanzo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria Kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba usomwe kwa mara ya kwanza.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 17

Wananchi Waliokosa Kupiga Kura katika Uchaguzi wa 2010

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Katika uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2010 baadhi ya wananchi ambao walikuwa wapiga kura halali katika chaguzi kuu za nchi za miaka iliyopita, hawakupewa haki hiyo pamoja na kuwa vipande vyao vya zamani vya kupigia kura walikuwa navyo.

- Jumla ya wapiga kura hao (wanawake na wanaume) walikuwa ni wangapi.
- Ni sababu zipi zilizopelekea kukosekana kwa haki yao hiyo.
- Serikali imeweka uamuzi gani kwa chaguzi zinazofuata kwa wapiga kura wa aina hiyo na uamuzi huo utaanza lini utekelezaji wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, mwezi wa Julai, 2009 hadi Mei 2010 Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliendesha kazi ya uandikishaji ya wapiga kura wapya na uendelezaji wa daftari la wapiga kura. Kazi hiyo ilifanyika kwa awamu mbili, kuanzia Julai, 2009 hadi Januari, 2010 na Februari, 2010 hadi Mei 2010.

Tume ilipanga kazi ya uandikishaji ya wapiga kura wapya na uendelezaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa kuzingatia maelekezo yote ya sheria za uchaguzi ya mwaka 1984 kama ilivyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Katika kuifanya kazi hiyo, Tume ilitumia makadirio ya watu zilizotokana na sensa ya taifa ya watu na makaazi ya 2002 zinazoonesha kuwa Zanzibar ilikuwa na watu 981,754 (wanawake 500,908 na wanaume 480,846) kati yao, watu 611,013

walikadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 18 na kuendelea, umri ambao unawezesha kuandikishwa kuwa wapiga kura kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kazi hiyo ilipomalizika mwezi wa Mei, 2010 Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilifanikiwa kuandikisha na kubadilisha shahada za wapiga kura 407,658 sawa na asilimia 66.71 ya makadirio ya idadi ya watu na kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya watu na makaazi ya mwaka 2002.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

a). Mhe. Spika, sio rahisi kutaja idadi kamili ya wapiga kura wenye shahada za zamani za kupigia kura na jinsia zao kwa kuwa hakuna wapiga kura walioiarifu Tume juu ya kukosa nafasi hii kubadilishiwa shahada za zamani za kupigia kura.

b) Mhe. Spika, sababu kubwa ya wapiga kura hao kushindwa kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa 2010 ni kushindwa kwenda katika vituo vya kujiandikisha na kubadilisha shahada zao katika awamu zote mbili za uandikishaji kwenye maeneo yao. Hakuna mpiga kura hata mmoja miongoni waliofika katika vituo vya uandikishaji vya wapiga kura na vielelezo vilivyokubalika kwa mujibu wa sheria ambaye hakubadilishiwa shahada yake ya zamani ya kupigia kura au kuandikishwa kuwa mpiga kura.

c) Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imo mbioni kuhakikisha kuwa wapiga kura wote ambao hawajabadilisha shahada zao za zamani za kupigia kura kutokana na sababu mbali mbali wanapatiwa shahada mpya za kupigia kura wakati kazi ya uendelezaji wa daftari la kudumu la wapiga kura zitakapoanza kuanzia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2013. Serikali inatoa wito kwa Wazanzibari wote waliofikia umri wa kupigia kura kujiandaa na kujitokeza kwa wingi kujiandikisha wakati kazi hiyo zinapokuwa zinaendelea katika maeneo yao.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata majibu marefu ya ziada kuhusu swali hili Nambari 17.

Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza Mhe. Spika, naomba unikubalie kuwa wapo watu wamepiga kura katika miaka ya nyuma lakini uchaguzi huu uliopita hawakupiga kura wakati vitambulisho vyao vya kupigia kura walikuwa navyo sababu tu ni kwa kuwa hawakuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi na kwa hivyo wakakosa haki zao, na ni wengi kama mheshimiwa anasema hakuna lakini mimi nasema wapo ni wengi.

Swali la kwanza, ilikuwaje kule nyuma wakaruhusiwa na walikuwa hawana hivi vitambulisho lakini katika uchaguzi huu uliopita ikawa hawakuruhusiwa kutumia haki yao na akitaka kwa majina nitamletea chungu nzima.

La pili, Mhe. Spika, ni mara nyingi Mhe. Waziri tunapomuelekeza kuwa kuna matatizo haya husema kuwa atayachukulia hatua. Hili ambalo nahakikisha watu wako wamekoseshwa haki yao atalichukulia hatua vipi alau ya kupata hivyo vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi bila ya kulazimishwa kwa kupeleka vyeti vya kuzaliwa ni watu wazima na wazee ili waendelee na hii haki yao.

Kifungu cha (c) nasikitika sana kwamba takwimu haikupatikana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Salim arudie maswali yake aelekeze maneno yake kwenye spika ili nimsikie vyenginevyo itakuwa vigumu kumjibu.

Mhe. Spika: Rudia maswali yako.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nnavyosema wapo Wazanzibari wengi ambao miaka ya nyuma si mara moja wala si mara ya mbili walipiga kura na mpaka leo vitambulisho vyao vya kupigia kura wanavyo, lakini katika uchaguzi uliopita hawakupata haki hiyo kwa sababu walikuwa hawana kwa bahati mbaya vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi, na walipokwenda kwa Sheha hawakupata barua ya kwenda kuchukua vitambulisho kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa.

Namuuliza Mhe. Waziri watu kama hawa ambao ni Wazanzibari nao wameshapiga kura na mtu yeyote mwenye kipande cha kupiga kura kwa mujibu wa Katiba anayo haki ya kupiga kura, atawasaidia vipi kuona kuwa wamepatiwa haki yao ya kupigia kura na wamepatiwa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

La pili nilikuwa nasema nasikitika sana mheshimiwa nimeuliza swali lakini sikupatiwa idadi kamili ya watu hao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi rafiki yangu maswali yake yenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, asisitike kwa kutokumpatia takwimu kwa sababu takwimu hizi lazima ziwe na vielelezo. Kwa bahati mbaya wahusika hawakupeleka kujiandikisha kwa mujibu wa taratibu wa sheria zinavyotaka. Kwa msingi huo huwezi kujua idadi yao mpaka pale watakapokwenda kwa Tume wakajiorodhesha ndio itakavyowezekana kujulikana.

Lakini Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie kwamba wananchi hawa watakapofuata sheria na taratibu zilizowekwa, nawahakikishia kwamba wataweza kupiga kura. Matangazo mbali mbali Mhe. Spika, yalitoka katika mwaka huu kwa nia ya wale ambao walikuwa na kadi zile za zamani za kupigia kura waende wakajiorodheshe ili wapate haki hiyo ya kupigia kura.

Kwa bahati mbaya hawakujitokeza kufanya hivyo. Sasa utaratibu umeandaliwa ili wananchi hawa waweze kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu unaokuja. Cha msingi ni kuzingatia kwao

kukamilisha masharti yote ya uandikishaji kama yanavyotakiwa na yatakavyotangazwa mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ili wananchi hao wapate nafasi yao ya msingi.

Suala la kudharau Mhe. Spika, wakati mwengine ndio linalotuponza. Cha msingi ni kufuata zile taratibu zilizoekwa ili watu hawa haki yao ya msingi waipate. Na kama kuna tatizo lolote jengine zaidi Mhe. Mwakilishi tukae tuzungumze unieleze kwa kina ili tuelewane vizuri tuweze kuchukua hatua zinazofaa.

TAARIFA

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kifungu nambari 7 (2) cha Katiba ukurawa wa nne kwa ruhusa yako naomba nikinukuu kinasema hivi, "Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria na kuweka masharti yanayoweza kumzuia au kuzuia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura kutokana na yeyote kati ya sababu zifuatazo, yaani Mzanzibari huyo kuwa na uraia wa nchi nyengine na kuendelea".

Lakini nilichokusudia ni hiki kukosa au kushindwa kwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura. Hawa walikuwa na vitambulisho vya uandikishaji kama mpiga kura kwa mujibu wa Katiba ilikuwaje sasa wakakoseshwa haki zao. Na kukoseshwa haki yao kwa mujibu wa kifungu hiki cha Katiba ni kuvunja Katiba ya nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu Mhe. Mwakilishi kama alivyoeleza.

Mhe. Spika, hatukuja hapa kulumbana na sisi hatukuwepo kwenye kituo kile cha uandikishaji wa wapiga kura. Hatuwezi kuwa na uhakika kwamba walikuwa kweli wana kadi zilizotimiza masharti kwa mujibu wa matakwa ya sheria.

Tunachosema hapa mtu yeyote yule ambaye ametimiza matakwa ya sheria ana haki ya kupewa kupiga kura na awe mpiga kura. Kwa hivyo pale mimi sikuwepo na yeye hakuwepo hana ushahidi kama wametimiza hayo masharti. Kama wametimiza hawawezi kukataliwa kwa nini wengine wapate nafasi hiyo na wengine wasipewe.

Ninachosema mimi kama kuna tatizo lolote basi wafuate taratibu ziliopo na kura wananchi wapate haki yao.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, hiki chombo ni chombo kimoja kikubwa na chenye kutegemewa na wananchi wa Zanzibar. Na kwa mujibu wa Kanuni ya 59 (3) naomba kwa heshima na taadhima nikinukuu kifungu hiki.

Kanuni hii inahusu mambo yanayofaa na yasiyofaa kuzungumzwa. "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayotoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza

kumtaja Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika". Mwisho wa kunukuu Mhe. Spika.

Kwa kuwa Mhe. Waziri wakati anamjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad hapa alisema yeye kuwa hana uhakika na yeye hana uhakika kwa sababu hawakuwepo. Kwa sababu hawakuwepo, kwa hivyo kusema maneno aliyosema Mhe. Waziri na kuingia kwenye *hansard* ni kukiuka Kanuni hii ya 59 (3).

Kwa heshima na taadhima nakuomba katika hili sasa umtake Mhe. Waziri afute usemi wake kusudi *Hansard* zisije zikapotosha umma.

Mhe. Spika: Hivi angesema ana uhakika ungemwambia lete ushahidi. Yeye anasema hana uhakika, hiyo ndio namna yenyewe. Utamlazimishaje aje aseme kwamba nina hakika juu ya jambo ambalo limetokea kwenye kituo cha uchaguzi yeye hana uhakika kwa sababu hakuwepo.

Sasa hivyo ndio hali yenyewe asemeje sasa, ninadhani katika hili tuliache. Maana akisema kama ana uhakika, maana yake atoe ushahidi awe na ushahidi wa jambo lililotokezea huko, yeye hana uhakika. Ninadhani tuendelee.

Nam. 38

Ukosefu wa Eneo la Kuegesha Gari

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Baraza la Mji Chake-Chake limeamua kutumika soko la Samaki la Tibirinzi kuwa soko la matunda, na kwa kuwa pembezoni mwa soko hilo kuna bahari ambayo imepandwa miti ya mikoko, na kwa kuwa hakuna eneo la kuegesha magari yanayoshusha na kupakia bidhaa.
Je, Serikali inaonaje ikalifukia eneo hilo ili kutengeneza eneo la maegesho ya gari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu **:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 38 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, awali ya yote naomba niwapongeze sana viongozi wa Baraza la Mji Chake-Chake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuanzisha soko jipya la matunda na mboga mboga pembezoni mwa soko la samaki

Kwa kweli kazi au ubunifu waliofanya umepunguza msongamano mkubwa uliokuwepo pale *stand* Chake-Chake.

Mhe. Spika**,** hatua za kutengeneza eneo la kuegeshwa magari katika eneo la Soko la Matunda na Mboga Mboga la Chake Chake zimeanza. Awali alitafutwa Mtaalamu kulifanyia utafiti eneo hilo ikiwemo kuangalia athari za kimazingira katika eneo ambalo linatarajiwa litafukiwa. Kazi

hiyo imeanza kwa hatua ya mapendekezo ya michoro kwa eneo zima likiwemo eneo la kuegeshea Magari na kazi hiyo hivi sasa inazingatiwa kwa pamoja na wataalamu wa mazingira kutoka Idara ya Mazingira.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo.

Ni wafanyakazi wangapi wamefaidika na soko hilo na jee huduma ya vyoo katika soko hilo ikoje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa jumla wafanyakazi waliofaidika na soko lile wanafikia mia moja, sina uhakika na hiyo *figure* lakini naambiwa wanafikia mia moja.

Na vyoo vimejengwa vipya pale, vyoo viwili kukidhi soko au watu wanatumia soko lile. Tumeona kweli lazima tuwafikirie kuna soko la zamani pale la samaki kipo choo cha zamani lakini na pale wamejenga vyoo vipya viwili.

Nam. 95

Athari za Kuyumba kwa Uchumi na Hali ya Maisha

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Mwaka 2011 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitimiza miaka 47 ya mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, licha ya jitihada mbali mbali za serikali yetu za kuinua hali za maisha ya wananchi bado hali za maisha ya wananchi wetu siyo za kuridhisha sana na juhudi zaidi zinatakiwa zifanywe kuleta afuweni.

- Jee, serikali inawambia nini Wazanzibari juu ya kuyumba kwa uchumi wa nchi, ongezeko la bei na kuongezeka kwa umaskini kwa watu wa hali ya chini.
- Serikali inawashirikisha vipi wananchi moja kwa moja katika kupanga mahitaji yao katika bajeti za kila mwaka.
- Jee, serikali haioni kuwa wakati umefika na kuwa "*serious*" kuachana na matumizi makubwa ya yasiyokuwa ya lazima ya fedha za wananchi hasa katika mambo ya sherehe, matamasha, warsha na safari nyingi za nje za viongozi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba unipe ruhusa kidogo nitoe maelezo mafupi kutokana na tokeo lililotokea jana.

Jana wakati tunajadili taarifa ya ZECO katika mijadala Mhe. Hamza alisema kwamba makusanyo yanayokusanywa na ZRB tokea aliyeondoka kamishna aliyeondoka yameshuka. Na kwa sababu chombo hiki ni chombo kikubwa sana na kinatakiwa kitoe taarifa sahihi kwa ajili ya wananchi wetu na kwa sababu mimi ni waziri mwenye dhamana ya mapato na kwa sababu wananchi wametaka kujua juu ya suala hili ni sahihi au sio sahihi. Nimeona nichukue fursa hii kuelimisha umma.

Ndugu yangu Mhe. Hamza nadhani ulimi uliteleza. Mapato yanayokusanywa na ZRB yameongezeka na wahenga wanasema mganga hajigangi lakini kama kuwapongeza basi mimi nawapongeza sana ndugu zangu wa ZRB.

Mhe. Spika, kuanzia mwezi wa Julai hadi Disemba, 2012/13 ZRB imekusanya jumla ya shilingi bilioni sitini na saba nukta sita nne. Ukilinganisha na Julai hadi Disemba, 2011/12 imekusanya jumla ya shilingi bilioni hamsini na tisa nukta sita ziro, ongezeko la bilioni nane asilimia kumi na tatu nukta nne sita

Maombi yangu kwa Waheshimiwa Wajumbe tujitahidini sana kutumia taarifa sahihi katika kuwaelimisha wananchi wetu na pale ambato sisi kwa upande wa serikali tunahisi kuna tatizo hatutosita kutoa taarifa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka nitoe taarifa hiyo ili wananchi waelewe kwamba ni sahihi ndugu zetu wa ZRB wanafanya kazi vizuri na mimi sina wasi wasi, tutakapofika mwezi wa sita mwaka huu, makusanyo yetu yataweza kuwa makubwa zaidi ya hapa tulipo.

Mhe. Spika, nitaiwasilisha hii kwa Katibu ili utoe fotokopi Wajumbe wote waweze kupata na kushuhudia wenyewe hesabu hizi.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kwa heshima na taadhima kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

- Mhe. Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mhe.Mwakilishi kuwa katika kipindi cha miaka 47 tokea Mapinduzi ya 1964, Serikali imekuwa ikichukuwa jitihada mbali mbali za kuinua hali ya maisha ya wananchi wetu, lakini bado hatujafikia hali ambayo itamfanya kila mwananchi kuridhika. Kutokana na hali hiyo, napenda kuwafahamisha wananchi mambo yafuatayo:-…

    - Uchumi wa Zanzibar hauyumbi na badala yake unakuwa mwaka hadi mwaka, lakini pia mahitaji ya wananchi wetu ndio yanaongezeka kwa kasi kubwa mwaka hadi mwaka, kutokana na kuongezeka kwa kasi ya idadi ya watu, na hivyo kuendelea kusababisha wananchi wengi hasa wale wa chini, hali zao za kimaisha kuwa sio nzuri, hasa wale wenye familia kubwa.
    - Uzalishaji mdogo wa mazao muhimu hasa chakula husababisha bei za ndani kutokuwa tulivu. Hata hivyo, hali ya mfumko wa bei inaendelea vizuri na kwa mwezi wa Disemba 2012 mfumko wa bei umeshuka na kufikia asilimia 3 tu.

- Upandishaji wa mafuta katika soko la dunia huchangia kupanda kwa bei za chakula pamoja na gharama za maisha.

Mhe. Spika, Serikali kwa kuyaona hayo, imeendelea kuwasaidia wananchi wake, kwa kupunguza kodi kwa bidhaa muhimu, hasa za chakula ili wananchi waweze kumudu maisha yao. Hata hivyo, Serikali pia inawaomba wananchi kuzingatia uzazi wa mpango kwa lengo la kuwa na familia tutakazoweza kuzimudu.

- Mhe. Spika, mipango mikuu ambayo serikali huitumia wakati wa kuandaa bajeti ni dira ya 2020 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA). Mipango ambayo wakati wa maandalizi yake imewashirikisha wananchi kwa ukamilifu. Aidha, Wajumbe wa Baraza lako tukufu nao pia huwawakilisha wananchi vizuri katika maandalizi ya bajeti ya kila mwaka, jambo ambalo linanipa faraja. Matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wawakilishi wataendelea kuwawakilisha wananchi kwa kiwango kikubwa zaidi, kwa lengo la kupata maoni ya wananchi wengi zaidi pamoja na kulijengea heshima Baraza letu. Ushiriki wa aina hii kwa maoni yangu ni mzuri zaidi.

- Mhe. Spika, ni kweli wakati umefika kwa serikali kupunguza zaidi matumizi ambayo sio ya lazima, na hivyo Mhe. Spika, ndivyo tunavyofanya kila bajeti na tutaendelea kufanya hivyo. Ombi langu kwa Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kushirikiana katika kusimamia ukusanyaji wa mapato na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo napenda kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza niipongeze serikali kwa kupunguza ushuru bidhaa ya chakula, lakini bado msamaha huo unawanufaisha vipi wananchi wakati bado kilio cha mchele hasa wa daraja la chini (mapembe) bado uko juu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba kuna asilimia 3 ya Zanzibar, wakati bado kuna kilio cha wananchi juu ya mfumko wa bei za vyakula katika masoko. Je, ni sababu gani?

Vile vile Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipoendelea kujibu swali nambari 3 kwamba uchumi wa Zanzibar haujayumba, unakua vizuri kama ulivyosema, lakini thamani ya fedha imeporomoka. Je, serikali ina mpango gani kwa kupitia viwango vya mishahara hasa kwa kima cha chini, ili iweze kuwanufaisha angalau nusu mwezi na hivi sasa umesema kwamba mapato yamezidi kukua kutoka *ZRB*.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, nadhani hili suali la (c) nimuombe Mhe. Waziri aulize kwenye swali la msingi, liko nje kidogo ya hapa na pengine linahitaji taarifa zaidi. Kwa hivyo, jibu lile swali (a) na (b).

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu maswali 3 ya nyongeza ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo. Kwanza mimi niliyepewa dhamana ya kodi nikishirikiana na waziri mwenzangu

wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tutaendelea kuwanasihi wafanyabiashara ili waendelee kushusha bei, hasa bei za mchele. Tumekuwa tukifanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo.
Mhe. Spika, kinachowakwaza wafanyabiashara wetu, pale ambapo mchele katika soko la dunia nao unapanda bei, lakini tutaendelea na kila itakapohitajika basi tutaendelea kupunguza kodi ili wananchi hasa katika hizi bidhaa muhimu waweze kufaidika.

Pili, Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim alitaka kujua sababu za msingi zilizofanya mfumko wa bei kushuka. Mfumko wa bei umeshuka kuna sababu nyingi.
Kwanza katika soko la dunia mafuta nayo yameshuka bei, ambapo yalikuwa yanachangia katika sehemu kubwa kuongeza mfumko wa bei.

Pili, kuna baadhi ya bidhaa zimeendelea kuzalishwa kwa wingi katika kipindi cha mwezi wa Disemba, hasa mazao ya baharini kama vile samaki wamezalishwa kwa wingi, Ambapo nayo ilikuwa ikichangia kwa kiwango kikubwa bei kuongezeka.

Mhe. Spika, suali lake la tatu kwa kupitia viwango vya mishahara. Naomba kumwambia Mhe. Jaku Hashim pamoja na Waheshimiwa wengine pamoja na wananchi wetu kwamba kila hali ya uchumi itakapoimarika serikali inaelewa kwamba viwango vyetu vya mishahara hasa vile vya chini bado viko chini, tutaendelea kuviimarisha ili wananchi wetu waweze kufaidika na matunda ya uchumi wa nchi yao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, Mhe. Waziri amewaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa waendelee kukaa na wananchi wao ili kuweza kuijadili mipango ya bajeti ya serikali. Ni jambo zuri na ni jambo ambalo linaendelea katika dunia hii.

Sasa ninavyojua Mhe. Spika, mwezi huu wa Januari hadi mwezi Machi ni mwezi wa maandalizi ya bajeti.

- Je, Mhe. Waziri anaweza akatupatia vipaumbele vya serikali, ambapo wizara yake imeandaa ili wawakilishi wavichukue na kuvipeleka kwa wananchi kwa ajili ya kupata mijadala, ili hatimaye bajeti itakayoandaliwa iwe ni bajeti ya wananchi?
- Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema wanaendelea kushirikiana na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili kuwanasihi wafanyabiashara wetu kupunguza bei za vyakula. Je, kwa nini ule utaratibu wa kutangaza bei za vyakula katika soko la dunia kila mwezi hauendelei, ili wananchi wakaangalia uhusiano baina ya punguzo la kodi na bei ambayo inaletwa na wafanyabiashara wetu?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nimsaidie Mhe. Hija Hassan pamoja na Waheshimiwa wengine, uzuri wa bajeti ni ile yenye mfumo wa *bottom up aporoach*, mawazo yanatoka chini yanakwenda juu. Mimi nilimtarajia Mhe. Hija Hassan na Wawakilishi wengine, wao waanze kuleta maoni yao, juu

ya nini wananchi wao wanatarajia katika bajeti inayokuja. Hilo lingekuwa busara zaidi kuliko kusubiri mpaka tukayaandaa sisi tukampa yeye.

Sisi tunakusanya kupitia kwenye sekta mbali mbali na mara nyingi yanakuwa tayari katika mwezi wa Machi au mwezi wa Aprili. Sasa hivi tuko katika makusanyo. Lakini ningemuomba kama ana maoni ya wananchi wake, kwa kupitia sekta yoyote anaweza akayapitisha ili ile sekta ikaweza kuyachukua.

Kwa mfano, wengine wana hoja za barabara katika maeneo yao, basi unaanza mapema kukaa na ile sekta ili waweze kuiona ile barabara na kuanza kuichukua. Jana mlizungumza hapa kuhusu barabara ya Mufti na mimi naifahamu, kwa hivyo huko ndiko mnakotakiwa kuanzia.

Pili, Mhe. Spika, mimi nakubaliana na hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija ya kutangaza bei kila mwezi, kama vile tunavyotangaza bei za mafuta. Nitashauriana na nitazungumza na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili tuone uwezekano wa kulitekeleza hili kwa pamoja ili wananchi wetu basi waweze kuelewa.

Lakini nataka niseme kwamba sasa hivi Zanzibar imekuwa, nitatoa mfano wa mchele, hatuna *iterm* moja ya mchele, unaweza kukuta kuna aina zaidi ya 10 za michele. Kwa hivyo, tutakaa na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili tuone ni jinsi gani tutakavyoweza kulifanya, ni wazo zuri na mimi nakubaliana na Mhe. Mwakilishi.

Nam. 97

Mshauri Mwelekezi na Uchangiaji wa Mapato ya Muungano

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ahsante Mhe. Spika, kabla sijajibiwa swali langu nambari 97, naomba uniruhusu niseme machache. Nauliza swali hili, kwa sababu kuna tabia ya baadhi ya Wajumbe kuja kuambiwa, mfano ukisema kuhusu Muungano ukaambiwa Muamsho. Hili suala halihusu muamsho, bali ni chombo cha wananchi na wanataka kujua faida gani wanayoipata kutoka kwa ndugu zao wa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nijibiwe swali langu nambari 97 lenye vipengele (a), (b) na (c).

Katika suala la mgawanyo wa mapato ya Muungano alitafutwa mshauri mwelekezi wa mambo ya uchangiaji na ugawaji wa mapato kati ya Serikali Mbili za Jamuhuri ya Muungano na ile ya Mapinduzi.

(a) Je, ni maamuzi gani yamefikiwa baada ya ripoti ya mshauri huyo.
(b) Je, Serikali haioni kwamba wananchi wa Zanzibar wanazidi kupoteza imani na muungano kwa kukosa maamuzi katika kushungulikia kero za muungano.

(c) Kama suala hili la utelekelezaji wa ugawanaji mapato kati ya Serikali zetu limeshindikana kwa miaka yote hiyo, kwa nini Serikali haitoi tamko kwa wananchi au hapa Barazani, kuwa suala hili limeshindikana na Baraza litoe maazimio ya njia mbadala ya kulishughulikia kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 97 lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 114 na 115 vya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, maamuzi yanayotakiwa kufanywa na serikali zetu mbili, ni yanayotokana na mapendekezo ya tume ya pamoja ya fedha, juu ya uchangiaji wa gharama za Muungano pamoja na mgao wa mapato yatokanayo na Muungano na sio mapendekezo ya washauri elekezi. Kwa sasa hakuna maamuzi yaliyofikiwa kuhusiana na mapendekezo ya tume ya pamoja ya fedha, kwa kuwa yanahitaji mazungumzo ya pamoja ya serikali zetu mbili (*SMT* na *SMZ*). Hali hii imetokana na kwamba *SMT* bado hawajayapitia mapendekezo ya tume. Lakini kwa taarifa tulizonazo, waraka juu ya mapendekezo hayo yanatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri hivi karibuni.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya kero za Muungano bado hazijapatiwa ufumbuzi, hata hivyo hakuna ithibati kuwa wananchi wamepoteza imani na Muungano wao kwa sababu kuna kero hazijapatiwa ufumbuzi. Muungano wetu ni wa udugu zaidi na ni wa miaka mingi na hatuwezi kupoteza imani. Tunavyoamini kuwa wananchi walio wengi wanachohitaji ni kupatiwa ufumbuzi wa kero hizo kwa haraka zaidi. Juhudi zitaendelea kwa serikali zetu za kutaka kuzipatia ufumbuzi wa haraka zaidi kero hizo.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema awali, suala la ugawanaji wa mapato ya Muungano kwa ukamilifu, katika serikali zetu mbili halijashindikana na linaendelea kushughulikiwa kupitia ngazi na vikao mbali mbali. Kwa sasa, serikali haioni haja wala faida ya kutoa tamko aliloshauri Mhe. Mwakilishi wakati kazi iliyo mbele yetu inawezekana, cha msingi ni kuendelea kukaa pamoja baina ya viongozi wa *SMZ* na *SMT* na kutoa maamuzi ya haraka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Tume ya pamoja ya fedha imekamilisha ripoti yake muda mrefu na kuikabidhi ripoti kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania.

- Kwa nini Serikali ya Muungano iliamua kukalia kwa muda mrefu wakati mambo hayo yanahusu uchumi wa nchi na wananchi wake.
- Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ni chombo cha wananchi na wananchi wanataka kujua maendeleo kwa kupitia sisi viongozi, hasa tunaotoka kwa wananchi badala ya kutoka majimbo ya Ikulu, tuwaeleze nini wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba arudie swali lake la pili taratibu, asiende kwa haraka hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ni chombo cha wananchi na wananchi wetu wanataka kujua maamuzi yanayotoka Tanzania Bara. Tume ya fedha ya pamoja ilikutana na kutoa maamuzi, lakini bado wananchi wetu majimboni kwetu wanatuuliza hasa sisi Wajumbe tunaotoka kwa wananchi, badala ya wanaotoka Ikulu. Wanataka kujua ripoti ya tume ya fedha ya pamoja ili tuweze kuona kilichopendekezwa, hata wananchi wetu katika majimbo yetu watakapotuuliza tupate jawabu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza SMT waliiomba tume ya pamoja ya fedha kuzipitia upya zile takwimu ambazo walizoziwakilisha katika ile ripoti. Kwa hivyo, tume ikazipitia upya zile takwimu na kuzifanyia masahihisho, au kuzi-*update* na baadae kuiwasilisha tena katika Serikali ya Muungano.

Kilichochelewesha mpaka Serikali ya Muungano kutotoa majibu yake juu ya ripoti ile, kwa kweli kwa sababu mimi sio mtumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, siwezi kuwasemea. Isipokuwa tu labda naweza nikadadisi baadae kutoka kwa Waziri mwenzangu angalau na mimi nifaidike. Nikishakudadisi naweza nikamnong'oneza Mheshimiwa kwamba kilichotokea ni hiki na hiki, lakini kwa sasa hivi siwezi kuwasemea. Ninachoweza kukisemea ni kile cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Pili, kilichopendekezwa ndani ya ripoti ya tume, kuna mapendekezo mengi ambayo tume hizo kwa mujibu wa katiba zinatoa ushauri kwa serikali mbili, hazitoi ushauri kwa Mabaraza yetu ya Kutunga Sheria na ndio maana Wawakilishi na Wabunge, hawajapata ile ripoti ambayo imependekezwa na tume. Lakini nina imani kwamba baada ya serikali mbili kuzipitia hizi ripoti, Waheshimiwa Wawakilishi na Waheshimiwa Wabunge vile vile wataweza kupata hilo pendekezo kama tulivyokubaliana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya uchambuzi ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali langu moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, alivyokuwa akijibu swali la msingi la Mhe. Jaku Hashim, Mhe. Waziri alisema kwamba serikali mbili hazijashindwa kuondosha kero za Muungano na wanaendelea kuzungumza ili kufikia muafaka. Lakini Wazanzibari wamekuwa wakilalamika sasa ni kipindi cha miaka 49 bila ya ufumbuzi, na kwa kuwa uchumi mambo ya fedha pamoja na nishati ni mambo ya Muungano. Hivi karibuni suala la gesi na mafuta kule Mtwara lilizua vurugu, jambo moja tu lilizua vurugu kwa kipindi kifupi sana. Lakini Wazanzibari miaka 49 tumetulia.

- Je, Mhe. Waziri amejifunza nini juu ya wananchi wa pande hizi mbili, nani mvumilivu na nani anapenda kupiga kelele pale akionewa.
- Hivyo, kuendelea kuwaacha Wazanzibari wakisubiri kuondoshwa kero huku miaka ikienda na mwakani tuna maadhimisho ya nusu karne ya Mapinduzi yetu. Tutegemee

nini kwa nusu karne ya Mapinduzi yetu juu ya suala hili la Muungano, mafuta pengine na mapato.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka niseme tu kwamba suala la uchumi na biashara sio masuala ya Muungano. Kutokana na sababu hiyo, Baraza la Wawakilishi lililopita lilifanya maamuzi kwamba masuala ya mafuta na gesi asilia yatolewe katika orodha ya Muungano. Serikali imelichukua lile wazo halikuwa baya na imeanza kufanya mazungumzo na Serikali ya Muungano. Juhudi mpaka kwa wakati huu Mhe. Spika, ni nzuri na kuna matumaini mazuri.

Nitakachowaomba ndugu zangu Wazanzibari, hatuna haja ya kufanya vurugu, hatuna haja ya kulumbana, haya masuala yanazungumzika na juhudi nzuri zinafanywa. Mawaziri wetu wawili hawa wa nishati wameanza vizuri sana, baadae yamekuja kwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais yamefanya matokeo mazuri sana. Kwa hivyo, hatuna haja ya kufanya vurugu tukilinganisha na ndugu zetu wengine wanavyofanya vurugu. Sisi tuendelee kuwa wavumilivu na wastahamilivu.

Katika sheria zetu zijazo, mimi nategemea kwa kiwango kikubwa sherehe za nusu karne zitakuwa nzuri, hivi sasa tumeshaanza kujiandaa ili Wazanzibari na dunia waweze kujua kuwa tumefikia miaka 50 ya Mapinduzi yetu na utulivu wetu na amani yetu ndani ya nchi yetu.

Nam 11

Uwekaji wa Nguzo za Umeme

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Katika ujenzi wa barabara mpya ya Bahanasa – Daya, Daya – Makongeni, Daya – Uondwe kumekuwa na ubadilishaji wa nguzo za Umeme kwa zile sehemu ambazo barabara hiyo itapitia na kutengeneza njia mpya ya umeme.

Kwa vile nguzo mpya ndizo zilizotumika pamoja na kuwa baadhi ya nguzo zilizobadilishwa ni nzima.

(a) Ni sababu gani zilizozifanya Wizara kuzirejesha nguzo zile Afisini badala ya kutumika kwa kupeleka umeme zile sehemu ambazo hazina huduma hiyo katika jimbo husika, pamoja na kuwa maombi hayo ya umeme yako Afisini kwao.

(b) Wizara haioni kuwa kufanya hivyo ni kuwaonea wananchi ambao wanahangaika huku na kule kutafuta njia ya kupatiwa huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 11 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- Mhe. Spika, hakuna kijiji ambacho kimepangiwa kupelekewa huduma ya umeme, lakini ikashindikana kwa sababu ya ukosefu wa nguzo, kila kijiji kilichopangiwa

kupelekewa huduma hiyo kitapelekewa kwa mujibu wa ratiba iliyopo. Pia napenda ifahamike kuwa si kila nguzo inaweza kutumika popote, taratibu za kiufundi huwa zinazingatia aina ya nguzo inayoweza kutumika katika sehemu husika. Nguzo iliyotolewa katika njia ya umeme mdogo "*low tension*" haiwezi kutumika katika njia ya umeme mkubwa "*high tension*".

- Lengo la serikali yetu kupitia wizara yangu ni kuhakikisha kuwa tunawapatia huduma ya umeme wananchi wote wa Zanzibar bila ya kupata usumbufu wowote. Kwa hivyo, tungewashauri wananchi kwamba wanapotaka kuungiwa umeme washirikiane na Shirika letu la Umeme

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, suali langu ni kwamba kwa zile nguzo ambazo zimeng'olewa, kuna nyengine zilitiwa mpya na nyengine zote zikatoka wizarani. Wakati jimbo langu lina vijiji vingi tu ambavyo bado havijapatiwa umeme. Swali ni kuwa kwa sababu tulisikia kuwa kampuni hii ya AT Yang inayotengeneza barabara zile tano za Mkoa wa Kaskazini, ilitoa fedha za kutosha ili mtandao ule wa umeme upite katika sehemu ambazo barabara hiyo haitopita.

Je, ilikuwa kuna ulazima gani hasa nguzo zile kurejeshwa ofisini wakati zinatoka katika Jimbo la Mtambwe A, pamoja na kuwa Mheshimiwa kasema kuwa nguzo hizi za *line* ndogo haziwezi kutumika tena, na kwa nini zisitumike wakati katika jimbo langu vile vile kuna sehemu zitakwenda *line* hizo ndogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba nguzo zilizotumika kwenye *line* ndogo, haziwezi kutumika kwenye *line* kubwa. Kwa hivyo, ni kweli tumeziondoa nguzo hizo hapo zilipokuwepo, lakini sio kwamba nguzo hizo tuzipeleke kwenye sehemu anayoifikiria, ni lazima tuende na utaratibu wetu wa shirika kwa kuangalia kupeleka *line* katika hiyo sehemu anayoiangalia yeye kwa mujibu wa taratibu. Sio tu kutoa nguzo hizi na kupelekwa katika kijiji hicho bila ya mpangilio ambao tunajipangia sisi Shirika la Umeme.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa sababu kuna taarifa kwamba kampuni ya AT Yang wameshalilipa shirika gharama zote, zikiwemo za kufidia zile nguzo zao. Kwa kuwa nguzo zile zilikuwa ni milki ya watu wa Jimbo la Mtambwe, sasa shirika kwenda kuzing'ang'ania nguzo zile kuzimiliki na kuziweka katika himaya yao. Je, huo si wizi wa wazi wazi kwa mali ya watu wa Mtambwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kwanza Mhe. Mwakilishi akumbuke kwamba wenye wajibu wa kusambaza umeme vijijini ni Shirika la Umeme peke yake. Kwa hivyo, ni kwamba pamoja na kuwa hiyo kampuni aliyoizungumza kuwa imeshalipia nguzo hizo walizoweka, lakini wajibu wetu ni kwamba baada ya kuziondoa nguzo zile, tuzipeleke Shirika la Umeme kwa ajili ya kupangiwa taratibu mpya na kupelekwa katika sehemu nyengine ambazo zitalingana na kupelekea huduma hiyo, kwa mujibu wa nguzo zenyewe zilivyo.

Nam. 86

Ahadi ya Kuezekwa Skuli ya Kitogani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub –Aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa tokea serikali ilipotoa ahadi ya kusaidia kuezekwa kwa skuli ya Kitogani. Licha ya kuahidiwa kuwa katika bajeti ya mwaka huu ahadi hiyo itatekelezwa, bado ahadi hiyo haijatekelezwa.

- Je, ni lini ahadi ya kuezekwa skuli ya Kitogani itatekelezwa.
- Hadi sasa serikali imepiga hatua gani katika kutekeleza ahadi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, kabla sijajibu swali ambalo liko mbele yangu. Jana hapa wakati natoa ufafanuzi wa swali nambari 58 kulijitokeza maswali ya nyongeza aliyouliza Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Saleh Nassor na niliahidi mbele yako Mhe. Spika, kwamba nitaleta vielelezo hivyo. Kwa hivyo, leo ninavyo hapa na sikuwahi kutoa *photocopy*, lakini naomba watu wako wakukabidhi na wapatiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, naomba wafanye *reference* kwenye ukurasa wa 6 kwa Bodi ya Mikopo ya Zanzibar na hii ni ripoti ambayo alisomewa Maalim Seif Sharif Hamad (Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais) katika ziara zake. Vile vile na hii hapa ni Ripoti ya Bodi ya Mikopo ya Tanzania, ambayo tulisomewa kwenye Kamati ya Ustawi wa Jamii, Sheria na Katiba kule Bungeni. Kwa hii vipaumbele vitajitokeza kwenye ukurasa wa 9, 10 na 11 Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma kwamba hichi ni chombo kikubwa, ambacho ni cha wananchi na wanakitegemea, kwa kweli maneno yanayozungmzwa humu wanayaamini.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika kwamba linalozungumzwa humu si kwa upande wa serikali tu, lakini hata kwa upande wa wenzetu Wawakilishi lazima yawe ni ya uhakika na yamefanyiwa utafiti wa kina, kwa sababu kupotosha hakutokani na upande wa serikali tu hata upande wa wenzetu Wawakilishi basi akizungumza kitu ambacho hakina uhakika ni upotoshaji katika chombo hichi kikubwa Mhe. Spika. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, sasa naomba ruhusa yako nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, ni kweli kuwa serikali ilitoa ahadi ya kuezeka majengo yote ya skuli ambayo yameshafikia hatua ya kuezekwa na kukabidhiwa kwa wizara. Pia, wizara huyafanyia ukarabati mkubwa majengo ya skuli iliyo katika hali mbaya. Skuli ya Kitogani ina jengo moja lenye madarasa manne ambalo linahitaji ukaratabati mkubwa ikiwemo kuezua na kuezeka upya, kupiga plasta na sakafu. Ni kweli kuwa serikali ilitoa ahadi ya kulifanyia ukarabati jengo hilo.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Katika Mpango Kazi wa Wizara, kazi za ukarabati wa majengo zimepangwa kufanyika katika robo ya tatu na ya nne ya mwaka wa fedha 2012/2013. Jengo la Skuli ya Kitogani limepangiwa kufanyiwa ukarabati katika robo ya tatu ya mwaka, yaani kipindi cha miezi ya Januari hadi Machi, 2013.

b) Kwa hivyo, hadi sasa wizara imelifanyia ukaguzi jengo husika na kufanya makisio ya gharama zinazohitajika kwa ujenzi. Jumla ya fedha zinazohitajika kwa ukarabati wa jengo hilo ni shilingi 35,000,000/-. Wizara inakusudia kuanza kulifanyia kazi jengo hilo mara tu tutakapoingiziwa fedha katika mwezi huu wa Januari, Machi, 2013.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu ambayo ameyatoa Mhe. Naibu Waziri kuwa bado hayasaidii tatizo langu na kunikosesha usingizi, kutokana na tatizo hili limekuwa la muda mrefu. Mhe. Naibu Waziri atakuwa tayari kuwajibika kama ahadi yake haitatekelezwa kama alivyotoa ahadi hiyo kiasi mara tatu kunipa ahadi hiyo mimi.

- Je, atakuwa tayari kuwajibika kama haitatekelezwa ahadi hiyo.

- Kwa kuwa Baraza hili limepitisha Sheria za Kulinda Watoto ikiwemo kusoma katika mazingira mazuri. Je, sababu zipi zilizopelekea wanafunzi kusoma wakati mvua inanyesha wakaondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama fedha zitatiwa kutoka Wizara ya Fedha kama ambavyo nilizungumza na likawa jengo hili halikufanyiwa matengenezo basi niko tayari kuwajibika. Vile vile kama ningeruhusiwa kupendekeza basi ningempendekeza Mhe. Mjumbe aikamate yeye hii nafasi.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali (b) sijapata jawabu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hebu lirejee swali lako la (b).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza hili limepitisha Sheria za Kulinda Watoto ikiwemo kusoma katika mazingira mazuri. Je, wizara yake inatekeleza vipi sheria hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, moja ni kuhakikisha kwamba watoto wetu wanasoma katika hali ya mazingira mazuri na ndio maana kwenye bajeti yetu atizame achukue *reference* ya ukurasa wa 22 kuna Mradi wa Uimarishaji wa Skuli za Msingi.

Mhe. Spika, pale kuna fedha karibu shilingi milioni 800 ambazo tumeziweka, ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanasoma katika hali nzuri ikiwemo hiyo kuezeka, kufanya matengenezo, kununua vikalio pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri alipotoa ahadi kipindi kilichopita kwa ajili ya kutengeneza skuli alisema kwamba kuna skuli ambazo zimepewa kipaumbele kwa sababu ziko katika hali mbaya sana, na kama kuna skuli ambazo ziko katika hali mbaya ndio maana zikapewa kipaumbele, kwa sababu zinaweza kuhatarisha amani.

Je, hizo skuli zilizopewa kipaumbele kwa sababu ziko hali mbaya na hizo zimepangiwa kwenye robo ya tatu.
Je, kama ziko kwenye robo ya tatu hicho kipaumbele kimetekelezwa au vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwenye bajeti yetu katika ukurasa huo wa 22 tuliahidi kwamba kuna skuli 150 ambazo tutazifanyia ukarabati katika bajeti hii na pia kuna skuli 15 ambazo tutazifanyia matengenezo makubwa.

Kwa kweli skuli hizi ambazo tumezitaja Mhe. Spika, ndizo skuli ambazo tumezipa kipaumbele kwa mwaka huu. Kwa hivyo, kama nilivyoahidi kwamba kwenye robo ya tatu na nne ndipo skuli hizi tutaanza kuzifanyia kazi.

Nam. 9

Matengenezo ya Barabara ya Bagamoyo – Kele

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Barabara ya Bagamoyo – Kele iliyopo katika Jimbo la Mtambwe imeanza kutoa huduma ya kuridhisha katika siku za kiangazi tokea serikali ilipojenga daraja pale Mto Mkuu.

Serikali imejipanga vipi katika kuifanyia matengenezo barabara ile, ili iweze kupitika ipasavyo na kwa muda wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo:-

Mhe. spika, ni kweli barabara ya Bagamoyo – Kele ni kiungo muhimu kwa wananchi wa Jimbo la Mtambwe. Matumaini yetu ni kwamba kuimarika kwa daraja ya Mto Mkuu kungeweza kuimarisha huduma za usafiri katika eneo lote la jimbo hilo.

Pamoja na changamoto nyengine hivi sasa barabara hiyo inafanyiwa matengenezo kupitia Mfuko wa *TASAF* na pale ambapo fedha hizo zikishindwa kumalizia jambo ambalo hatulitegemei basi tutaingiza barabara hiyo kama ni mradi wa dharura katika mipango ya Miradi ya Mfuko wa Barabara, ili kuikamilisha kama tulivyoahidi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ahsante kwanza nianze kwa kutoa shukurani kwa niaba ya wananchi kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia *TASAF* kwa kupata msaada wa kutengeneza barabara hii kama Mhe. Naibu Waziri alivyoeleza.

Lakini Mhe. Spika, kwa kuwa fedha zilizopatikana zilikuwa hazitoshelezi kwa kuitengeneza barabara yote nzima, na kwa sababu Kampuni ya *AT Yang* katika kuchimba kifusi kwenye eneo la barabara hiyo, ilibidi ifanye *grading* kwa sehemu kubwa, ambayo hivi sasa ikinyesha mvua haipitiki.

- Je, Mhe. Waziri haoni kuwa kusubiri mpaka ikatiwa katika makisio na mvua hizi zinazofuatia na kutokana na sehemu hii ambayo hii kampuni yetu iliyofanya *grading* njia hii itakuwa haitumiki tena na wakati fedha nyingi zimeshatumika kwa sehemu ya barabara hii, ili iweze kupitika.

- Kwani haiwezekani kwa hivi sasa sehemu hii ndogo iliyofanyiwa *gradding* na Kampuni ya *AT Yang* wizara ikazungumza nao, ili wachukue jukumu la kuitengeneza wakati wametumia sehemu kubwa ya Jimbo la Mtambwe kwa kuchukua kifusi kwa barabara ambazo inazitengeneza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, imani yetu ni kwamba utaratibu ule tuliofikia katika hatua ya utekelezaji wa barabara hii, basi tukiweza kukamilisha zoezi lile na kama kutakuwa na mapungufu yoyote yanayotokana na matumizi, tunaamini kwamba Kampuni ya *ASHAN* kama tulivyoweza kuzungumza huko nyuma na tukakubaliana na mambo mengine ya msingi nalo hili halitokuwa kikwazo.

Lakini matarajio yetu ni kwamba kuona barabara hii yote yenye urefu wa kilomita 4.5 tunaweka kifusi na kuishindia vizuri na kama kutakuwa na mahitaji katika maeneo maalum kama haya anayoyaeleza Mhe. Mwakilishi, basi tutazungumza na wenzetu na kuona *concern* hiyo inatekelezwa kadri iwezekanavyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea kidogo. Kwa kuwa tunao mpango wa bajeti ya mwaka unaokuja 2013/2014 kuitengeneza kwa njia ya kiwango cha kifusi njia ya kutoka Uondwe hadi Nyali. Naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tutaingiza sehemu hiyo, ili iende pamoja na ile barabara inayoungana nayo. *(Makofi)*

Nam. 90

Mchango wa Sekta ya Utalii na Michezo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Tokea kuanza kwa sekta ya utalii nchini kumekuwa kunatolewa takwimu nyingi kuhusu mchango wa sekta hii kwa maisha ya kawaida ya wananchi wetu wa Zanzibar. Wengi wao hawana taarifa za kutosha kuhusu mchango wa sekta ya utalii nchini katika maisha ya kawaida ya mwananchi hasa katika maeneo ya pwani na vijiji vyake na maeneo ya hifadhi na rasilimali adimu ambayo sekta hii imejiimarisha.

(a) Je, ni watalii wangapi wametembelea Zanzibar kwa kipindi cha miaka 2 iliyopita 2011/2012 na ni fedha kiasi gani zimepatikana.

(b) Je, kati ya watalii hao ni wangapi waliotembelea Hifadhi ya Msitu wa Jozani na wananchi wa Jozani na Pete wamefaidika vipi na rasilimali hiyo.

(c) Je, wizara ina mipango gani ya kuongeza vivutio vyengine kwa wageni kama wanyama mfano nyumbu, swala, twiga ili kuongeza mapato zaidi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 90 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- Kwa kipindi cha miaka 2 iliyopita Zanzibar ilitembelewa na watalii 344,294. Kwa mujibu wa taarifa ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) Jumla ya shilingi Bilioni 92.4 zilikusanywa katika mwaka 2010/11 kutokana na vianzio mbali mbali. Kati ya makusanyo hayo shilingi Bilioni 72.7 zinatokana na Biashara ya Utalii, na Mwaka 2011/12, *ZRB* imekusanya jumla ya shilingi Bilioni 120.5.

b) Kati ya watalii 175,065 waliotembelea Zanzibar mwaka 2011, jumla ya watalii 18,549 wametembelea Hifadhi ya Jozani. Kwa mwaka 2012, jumla ya watalii 18,802 wametembelea msitu huu, na wananchi wa Jozani na Pete walifaidika kwa kupata gawio linalotokana na ada ya kiingilio inayopatikana wakati watalii wanapotembelea hifadhi hiyo.

c) Serikali kupitia wizara yangu haina mpango wa kuleta wanyama kama vile swala na twiga na wengineo katika vituo vya wageni, isipokuwa Kamisheni ya Utalii inashajihisha wananchi katika maeneo yao kuibua vivutio kama vile mapango, maeneo ya kihistoria, mashamba ya viungo na kadhalika, ili kutekeleza dhana ya utalii kwa wote. Aidha, serikali imefungua milango kwa muwekezaji yeyote ambaye mwenye nia ya kutekeleza katika nyanja hiyo, kuongezeka kwa vivutio vya utalii kutakuwa na faida kwa nchi na wananchi wake kwa kuongeza nafasi za ajira na mapato.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante. Je, serikali ina mpango gani wa vijiji ambavyo viko kwenye ukanda wa pwani vinanufaika vipi na sekta hiyo, ili yasijekutokea kama yaliyotokea Mtwara.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu karibuni itatangaza Kamati ya Utalii za Wilaya zote 10 za Zanzibar. Katika kamati hizo zitaundwa na wenyewe wa wilaya husika na maeneo ya utalii, kutakuwa na utaratibu wa kuona namna gani vyanzo vya utalii wananchi watafaidika vipi katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mafupi, lakini yamelenga kwenye maswali ambayo yameulizwa. Mhe. Spika, kwenye majibu ya swali la nyongeza la Mhe. Jaku Hashim Ayoub tayari ameshalijibu swali langu, isipokuwa nilitaka nimuulize kuhusu Mji Mkongwe, kwa sababu vyanzo vya mapato havitokani kwenye vijiji tu, lakini pia kwenye eneo lenye heshima kimataifa la Mji Mkongwe anajua Mhe. Waziri linachangia kiasi gani.

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Spika naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Mhe. Spika, ili nchi yetu iweze kufaidika na Sekta hii ya Utalii zaidi kama ambavyo imeelezwa kwenye swali na majibu ya Mhe. Waziri ni muhimu mno kudhibiti mapato yanayotokana na uingiaji wa watalii.

Vile vile tunajua sote kwamba kwa hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashindwa kupata mapato yote kutokana na watalii wengi kupata *visa* kutoka nje ya nchi na mapato haya yanayopitia katika Ofisi za Kibalozi za Tanzania nchi za nje yamekuwa yakilalamikiwa sana kwamba hayaingii katika Hazina ya Zanzibar wakati utalii si suala la Muungano.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikia wapi katika hatua za kulimaliza suala hili, ili mapato yote yanayotokana na watalii wanaokuja Zanzibar wanaochukua visa zao katika Ofisi za Kibalozi nchi za nje yaweze kuingia katika Hazina ya Zanzibar na wala yasitumiwe kwenda kufaidisha Tanganyika, ambao wao wanazo mbuga zao na wanapata mapato yao ya utalii. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naomba nikubaliane naye kwamba Mji Mkongwe ni eneo ambalo Utalii wetu wa Zanzibar unategemea tena ni hazina moja kubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe pamoja na mimi tushirikiane, ili kuhakikisha kwamba Sekta ya Utalii katika Mji Mkongwe inaimarika zaidi kwa maslahi ya wananchi wa Mji Mkongwe pamoja na wananchi wetu wa Zanzibar.

Kuhusu swali lake kwamba serikali imefikia wapi katika suala la mapato yanayotokana na *visa*. Mhe. Spika, ni kweli kwamba hili ni eneo moja ambalo wizara yangu kupitia Kamisheni ya Utalii ilikuwa ikilizungumza kwa muda mrefu pamoja na wenzetu wa Uhamiaji, kwamba tunalo tatizo linalohusiana na *visa* kwa wale watalii wanaokuja Zanzibar.

Hivi karibuni tumefanya kikao pamoja na Kamisheni ya Utalii na Uhamiaji kwa ajili ya kulizungumza suala hili na tumekubaliana kwamba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa nayo tuishirikishe katika kuandaa utaratibu bora na imara, ambao utahakikisha suala hili linaifaidisha Zanzibar. Kwa hivyo, bado tunaendelea kulizungumza na tuna imani kwamba si muda mrefu ufumbuzi wake utapatikana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- Ninavyofahamu mimi ni kwamba watalii wako kwa madaraja, yaani kuna daraja la kwanza na wengine huwaita vishuka. Je, ni watalii wepi wanaokuja zaidi nchini kwetu wa daraja la kwanza au vishuka.

- Ujaji wa watalii unakuja kwa njia mbali mbali; wako wa *package* wanaochukuliwa fedha zao na kuja kulipwa moja kwa moja kwenye taasisi inayohusika na wapo wanaokuja moja kwa moja na kulipa wenyewe. Je, katika njia mbili hizi ipi ni bora, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa hivi sasa watalii wengi wanaokuja Zanzibar ni wale wa daraja la chini. Kwa kweli jitihada inafanywa kuona kwamba tupate watalii wachache wa daraja la juu, ambao wanatumia zaidi, na watalii wa daraja la chini wanakuja wengi, lakini hawatumii sana nchini na kwa hivyo mapato huwa kidogo.
Kwa hivyo, tunachokifanya sasa ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira na kuu-*promote* utalii wetu katika nchi ambazo watalii wa daraja la juu watakuwa wanakuja. Mhe. Spika, jitihada hiyo inaendelea na tunaamini kwamba itafanikiwa.

Kuhusu suala la *package tours* na watalii mmoja mmoja. Mhe. Spika, hutegemea na aina na pahala ambapo unachukua. Kwa mfano, kama unachukua maeneo ambapo watalii wa daraja la juu unapata kwa *package*, basi twabaan utapata watalii wengi zaidi. Kwa hiyo, hiyo inategemea na aina na pahala ambapo watalii hao wanatoka.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru na hapa ndio mwisho wa maswali yetu. Tunaendelea.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti Maalum ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika juu ya Uchunguzi wa Utendaji wa Shirika la Umeme Zanzibar

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyokubaliana jana kwamba leo ni zamu yake Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*), kwa ajili ya kufanya majumuisho kwa hoja ile ya ripoti ya kamati.

Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika). *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Spika, awali naomba nikushukuru tena kwa mara nyengine kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako kwa nia ya kufanya majumuisho yenye kufunga mjadala juu ya Ripoti ya Kamati yetu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kabla ya kuanza naomba kuwataja na kuwashukuru sana wale wote waliochangia ripoti hii, ambao walikuwa ni jumla ya Wajumbe 25 wa Baraza lako tukufu. Kwa hivyo, naomba niwataje majina yao kama ifuatavyo:-

- Mhe. Ali Salum Haji,
- Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa,
- Mhe. Salmin Awadh Salmin,
- Mhe. Saleh Nassor Juma,
- Mhe. Mansoor Yussuf Himidi,
- Mhe. Ismail Jussa Ladhu,
- Mhe. Asha Bakari Makame,
- Mhe. Nassor Salim Ali,
- Mhe. Mohammed Mbwana Hamad,
- Mhe. Mohammed Haji Khalid,
- Mhe. Ussi Jecha Simai,
- Mhe. Abdalla Moh'd Ali,
- Mhe. Mgeni Hassan Juma,
- Mhe. Hassan Hamad Omar,
- Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi,
- Mhe. Hija Hassan Hija,
- Mhe. Makame Mshimba Mbarouk,
- Mhe. Rufai Said Rufai,
- Mhe. Farida Amour Moh'd,
- Mhe. Fatma Mbarouk Said,
- Mhe. Hamza Hassan Juma,
- Mhe. Abdalla Juma Abdalla,
- Mhe. Mbarouk Wadi Mussa,
- Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na
- Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niwashukuru sana Wajumbe wote ambao wamechangia hotuba hii na wale ambao hawakuchangia, lakini kwa namna moja ama nyengine wameoneshwa kuguswa na ripoti yangu. Kwa kweli nawashukuru sana na hasa kwa kuwa mbali ya mawazo yao, lakini takriban Wajumbe wote wameonesha hisia za uwakilishi wa wananchi wao waliowachagua na kuwaleta katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mbali ya kuwashukuru Wajumbe, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi ambao mara kwa mara walikuwa wakitupa mashirikiano makubwa, pia walikuwa wakioneshwa kutuunga mkono katika suala zima wakati kamati yetu ilipokuwa inalifanyia kazi suala hili. Kwa kweli kuanzia tangu pale kamati ilifanya kazi ya kuchunguza na hadi hatua ambapo leo nasimama kuwasilisha ripoti hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, takriban michango ya Wajumbe ililenga katika maeneo matatu makubwa. Eneo la kwanza la michango ya Waheshimiwa Wajumbe, ililenga katika kuipongeza Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kwa namna ilivyofanya kazi kubwa sana na hatimaye kuwasilisha ripoti katika Baraza.

Takriban asilimia mia moja ya Wajumbe waliipongeza kamati na wala hakuna mjumbe hata mmoja miongoni mwa waliochangia aliyeiponda kamati au aliyesema kwamba kamati haikufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mchango wa aina ya pili ulilenga kwa Wajumbe katika kusisitiza yale yaliyokuwemo kwenye ripoti na mengine ambayo wao wanayajua zaidi ambayo hayamo kwenye ripoti. Kwa hiyo eneo la pili la michango ya wajumbe ililenga katika kusisitiza yale yote yaliyokuwemo kwenye ripoti.

Jambo la tatu katika uchangiaji Mhe. Spika, kulikuwa na mambo machache sana ambayo yalihitaji ufafanuzi ambayo yanatokana na ripoti yetu.

Kwanza ningependa nianze na lile la mwisho alilolitaka kufahamu Mhe. Hamza Hassana Juma kwamba Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya GECCO ina wanahisa wangapi au wanaomiliki Kampuni ya GECCO ni akina nani.

Naomba niseme kwamba kwa mujibu wa orodha tuliyoipata kutoka kwenye Ofisi ya Mrajisi wanaomiliki hisa ambao ndio Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hili ni wafuatao:

JINA	HISA
• Ndg. Mohammed Thuwein	35
• Ndg. Habibu Mnyaa	40
• Ndg. Ali Abeid Haji	15
• Ndg. Hamidu Saidani Ali	20
• Ndg. Hassan Ali Hassan	15
• Ndg. Masoud Khamis Said	25
Jumla ya Hisa Zote zilizouzwa	**150**

Kwa ufupi wanaomiliki Hisa Katika Kampuni hii ni hao niliowataja.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningependa nilitolee ufafanuzi ni hoja itokanayo na pendekezo la 6 na pendekezo la 7 la ripoti yetu. Nianze na pendekezo la 6 ambalo lilihusu juu ya suala la majenereta. Kamati ilisema kwamba kwa sasa majenereta ni mzigo kwa shirika lakini pia majenereta yale 32 yamekuwa ni mzigo kwa serikali.

Mhe. Spika, ni ukweli na tukubaliane kwamba Shirika limeshindwa kuyaendesha majenereta 32. Limeshindwa kwa sababu wamesema ili waweze kuyahudumia majenereta waliomba serikalini kwamba serikali ikubali kuwapa milioni 500 kwa kila mwezi, hilo ni la kwanza. Lakini la pili kama ikiwa serikali haitotoa fedha hizo basi serikali iwaruhusu shirika wapandishe bei ya umeme kutoka unit kwa unit moja kwa shilingi 560.

Mambo hayo mawili ambayo ndiyo yaliyokuwepo sasa kwamba ili shirika waweze kuyaendesha majenereta yafikie katika lile lengo ambalo ndilo lililofanya yanunuliwe ya kuzalisha umeme wa dharura kwamba ama serikali ichangie au waruhusiwe wao waongeze bei ya umeme. Tupime mambo yote mawili kwa wakati mmoja tutaona kwamba yana uzito wake na yana changamoto zake katika utekelezaji. Kwa ufupi ni kwamba kwa sasa shirika halina uwezo wa kuyaendesha majenereta hayo.

Mhe. Spika, tukumbuke kwamba majenereta haya yalinunuliwa kwa fedha nyingi sana kwa bola milioni 12 ndio majenereta haya yalinunuliwa. Kamati ilitoa mapendekezo matatu hatukutoa pendekezo moja.

Pendekezo la kwanza kwamba basi serikali ikubali kuubeba mzito huu kwa kutoa shilingi milioni 500 kwa kila mwezi.

Pendekezo la pili basi kutafutwe utaratibu ambao utawezesha majenereta yale yatumike kwa teknolojia ndogo. Wale wenyewe walitwambia kwamba upo uwezekano wa majenereta yale

kutumia katika disel ya kawaida. Lakini wakatupa angalizo kwamba hayatokuwa na muda mrefu wa kuishi. Ila kama kutababidilishwa teknologia huenda majenereta yale yakatumika kwa disel ya kawaida na majenereta yale yakafanya kazi.

Pendekezo la tatu tulisema kwamba basi yote mawili yasipowezekana tufanye lile linalowezekana nalo ni kwamba majenereta yale yauzwe ili yatafutwe majenereta ambayo serikali na shirika ambayo watakuwa na uwezo wa kuyagharamia.

Kwa hivyo hayo ndio mapendekezo yetu matatu, naamini moja kati ya matatu hayo upo uwezekano wa serikali kulichukua moja na kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, hoja itokanayo na pendekezo la saba kwamba tulipendekeza iundwe Tume Huru itakayochunguza. Kwanza inavyosemekana kwamba chanzo cha tokeo lile ni kuripuka, tuanzia hapo tu ni kuripuka, lakini hatuambiwi chanzo cha kuripuka ni kitu gani. Lakini Kamati ilipofanya uchunguzi ilibaini kwamba chanzo cha kuripuka ni uzembe, uliosababishwa na mfanyakazi ambaye hatukuambiwa kwamba aliambiwa akaezeke juu kibanda alipopanda pale akadondosha nyundo iliyoangukia juu ya tenki ambalo lilikuwa lina kiyoo ikapasua nyundo ile, gesi ikapita na ndio hicho kilichosababisha hayo yote.

Sasa kama chanzo ni hicho Mhe. Spika, tusione kwamba hili ni hili tu, hili ndio lililopelekea gharama ya kufanyiwa matengenezo, hili ndilo lililopelekea Unguja kukosa umeme miezi mitatu, hili ndilo lililoathiri maisha ya wananchi na hili ndilo lilopelekea kununuliwa majenereta ambayo tutaeleza ni kwa vipi. Kwa hivyo katika suala hili ambalo sasa linaoneshea lina utata, ni lazima uchunguzi upite. Ili wananchi waweze kujua chanzo cha matatizo ni kitu gani. Ni *crisis* kubwa ambayo haiwezi ikaachiwa ikapita hivi hivi.

Mhe. Spika, sababu ya kwanza ya tatizo hili ni uzembe kama tulivyosema. Lakini tatizo lote hili lililotokezea Kamati ilipohoji shirika, shirika hawana taarifa juu ya haya yaliyotokea, walatu tupeni tu taarifa ya kuweza kuangalia haya matatizo yalianzia wapi yakenda wapi, mnatumia nini na nini, hawana. Kitu ambacho hakikubaliki. Kwa vyovyote vile kama shirika liko makini na serikali iko makini kwa vyovyote wangeliandaa ripoti japo ya mkononi. Lakini kwa *crisis* kama hii halafu ukasema kwamba hakuna ripoti yoyote, fedha nyingi zinatumiwa. Sisi hilo hakutaliani nalo. Lazima uchunguzi upite ili baadae kijulikane nini kilichotokea.

Mhe. Spika, sambamba na hilo kwa kuwa suala hili la mripuko ndio lililopelekea majenereta. Na suala la majenereta nalo vile vile linautata kwamba serikali mara nyingi tumekuwa tukipata maelezo tofauti. Mara ya kwanza liliulizwa swali hapa tukaambiwa kwamba majenereta yale yamenunuliwa kwa msamaha wa madeni wa MAN TRAC.

Mara ya pili tukaambiwa mpaka tunakwenda kwenye kikao tukaambiwa kwamba majenereta yale yaliletwa tu na wahisani wakayaweka. Ndio taarifa tulizozipokea, lakini baada ya uchunguzi tulioupitisha ni kwamba mkataba wa ununuzi wa majenereta yale ni baina ya ZECO na Kamapuni ya MAN TRAC. Tulitia kiambatanisho cha 95 humu kuelezeeni kwamba nani aliyenunua majenereta yale. Kwa hiyo majenereta yale yamenunuliwa na Shirika letu la ZECO kama mnunuzi na MAN TRAC kama muuzaji.

Kwa hiyo katika mazingira hayo maana yake nini, maana yake sheria zilizotakiwa zitumike ni sheria za Zanzibar kwa sababu Shirika la ZECO ni Shirika la Zanzibar. Hakuna namna nyengine kwamba sheria zilizopaswa zitumike ni sheria za manunuzi ya Zanzibar ya mwaka 2005. Tunasema kwamba hata ununuzi uliohusiana na hali ya dharura sheria imekiukwa. Kwa msingi huo ndio tukajenga hoja kwamba lazima suala hili lifanyiwe uchunguzi wa kina ili hatimae ijulikane.

Naomba nikumbushe kwamba marekebisho ya umeme yaliligharimu shirika bilioni moja na nusu na ununuzi wa majenereta uligharimu dola milioni 12. Hatuwezi tukayawacha mambo haya yaende hivi hivi, kwa sababu Mhe. Spika, mambo haya si mageni. Katika nchi yetu hii hii Tanzania tuna kesi maarufu ya ununuzi wa Rada, hakuna anayeweza kufikiria lakini yametokea. Rada ikanunuliwa nyote mnafahamu, matokeo yake wazee wa vijisenti wakazuka. Lakini vile vile hasa katika ununuzi wa masuala ya majenereta tu, tutakumbuka ile kesi maarufu iliyomfanya hata Waziri Mkuu wetu aweze kujiuzulu suala la ununuzi wa majenereta ya Rich Mond na kuna kesi ya Rich Mond sijui mambo ya Simbiond, sijui mambo ya nini, yote ni matatizo kama haya yanayojitokeza.

Mhe. Spika, Kamati imependekeza uchunguzi huru upite ili hatimae tuelezwe nini hasa kilichotokea na ukweli wa mambo uwekwe wazi kwa sababu Kamati yako yaikuwa na uwezo wa kwenda ndani zaidi na umbali zaidi katika hilo. Katika hilo Mhe. Spika, Kamati ilikuwa na *interest* ya kwenda mbali zaidi kama ilivyoelezwa jana lakini kwa mujibu wa muda uliotupa hatukuweza kufanya kazi hizo. Tuliacha kwenda EWURA, tuliacha kwenda Ubalozi wa Norway, tuliacha kwenda Afrika ya Kusini ambako nguzo zinanunuliwa na mita zinanunuliwa.

Mhe. Spika, kesi ya Bara ilipotokea kule kuna watu vile vile walisema kwamba nguzo zinanunuliwa Afrika ya Kusini lakini kumbe nguzo zinanunuliwa Njombe zinapitishwa Mombasa zinarudi tena Tanzania. Hiyo ndio michezo iliyopo kwa hivyo na Kamati yako hii lipaswa kufatilia kote huko ili kujiridhisha lakini bahati mbaya muda hatukuwa nao, tulichoweza kukifanya ni hicho.

Mhe. Spika, kuna hoja nyengine ilizuka kwamba basi kwanza washtakiwe au kwanza wahojiwe wale ambao walitoa pesa nyingi lakini risiti walizopewa ni risiti zenye pesa kidogo. Hasa kwanza ikimlenga ndugu Makungu. Mimi ningelipenda Waheshimiwa tusomeni vizuri ukurasa wa 17 wa ripoti tuusomeni vizuri na tuusome halafu tuufahamu tumekusudia nini. Kwa sababu hatukupenda kila siku tuwe tunakuja kufahamisha jambo hilo hilo. Napenda msome baadae mfahamu tumekusudia nini.
Ninachosema kwamba hizo barua zilizosemwa kwamba ni za kuandikia, zile ni barua za ubabaishaji tu, hakukuwa na barua kama hiyo. Naomba msome mujiridhishe. Lakini katika hilo hilo naomba niseme kwamba kawaida ya wale wote tunaokwenda hospitali yule daktari anayekupa dawa mara nyingi ndiye unayempa fedha. Hospitali ni nadra sana kumuona keshia. Kwenda hospitali ni nadra sana kusema kwamba nimeshachukua dawa nataka kwenda kwa keshia ni nadra sana. Anayekupa panadoli 500 unachukua 500 unampa. Katika suala hili kwamba mtu akupigie tathmini bwana nenda kwa Omar Ali Shehe yeye ndiye aende akakufanyie mahesabu ni rahisi sana yule aliyekufanyia mahesabu akikwambia mpe pesa mara nyingi kwa

siye waswahili tuliokuwa hatujui kitu ni rahisi sana pesa kutumbukia hapo na hasa kwa mazingira ya watu wetu.

Nakubaliana kwamba hawa wahojiwe lakini hili liwe ni la pili, la kwanza liwe ni lile fedha zimekwenda wapi na nani kachukua fedha na kwa nini kachukua. Ni kitu ambacho kama hivi tunavyosema milioni 37 unatoa milioni 37 unaandikiwa risiti ya milioni 2 lakini kazi inayofanywa ni ya milioni 37 kazi inayofanywa ni ya fedha Ile ile, ingelikuwa fedha haikutimia kwa milioni mbili, ah! Basi kazi ingeliendelea kukaa kwa sababu pesa hazikutimia. Lakini risiti unapewa ya milioni 2 kazi unayofanyiwa ni ile ile ya milioni 37, hizi nyengine zilizopita zimekwenda wapi na kwa nini ikiwa pesa hazikutimia kwa nini kazi isisimame kwamba fedha hazikutimia.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kazi zote zilizofanywa na Kamati zilifanywa kwa mashirikiano makubwa sana na *management* ya shirika. Tangu tulivyofanya vikao na wananchi *management* ya shirika ilikuwepo, vikao vyote vya mahojiano na wafanyakazi *management* ya shirika ilikuwepo. Safari zote za Unguja kwenda minara kwenye mashamba na mahoteli *management* ya shirika ilikuwepo. Ilitaka kutokezea siku ya kwanza ambapo tulianza kazi Pemba kwamba meneja wa shirika hakuwepo, tulimlazimisha lazima awepo Pemba na siku ya pili tunamshukuru kwamba siku ya pili alikuwepo na hakuondoka mpaka siku tuliyoondoka. Na hata tulivyokwenda Dar-es-Salaam siku ya kwanza kenda MAN TRAC alituletea afisa wake. Lakini kwa kujua umuhimu wake tukamwambia tuko tayari turudi ili siku nyengine tuje twende na wewe MAN TRAC. Kwa maana kwamba hatukutaka yote yanayotokea iwe ni Kamati tu imejifungia peke yake tulitaka chchote kinachotokea wao wawe ndio mashahidi wetu.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza hili Mhe. Spika, hatuwezi tukawaweka mashahidi katika chemba hii. Lakini pahala ambapo tunaweza tukawaita mashahidi ni kwenye Kamati na watu hawa tukawaita kwenye Kamati, wote tuliwaita. Naomba mrudie kwenye kumbukumbu za mahudhurio kwamba kila siku ya Mungu tulikuwa tukichukua mahudhurio nani yupo na nani hayupo.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba tulichokiandika ndicho kilicho, hakuna maelezo mengine. Mhe. Spika, tulichokiandika kwenye ripoti hakuna chengine kitakachotokea zaidi ya tulichokiandika kwenye ripoti. Mengi yametokea na hata wao hata Meneja wa Shirika, mwengine mwingi alikuwa akishangaa kwamba aah! Kumbe mambo yako hivi. Ndiyo. Ninachotaka nisisitize kwamba tulichokiandika ndicho kilichopo hakuna maelezo ya ziada.
Mhe. Spika, wakati tunafanya kikao na wafanyakazi hasa Unguja Kamati yako ilipata wakati mgumu sana. Naomba niseme kwamba tulipofanya kikao na wafanyakazi wote wa Shirika Unguja tuliwaomba wenzetu wa *management* watoke nje. Katika eneo hilo tu ambalo *management* hawakukuwepo. Tulitaka waondoke kwa sababu tulitaka wafanyakazi wawe huru zaidi katika kujieleza. Nataka niwaeleze wafanyakazi waligoma kutoa ushirikiano kwanza kwa sababu walisema kwamba nyie watu wa Baraza la Wawakilishi hamna chochote. Naomba niwakumbe wenzangu na naomba niwambie Baraza la Wawakilishi, mnachotaka kuja hapa ni kutuchonganisha na kututafutia balaa. Kwa kumbukumbu zao wao wanasema kwamba iko Kamati kama hii iliwahi kwenda na ikawahoji lakini hakuna chochote kilichotokea isipokuwa ni balaa zaidi kila siku zikiendelea.

Mhe. Spika, nikiwa kama Mwenyekiti, wa Kamati niwachukuliwa ahadi kwamba sijui matokeo yatakuwa ni yepi katika utekelezaji lakini niliwaahidi wafanyakazi kwamba mtakachotwambia ndicho tutakachokiripoti. Nikenda mbali zaidi kwamba sisi tukiwa kama Wawakilishi tutahakikisha kwamba serikali inapendekeza mapendekezo yenu.

Nilisema hivyo nikiwa na *confidence* sijui niliipata wapi lakini nilisema kwamba tutahakikisha kwamba serikali inatekeleza. Kwa sababu naamini na serikali nayo *interest* yake ni kuona kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, kwa hivyo wafanyakazi walikuwa huru kutueleza na katika hili kwa kweli naomba niwashukuru tena kwa mara ya pili wafanyakazi. Mhe. Spika, unapojifungia katika jengo hili fikra zinaweza zikakueleza kwamba ni nyie tu humu ndani ndio mnaoonana na kusikilikana. Lakini kama unataka kujaribu kwamba unachokisema wananchi waliokuwepo Micheweni wanakusikia hebu jaribu sema halafu utoke nje. Ukitoka nje ndio utakapojua kumbe sio sie peke yetu humu tunaozungumza na wanaotusikiliza. Kuna na wananchi Zanzibar nzima wanatuangalia na wanafuatilia kwa karibu mambo yanavyokwenda.

Ninachotaka kusema Mhe. Spika, wananchi wamekuwa wakifatilia mjadala huu kwa karibu sana na wamekuwa wakiguswa na suala hili kwa kweli kwa karibu sana. Ninachotaka niseme kwamba Mhe. Spika, ripoti hii ambayo ni ya tatu ni kipimo na ni kigezo chengine kwetu sisi Wawakilishi pamoja na serikali yetu. Zaidi nitasema kwa sasa ni kipimo kwa upande wa serikali kwamba leo hii tunautua mpira kama ni mpira basi tunauelekeza katika goli la Mhe. Mohammed Aboud (Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais), tunautua mzigo huu kwa serikali.

Katika suala hili la utekelezaji wa dhana hii ya Utawala Bora naomba nitumie fursa hii Mhe. Spika, nimsifu sana, sana, sana Mhe. Mrisho Jakaya Kikwete, akiwa Rais wa Jamuhuri ya Tanzania lakini pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa namna alivyokuwa yupo makini na yupo serious sana katika kupambana na mambo haya ya ufisadi na ubadhirifu. Nasema hivyo kwa nia nzuri sana na wala sitaki niseme vibaya kwa sababu Chama cha Mapinduzi ndio kinachotawala. Kwa hivyo tuna wajibu wa kusema mambo yanayohusiana na suala hili. Naomba nimpongeze sana kwa kweli.

Nimekuwa nikivutika mno na namna anavyoshughulikia mambo haya. Nilitamani sana Mhe. Spika na Msaidizi wake Makamo Mwenyekiti wa CCM Zanzibara ambaye ndiye Rais wa Zanzibar naye afuate nyayo za Bosi wake. Ingelipendeza sana na ingelikufurahisha sana hasa kwa kuamini kwamba ilani inayotekelezwa ya Chama cha Mapinduzi ni Ilani moja, sera zinazofuata ni sera za Chama cha Mapinduzi kwa hivyo kama ikiwa Mwenyekiti anafanya hivyo na Makamo Mwenyekiti, wangelikipa sura nzuri sana Chama cha Mapinduzi Bara na Visiwani.

Naomba kwa unyeyekevu wa hali ya juu ripoti yetu ifanyiwe kazi Mhe. Spika, ripoti itakapofanyiwa kazi Mhe. Spika, itawarudishia matumaini wananchi wetu na itajenga haiba ya wananchi kwa serikali yao na itajenga haiba kwa Baraza lao hili.

Mhe. Spika, jambo jengine kabla sijamalizia naomba niseme kwamba katika siku mbili za karibuni kumekuwa na namna fulani ya kueletewa vitisho. Mhe. Hija Hassan Hija jana kazungumza. Kwamba nitaoneshwa, mimi naamini kwamba kuna kufa na siku moja nitakufa, wala hilo haliwezi likanikatisha tama ya kutokufanya kazi. Changamoto hizo Mhe. Spika, ndio zinatufanya sasa tuzidi kukaza buti katika hili. Wala wasifikirie kwamba maneno yatatushisha sisi. Sisi hatutishwi na maneno, nitafurahi sana kama wananchi wa Chakechake wataacha kunichagua kwa sababu ya kusimamia ukweli huu. Nitafurahi ikiwa chama changu kitashindwa kunipitisha kwa sababu ya kusimamia ukweli huu.

Lakini nitafurahi iwapo Mhe. Spika, utaniondosha katika Kamati ya PAC kwa sababu ya kusimamia ukweli huu. Ukiniona kuwa nimeshakuwa kero Mhe. Spika, katika kamati hii naomba uchukuwe maamuzi yako mwenyewe.

Mwisho kabisa naomba Mhe. Spika, nimalizie kwa kukabidhi sasa ripoti yetu yenye mapendekezo 12 na mapendekezo ya ziada yaliyopendekezwa na Mjumbe Mhe. Hamza Hassan Juma mapendekezo mawili.

Naomba nikukabidhi sasa ripoti hiyo na niseme kwamba Mungu Ibariki Zanzibar, Mungu wabariki Wazanzibari. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Wajumbe wote wa Baraza waliohudhuria leo wameunga mkono hoja hii, nawashukuru sana. Kwa maana hiyo ripoti hiyo inapokelewa rasmi na Baraza hili na inakabidhishwa rasmi kwa serikali kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Tunakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kukamilisha kazi hiyo. *(Makofi)*

TAARIFA YA SERIKALI

Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi Iliyoundwa Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kupata fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuja kuwasilisha utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ilioundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa, mwenyekiti wa Kamati ile alikuwa Mhe.

Salmin Awadh Salmin, mwakilishi wa jimbo la Magomeni. Wajumbe wengine walikuwa ni Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Isamil Jussa Ladhu, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Abdalla Juma Abdalla. Makatibu walikuwa Ndugu Nassra Awadh Salmin na Ndugu Maryam Rashid.

Mhe. Spika, sisi kama Wizara kama tulivyosema wakati ilipowasilishwa au alipofanya majumuisho Mwenyekiti kwamba tunaishukuru sana Kamati na Wajumbe wote wa Baraza kwa mapendekezo yale au kwa mchangiaji na wale waliotueleza na kututaka au kutushauri kwa kweli lazima nikiri Mhe. Spika, ripoti imetusaidia sana katika kutuonesha njia na namna ambavyo tunapaswa kuwajibika hasa katika masuala ya kijamii.

Mhe. Spika, mapendekezo ya Kamati Teule kwa ujumla yalikuwa kumi na tatu ingawa ripoti yenyewe ilikuwa na kurasa 64 mbali na viambatanisho. Kwa jumla niseme Mhe. Spika, kwamba ile *theme* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sisi Baraza la Manispaa tunaikubali kwamba lazima tubadilike katika utendaji wetu, naomba kusisitiza kwamba lazima tubakilike katika utendaji wetu. Kwa hivyo mapungufu kamati waliyoyaona mengi yao tumekiri yapo na tumetoa hii kama *road map* ya utekelezaji wake na Baraza la Manispaa si-*exception,* kwa hivyo *theme* ya tubadilike. Kwa hivyo mtizamo wetu Mhe. Spika, ni kurekebisha utendaji wetu katika Baraza hasa katika uongozi na kuwa na mtizamo wa kuwa na maamuzi ya pamoja, hili suala lazima nikiri hapo nyuma halikuwepo, lazima tufanye kazi kwa pamoja na hasa baada ya maamuzi kupitishwa basi tufuate taratibu na sheria za nchi.

Sasa kwa ruhusa yako baada ya utangulizi huo, naomba Mhe. Spika, nipitie pendekezo moja baada ya jengine, na kwanza nioneshe kwenye bango kitita hilo pendekezo lililotolewa, ushauri, hatua zilizopangwa kutekelezwa, utekelezaji halisi na maelezo kama yapo.

Mhe. Spika, pendekezo la kwanza lilikuwa juu ya Mkurugenzi wa Manispaa na wale walioshiriki kwa namna moja au nyengine kutofuata sheria na kanuni mbali mbali kuchukuliwa hatua za kisheria. Mhe. Spika, katika hatua zilizopangwa kutekelezwa kuliwasilisha suala hilo kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi ya Ukurugenzi. Najua ile ni nafasi ya uteuzi wa Rais kwa hivyo lazima ipitie kule.

Utekelezaji, Mhe.Spika, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ameshaondolewa katika nyadhifa hiyo kwa barua yenye kumbukumbu namba hiyo ya tarehe 22/10/2012 na ile yenye kumbukumbu Afisi ya Rais Tawala za Mikoa hiyo ya tarehe 30/12/2012.

Aidha nafasi nyengine nzito ambayo tumeona ina umuhimu sana katika utendaji wa Baraza ni Mhasibu katika Baraza la Manispaa; ambaye kwa kweli tumeona kwa fani yake ana fani nyengine kwa hivyo na yeye tumemfanyia uhamisho kwa barua hiyo iliyotajwa ya tarehe 14 Januari. Mhe. Spika, masuala haya yamepelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa uchunguzi zaidi na kutoa mapendekezo ya hatua za kisheria za kuchukuliwa. Kuna walioingia makosani na wengine hawamo makosani. Sasa tuseme sisi Wizara tuna *mandate* hiyo au tuna uwezo huo wa kumshtaki mtu hatuna. Kwa hivyo tumetaka ushauri wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wamepewa *copy* hii wakaipitia halafu watushauri kisheria hatua za kuchukuliwa kwa wale wote waliotajwa na mapungufu ya kisheria.

Mhe. Spika, hatua nyengine iliyopangwa kutekelezwa ni kupitia majukumu ya kiutendaji kwa wale wote waliotajwa na kuyafanyia kazi na kuchambua makosa yaliyojitokeza dhidi yao. Utekelezaji halisi majukumu yanaendelea kupitiwa sambamba na aina ya makosa kwa hatua za kisheria na kinidhamu kuchukuliwa. Kwa maelezo zaidi kazi hii inahitaji umakini katika kutekeleza, kwani inahitaji uchambuzi na ukusanyaji mzuri wa vielelezo, hivyo kazi inaendelea na tayari ofisi imeshaomba ushauri wa kisheria kutoka Tume ya Utumishi Serikalini na Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Aidha, *scheme of service* ya Baraza inatengenezwa upya kama ilivyo agizo hilo kwa taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pendekezo au ushauri wa pili tuliopewa ni kwamba wateja wa Baraza la Manispaa waliodhulumiwa haki zao warejeshewe wenyewe kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha. Hatua zilizopangwa kutekelezwa kwamba kufanya uhakiki wa zoezi hili yaani kufaya zoezi la uhakiki kuwatambua wale wote waliodhulumiwa ingawa orodha ya watu imeshatajwa. Lazima na sisi tupitie upande wetu twende nao tupitie mikataba, tuangalie vizuri kwa hivyo hiyo ndio imepangwa kutekelezwa. Utekelezaji halisi Mhe. Spika, zoezi la kuwatambua na kuhakiki limeshaanza na utekelezaji unaendelea.

Agizo la tatu Mhe. Spika, ni kwamba Baraza la Manispaa iyatengeneze masoko yake kwa kulinda dhana ya soko na sio kujenga maduka ya kudumu ambayo yataiondosha dhana hiyo. Hatua iliyopangwa kutekelezwa ni kuwasilisha pendekezo hili Baraza la Manispaa. Hatua ya kuwasilisha pendekezo hilo imefanyika, kwa barua hiyo na hatua za awali ni kupitia upya *management* ya masoko yetu yote kwa lengo la kupata viongozi wapya wenye taaluma na uzoefu wenye ushindani wa soko.

Vile vile Baraza la Manispaa kwa kuitikia pendekezo la kamati la kuwaajiri wataalamu katika safu ya uongozi mzima wa manispaa umeshatangaza nafasi tisa za kitaalamu katika kiwango cha shahada au diploma ya juu. Nafasi zilizotangazwa ni kama ifuatavyo:

Kwanza wanasheria nafasi mbili, Mhandisi wa Majengo nafasi moja, Mhandisi wa Mazingira nafasi moja, *Town planner* nafasi moja, Uchumi nafasi moja, *Information Technology* nafasi mbili, *Health Environment Officer* nafasi mbili, Afisa wa Mipango nafasi moja, Fundi Mkuu Magari nafasi moja.

Mhe. Spika, hili naomba kusisitiza kwamba Kamati ilitushauri sana kwamba kwa kweli Baraza la Manispaa halina wataalamu ingawa mambo yanakwenda lakini yanaweza kwenda vizuri zaidi tukipata wataalamu katika fani mbali mbali. Kwa hivyo tumelichukua agizo hilo na tumezitangaza nafasi hizi Mhe. Spika, tumezitangaza rasmi…

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza tunaishukuru sana serikali kwa kutuletea jawabu zinazoonesha utekelezaji wake. Lakini Mhe. Spika, nilikuwa naomba Mhe. Waziri kuna *document* alikuwa anaisoma sasa hivi sisi huku hatuna. Sasa ilikuwa vizuri twende sambamba na ile anayosoma yeye na yale yaliyokuwemo humu. Hii *document* hizo nafasi zilizotangazwa

humu katika kabrasha tulizopewa sisi hazimo. Sasa ilikuwa vizuri ule mtiririko wa maelezo yake uende sambamba na huu tuliokuwa nao sisi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, hizo nafasi ni kweli lakini kwenye *presentation* mimi nina *text* yangu sio kama *speech* niisome yote aa, mimi nina *text* yangu na hiyo niliyokupeni ni *guide line* ya utekelezaji na haitofautiani sana labda hizo nafasi ndio hazimo umo. Sasa hii nimeifanyia *editing, cut and paste* Mheshimiwa nilete kitu kidogo ambacho hakifahamiki? Lakini kwa kweli kilichomo humo ndio ninachokisoma labda hii nyongeza hizo nafasi tu ambayo niliona haja nizitafute na nikazipata ndio maana ninazisoma hasa, sasa baadae Mhe. Spika, nitatoa *photocopy* kila mmoja aipate, lakini kwa kweli Mhe. Spika, ninayosoma kimsingi ndio hiyo hiyo nimeifanyia *editing t*u. Hii nitaitoa *photocopy.*

Mhe. Spika: Nafikiri tuendelee hiyo *photocopy* itoe ili Waheshimiwa Wajumbe wapate.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, pendekezo jengine ni pendekezo la nne Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa atekeleze majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi. Vile vile ashirikishe wakuu wa Idara zake kwa yale mambo yanayowahusu. Hili Mhe. Spika, ndio vile nilivyosema suala zima ni maamuzi na uongozi wa pamoja, kitu hiki kidogo hapo nyuma hakikuwepo katika Baraza la Manispaa. Sasa tumejirekebisha sasa kuna maamuzi ya pamoja na vikao vya pamoja na kuheshimu maamuzi na maelekezo yanayoamuliwa kwa pamoja.
Kwa hivyo hatua zilizopangwa kutekelezwa Kaimu Mkurugenzi kukaa na watendaji wenzake wa Baraza ili kuliwasilisha pendekezo hilo kwa mipango ya utekelezaji wake kwa kina. Tayari vikao viwili vya kutoa elimu vimefanyika kwa uongozi uliopo na Waziri katika kuhakikisha Waziri mwenyewe amejiwekea utaratibu wa kukutana na uongozi wa Manispaa kila mwezi angalau mara moja. Pia Waziri ameshakaa na waheshimiwa madiwani katika kikao chake cha mwanzo baada ya ripoti hii kupokelewa tarehe 4 Disemba, 2012. Na vikao hivi vitakuwa vikiendelea kila mwezi na kila itapohitajika.

Mhe. Spika, ushauri wa tano ni kwamba serikali ijenge soko kubwa ambalo litakidhi haja kwa wafanyabiashara wetu. Hatua zilizopangwa kutekelezwa kwamba kwa sasa serikali haijapanga kujenga soko kubwa la kisasa. Hata hivyo milango iko wazi kwa wawekezaji binafsi kuleta maombi yao serikalini, ila serikali kwa sasa imelenga kuyafanyia ukarabati masoko yaliyoko ya Mwanakwerekwe, Mombasa, Mikunguni, Saateni na soko la Darajani.

Mhe. Spika, utekelezaji tayari soko la Mombasa limesharejeshewa huduma za maji, umeme na kuimarishwa kwa usafi na kuvifanyia ukarabati vyoo kwa ajili ya kuwahudumia wafanyabiasha watakaopokelewa. Mhe. Spika, serikali imekusudia kuyaimarisha masoko yake na kuhakikisha kwamba yanatumika vizuri kwa wafanyabiashara kuhamia katika masoko hayo. Vile vile Mhe. Spika, mpango kazi umeshaandaliwa wa kulifanyia kazi pendekezo la kuendeleza soko la Saateni na suala zima la kuwapeleka wafanyabiashara wadogo wadogo wasio na milango katika eneo la Darajani.

Mhe. Spika, pendekezo la Sita ni vyema likaandaa mikataba yenye hadhi ya kisheria, Baraza kuheshimu mikataba inayofunga ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Tumepanga kuipitia mikataba yote na kuiweka kisheria zaidi. Kwa sababu tuligundua pale nyuma ilikuwa inamalizwa pale pale Baraza la Manispaa na kulikuwa na mapungufu kadhaa kama Kamati ilivyoyaona, kwa hivyo tumepanga kuipitia mikataba yote na kuiweka kisheria zaidi kwa kushirikiana na wahusika wote. Tayari mikataba ya Baraza imeorodheshwa na mapitio ya mikataba imeanza kuchukuliwa hatua. Kwa maelezo zaidi Mhe. Spika, wale wote waliofunga mikataba wataarifiwa mabadiliko yaliyopo kwa nia ya kuiweka kisheria zaidi.

Pendekezo la Saba Mhe. Spika, ni kwamba Baraza kuwatafutia eneo mbadala wafanyabiashara wote wanaouza biashara zao pembeni mwa barabara katika soko la Mwanakwerekwe kwa lengo la kulinda hadhi ya mji sambamba na kuepusha ajali zisizokuwa za lazima. Mhe. Spika, tumepanga kulifanyia ukarabati soko la Mombasa kwa nini? Lengo letu kwamba wale wafanyabiashara ambao wanapanga biashara barabarani na bila ya utaratibu basi wote waelekee katika soko hilo la Mombasa ili waendelee kupata rizki zao. Mhe. Spika, kama nilivyosema ukarabati wa soko la Mombasa umeanza kwa kurejesha huduma za maji na umeme katika soko hilo, shughuli za usafi zimeimarishwa ndani ya soko na ukarabati wa vyoo umefanyika pamoja na miundombinu mengine.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi zote hizo lakini tumegundua kuna tatizo kubwa sana ambalo Waheshimiwa Wawakilishi nakuombeni sana mtusaidie, tatizo lenyewe ni kwamba kumejitokeza ugumu wa kutofuata sheria kwa baadhi ya wananchi wetu. Wale walinzi wetu wa Manispaa au watu wa soko wanatishwa, wanapigwa kwa mapanga, matufali, kwa kumuelekeza mtu fuata taratibu usifanye biashara hapa fanya hivi, kwa hivyo kwa kweli lile suala zima la kufuata utaratibu unakuwa kama adui wewe, kwa nini unaelekeza tufuate taratibu. Sasa hili ningekuombeni sana Waheshimiwa tusaidiane, sisi ndio tunaotunga sheria na sisi ndio wenye nchi tusaidiane kuelimisha. Baraza la Manispaa linafanya, serikali inafanya, lakini na sisi kwenye majimbo yetu tuwasaidie sana kuwafahamisha watu, nchi yoyote inaendeshwa kwa sheria, nchi yoyote inaendeshwa kwa taratibu, kwa kweli haipendezi kuona watu wanapanga vitu barabarani. Lakini kweli tukachukue burdoza pale au Katapila tusage vitu pale au kila siku tuwapeleke FFU hatupendi tufike huko. Sasa tujitahidi ninakuombeni sana Waheshimiwa tusaidiane kuelimisha watu wetu kwa kweli wafahamu taratibu, serikali inawatakia mema watu wake na inawapendelea wapate rizki lakini kwa mahala mlimokusudia sio popote tu.

Mhe. Spika, nimezungumza hilo kwamba tumepanga kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara sehemu isiyoruhusiwa. Kazi ya utoaji wa elimu na uorodheshaji wa wafanyabiashara waliopo nje ya soko imeanza kwa lengo la kuwafahamisha madhara ya kufanya biashara mwahala msimofaa na kuwatambua ili kuweza kuwapanga vizuri katika soko la Mombasa.

Hatua nyengine Mhe. Spika, ambayo tumepanga kutekeleza ni kuzipitia kanuni za Baraza la Mji na Halmashauri ili kukabiliana na wafanyabiashara wasiokubali kutii sheria. Tayari Mhe. Spika, Baraza limeanza hatua za kurekebisha kanuni na tayari baadhi ya mapendekezo ya mabadiliko hayo yameshajadiliwa katika kamati husika, na semina imeandaliwa ya watendaji na waheshimiwa madiwani kupitia baadhi ya kanuni, na hatua ya kujadiliwa na Baraza kuu kabla ya

kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa kupata ushauri zaidi. Kwa upande wa Halmashauri ya Magharibi tayari kanuni zimefikishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, pendekezo la Nane lilikuwa Baraza la Manispaa liachane na tabia ya kuwatumia watendaji wake kwa zile kazi zinazotolewa kwa mtu binafsi, tumepanga kuwasilisha pendekezo hilo Baraza la Manispaa kulifanyia kazi. Tunashukuru tayari hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuisimamisha kazi Kampuni iliyokuwa ikitengeneza maeneo ya Michenzani katika kazi za bustani na kuweka vigae. Kazi hiyo sasa inaendelezwa na Baraza la Manispaa wenyewe.

Mhe. Spika, ushauri wa Tisa, ilikuwa kwamba Mkurugenzi wa Baraza na watendaji wazijue kwa kina sheria za nchi hususan zile wanazofanyia kazi. Tumepanga kutoa maelekezo kwa uongozi wa Manispaa juu ya azma hiyo, tunashukuru maelekezo yamewasilishwa kwa uongozi kwa barua iliyotajwa hapo juu ya tarehe 9 Januari 2013. Vile vile Mhe. Spika, Afisi inafuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wa suala hili pamoja na kupendekeza watendaji kupatiwa semina juu ya sheria za nchi na uwajibikaji wake.

Mhe. Spika, pendekezo la Kumi lilizungumzia kwamba ripoti hii ibakie katika maktaba ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi ili iwe rahisi kwa kila mtumiaji wa maktaba hiyo kuipata kwa wepesi. Tumepanga katika kutekeleza kwamba suala hili kuwasilisha pendekezo husika kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi. Pendekezo nimewasilisha kwa barua yenye kumbukumbu hiyo ya tarehe 9 Januari 2013 na tayari utekelezaji wake umekamilika.

Pendekezo la Kumi na Moja Mhe. Spika, ni kwamba watendaji wa Mamlaka ya Uhifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe wanapotoa barua ya taasisi yao waandike majina yao ili ajulikane nani aliyesaini barua ile ingawa wanafanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi. Hatua iliyopangwa kutekelezwa ni kuiandikia na kuliwasilisha pendekezo hili katika Mamlaka ya Uhifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe. Katika utekelezaji Mhe. Spika, pendekezo limeshawasilishwa katika Mamlaka kwa barua namba hiyo iliyotajwa ya tarehe 9/01/2013 na tayari maelekezo yamepokelewa na kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, pendekezo la Kumi na Mbili lilizungumzia sheria ya Baraza la Manispaa na Kanuni za Kudumu za Baraza, zifanyiwe mapitio na ziendane na mazingira halisi. Azma yetu ni kukamilisha maandalizi ya utaratibu wa utekelezaji wa sera ya serikali za mitaa. Kwa utekelezaji sera ya serikali za mitaa imeshatayarishwa na imesharidhiwa na serikali, na rasimu ya mpango wa utekelezaji yaani *strategic plan* umeshaandaliwa na uko tayari na hii itatusaidia sana katika kuandaa hizo sheria mpya baada ya sera. Mhe. Spika, hatua nyengine iliyopangwa kutekelezwa ni kuipitia sheria ya Baraza la Manispaa na Halmashauri pamoja na Tawala za Mikoa na sheria za serikali za mitaa, ambayo yatajumuisha mapitio ya sheria nambari 3 na nambari 4 za mwaka 1995 pamoja na Baraza la Manispaa.
Vile vile kuzipitia kanuni za kudumu za Baraza. Mhe. Spika, kwa utekelezaji Baraza limeanza hatu za kurekebisha kanuni za kudumu na nyenginezo na tayari mapendekezo ya mabadiliko hayo yameshajadiliwa katika kamati husika na yamo katika hatua ya kujadiliwa na Baraza Kuu kabla ya kuwasilishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ushauri zaidi na hatimaye kuridhiwa na Waziri na kuanza utekelezaji wake. Labda mtu au Mheshimiwa atauliza hizo kanuni tunazozizungumzia ni zipi? Hii naomba radhi imenipitikia baadae nikatayarisha karatasi

ya pembeni ninayo hii nitaitoa *photocopy*. Kanuni zenyewe na hizi hasa kwa kweli zitatusaidia sana katika kuondoa migongano kati ya waheshimiwa madiwani na watendaji. Kanuni zenyewe kwanza ni kanuni ya *street traders and hawkers* ya mwaka 1963, kanuni nyengine ni kanuni ya uanzishaji wa masoko ya mwaka 1963, kanuni nyengine ni kanuni ya masoko madogo madogo na faini ya papo kwa papo ya mwaka 2013. Na kanuni nyengine ni kanuni ya matangazo ya biashara yaani *advertisement* na kanuni nyengine ni kanuni ya udhibiti wa maeneo ya wazi ya mwaka 2004, na mwisho ni kanuni ya udhibiti wa uzururaji wa wanyama ovyo.

Mhe. Spika, pendekezo la 13 ni kwamba serikali iyatekeleze mapendekezo ya ripoti kwa vitendo ndani ya miezi 3 kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti na hatimae serikali iwasilishe utekelezaji wake mbele ya Baraza hili tukufu. Hatua iliyopangwa ni kwamba ni kutekeleza mapendekezo yote kama yalivyoelekezwa. Utekelezaji halisi, utekelezaji umeanza kwa awamu kwa mapendekezo yote kama yalivyowasilishwa. Kwa maelezo zaidi Mhe. Spika, katika utekelezaji kuna mapendekezo ambayo yalihitaji muda mfupi, maamuzi ya haraka yaani *short term* hayo hatukuchelewa tumeyachukulia hatua kama tulivyoyaripoti. Lakini kuna mengine Mhe. Spika, yatahitaji muda mrefu yaani *long term* kuyakamilisha na hiyo inatokana na kufuata utaratibu yaani mfano kurekebisha sheria na mipaka ya maeneo. Hayo kwa kweli itabidi yasubiri kwa sababu haya hayako moja kwa moja ndani ya mikono yetu, yapo ndani ya utendaji lakini wizara au sekta zinazohusika kama ardhi au upande wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo haya kwa kushirikiana na wenzetu tutakwenda nayo ili tuone nayo tunaharakisha ili na sisi tupate utendaji mzuri.

Sasa Mhe. Spika, kama nilivyosema mapendekezo ya jumla yalikuwa 13 na haya kwa kweli nikiyapitia kwa *summary* aliyoifanya Mwenyekiti na Kamati ni nzuri sana kwa sababu haya yamegusa zile *chapter* tano zote au yale mapendekezo makubwa waliyoyatoa katika kitabu kile. Kwa ujumla ilikuwa kule kulikuwa na *chapter* nane na hasa kwa kweli hasa agenda zilizoguswa ni tano hasa. Sasa ukitizama mapendekezo haya kwa ujumla yameyagusa yale yote kwa ndani, kwa hivyo mimi ninawashukuru sana Kamati kwa *summary* ile hasa Mwenyekiti kwa *summary* ile ya mapendekezo na kama nilivyosema si rahisi mimi kuichambua moja moja moja. Lakini kwa ujumla kama walivyotuelekeza na sisi tutakuwa dira sasa wa kutekeleza haya ambayo tumeshauriwa. Kwa hivyo kimsingi Mhe. Spika, sisi haya tuliyoshauriwa, tuliyoelekezwa pamoja na kitabu hiki tunakichukua kwa kushirikiana na wenzetu hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuona kwamba tunayatekeleza na kupata ufanisi.

Lakini kubwa nimalizie Mhe. Spika, ni suala la kuendesha Baraza kitaalamu, kama Kamati walivyoona kuna mapungufu ya watendaji kitaalamu, sasa hilo tunalivalia njuga tuone tunalifanikisha mapema iwezekanavyo kwa kushirikiana na wizara inayoshughulika na masuala ya ajira ili tuweze kupata watendaji ambao tunahisi watatoa sura mpya ya mabadiliko katika utendaji wa Baraza zima.

Mhe. Spika, naomba nimalizie na niseme naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe taarifa imewasilishwa nadhani maneno kidogo yako kwa sababu nimepata ombi la Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye anataka kuchangia na baadae Mhe. Hamza Hassan Juma. Karibu Mheshimiwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mola wetu Mtukufu kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima wa afya na leo hii kupata fursa ya kuendelea na shughuli zetu katika Baraza hili, wakati huu tukiwa tunajadili Taarifa ya Serikali juu ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa kuwa mtu wa kwanza kuchangia. Nashukuru pia kupata nafasi hii kwa sababu mimi nilikuwa ni mmoja kati ya Wajumbe watano uliowateuwa kuunda Kamati Teule iliyofanya kazi hii kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa. Mwenyekiti wetu amepata safari lakini wajumbe wengine tupo.

Mhe. Spika, katika ripoti yetu ambayo imewasilishwa katika kikao kilichopita ukurasa wa 64 katika yale mapendekezo ya jumla pendekezo la 13 lilikuwa linasema, Kamati inaliomba Baraza hili tukufu liitake serikali iyatekeleze mapendekezo ya ripoti hii kwa vitendo ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hii na hatimaye serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wake mbele ya Baraza hili tukufu. Lengo ni kuijenga nchi yetu na kuifanya izidi kuwa ni sehemu ya furaha kwa kila mtu anayeishi katika nchi hii.
Mhe. Spika, niseme nimesikitishwa sana sana na serikali kuendelea kuonesha kutokuwa makini katika kujibu hoja zilizoibuliwa ndani ya Baraza hili. Najiuliza hivi ripoti hii yenye kurasa jumla yake 65 na vielelezo vyote hivi leo maelezo ya utekelezaji wake ndio haya Mhe. Spika! *Are we serious*? Wakati Mhe. Waziri anasoma ripoti hii tayari Mhe. Hamza Hassan Juma alinyanyuka kuonesha moja ya kutokuweko *seriousness*, kutoonesha umakini kwamba anachotusomea ambapo sisi ndio tunaotaka tupokee ripoti ya utekelezaji kuna baadhi ya maelezo hayamo, lakini kama alivyosema mwenyewe ni maeneo machache hata haya Mhe. Spika, kwa jumla yake nimesikitika na katika haya kwa niaba ya kamati naomba mimi mmoja niweke wazi kabisa.

Mhe. Spika, umakini unaanza kukosekana katika hata kuorodhesha yale mapendekezo. Mapendekezo aliyokuja kutolea taarifa Mhe. Waziri ni mapendekezo 13 ambhayo sasa ni maazimio ya Baraza kwa sababu yaliletwa na kamati yakaidhinishwa na Baraza. Haya hata katika ripoti yetu tumeyaita ni mapendekezo ya Kamati Teule kwa ujumla yako katika ukurasa wa 63 hadi 64. Lakini Mhe. Waziri mwenyewe kakiri katika kumalizia maelezo yake, kwamba ripoti hii iligawika katika sehemu kadhaa kulingana na hadidu rejea ambazo Mhe. Spika, ulitupa na katika kila hadidurejea kulikuwa kuna mapendekezo makhsusi ya hadidu ile. Sasa mimi nilitegemea ni kweli *summary* ni *summary* yoyote, lakini unapokuwa na mapendekezo au maazimio makhsusi basi ni lazima na ripoti ya utekelezaji katika chombo kikubwa cha wananchi kama hiki nayo yawe mahsusi hayawezi kuwa kijumla jumla kama haya Mhe. Spika. Kwa sababu lengo la kuleta utekelezaji hapa ni kupima ufanisi wa chombo hiki katika kusimamia serikali.

Mhe. Spika, Ibara ya 5(a) ya katiba yetu imeweka wazi kwamba majukumu ya chombo hiki ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Katika kikao hiki nilitahadharisha, kwamba mara nyengine kukosekana kwa umakini kunaweza kupoteza hata ile imani ya wananchi ambayo ilikuwa imejenga katika chombo hiki. Nashukuru kwamba katika siku za mwisho hizi wananchi

mitaani huko tunaanza kuona wanarejesha imani wanafuatilia mijadala hii, lakini mambo kama haya yanawavunja moyo wananchi na hata sisi wawakilishi wa wananchi tunaofanya kazi hii.

Mhe. Spika, kufanya kazi za Kamati Teule sote tunajua si kazi nyepesi hata kidogo unaacha yako inabidi waingie wafanyakazi kwa muda wa ziada kukusanya ushahidi na vielelezo, lakini halafu unapoleta hapa serikali ikajibu kwa jumla jumla kama hivi Mhe. Spika, imenisikitisha.

Naomba nitoe mifano tu, kwa sababu sitaki kuchukua muda mrefu. Mhe. Spika, ukiangalia katika hadidurejea ya mwanzo kwa mfano, ukurasa wa 15 wa ripoti palikuwa na hatua za kuchukuliwa kutokana na matokeo ya uchunguzi huo. Nilisema la kwanza, kutokana na vitendo mbali mbali vya ukiukaji wa sheria na kanuni za Baraza zilivyobainika dhidi ya Baraza la Manispaa Kamati hii inaishauri serikali kumchukulia hatua za kinidhamu na kisheria Mkurugenzi huyo, hili limejitokeza katika yale ya jumla. Lakini halafu kuna suala zima kwa mfano la kipengele cha 4. Serikali ichukue hatua za makusudi kuona kwamba pande mbili za Baraza madiwani na watendaji zinashirikiana ili kuleta tija iliyokusudiwa, ukisoma hilo katika ya jumla hulipati utekelezaji wake. Niondoke hapo Mhe. Spika.

Ukija katika eneo jengine ambalo lilikuwa katika kuna kipengele kimoja hapa ametajwa mtendaji wa Baraza la Manispaa liko katika ukurasa wa 38 wa ripoti. Hii inahusu uchunguzi katika hadidurejea ile inayohusu matumizi na utoaji wa *tender* katika shughuli mbali mbali. Ukurasa wa 38 wa ripoti unasema nambari moja, "kwa kuwa Ndugu Vuai alitoa maelezo yanayotofautiana mbele ya kamati kwa lengo la kuipotosha kamati hiyo na kuficha ukweli juu ya utendaji wa Baraza la Manispaa tunapendekeza achukuliwe hatua za kisheria chini ya kifungu cha 22 cha sheria Nam. 4". Sasa humu huyaoni hayo Mhe. Spika, haya ni mapendekezo makhsusi sio yale ya jumla ambayo yamewekwa kule mwisho, lakini na hayo Mhe. Spika unayapa kila pahala.

Sasa ukisoma nilitegemea mimi ripoti ya serikali kwanza ingekuja kwa ile moja moja ya kila hadidurejea kwa sababu ndio iliyotupa muongozo wako kwenda kufanya kazi ile halafu ndio yaje haya ya jumla, hayaonekani. Hilo moja Mhe. Spika, limekosa umakini.

Lakini la pili hata hayo serikali waliyoamua kuyatolea taarifa mimi nilikuwa najiuliza wakati Mhe. Waziri anasoma hapa tuchukue mfano hili la mwanzo kabisa. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine kutokufuata sheria na kanuni mbali mbali kuchukuliwa hatua. Sasa serikali inajibu hapa, hatua zilizopangwa kutekelezwa, la mwanzo imesema kuliwasilisha suala hili kwa Katibu Kiongozi kwa ngazi ya Mkurugenzi halafu tumeelezwa barua zilizofuata za kumuondosha katika wadhifa huo kama ilivyoelezwa hapa.

Lakini ya pili katika hatua imesema, kupitia majukumu ya kiutendaji wale wote waliotajwa na kuyafanyia kazi na kuchambua makosa yaliyojitokeza dhidi yao. Sasa Mhe. Spika, pendelezo linasema, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine kutokufuata sheria na kanuni mbali mbali kuchukuliwa hatua, ukisoma humo ndani ukienda kule kwenye *specific* kuna hatua za kinidhamu na hatua za kisheria, wako Mhe. Spika, ambao tuliwaonesha wamekiuka hata sheria ya hifadhi na kinga ya Baraza hili kwa kutoa taarifa za uongo mbele ya kamati hilo ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria ile.

Sasa mimi nilitegemea sio aje atwambie kwamba anapitia majukumu ya kiutendaji na wale wote waliotajwa na kuyafanyia kazi na kuchambua makosa yaliyojitokeza dhidi yao. Makosa yameshabainishwa humu na kuna vielelezo, mimi nilichotegemea ni kile ambacho nilikisema tulipokuwa tukipitia ripoti iliyopita na nilikipendekeza kwa wenzangu hapa, kwamba najua sisi hatuna mamlaka ya kusema kwamba baada hii tupeleke Mahkamani kuna utaratibu wa kupita kwa mfano kwenye vyombo vinavyohusika kama ni polisi au DPP. Sasa nilitegemea katika hili kama serikali ilikuwa inafanya kazi ingetwambia kwamba jalada hili na vielelezo vyake viko kwa DPP na vinafanyiwa kazi kwa uchunguzi hilo hulioni katika maelezo ya serikali Mhe. Spika.

Mhe. Spika, sitaki kwenda moja moja kwa sababu najua nitachukua muda nataka kutoa mfano tu kuonesha kwamba hii ripoti haina maana yoyote katika Baraza hili. Chukulia hili pendekezo la pili, wateja wa Baraza la Manispaa waliodhulumiwa haki zao warejeshewe wenyewe kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha, iko ukurasa wa pili. Hatua zilizopangwa kutekelezwa, kufanya zoezi la uhakiki la kuwatambua wale wote waliodhulumiwa. Halafu utekelezaji halisi unasema shughuli hii haijafanyika. Maelezo, utekelezaji unasubiri safu mpya ya uongozi wa kiutendaji wa Baraza.

Mhe. Spika, kwanza taasisi ipo aliyeondoka ni mtu na hivi sasa kuna kaimu naye aliyekuwepo tunaambiwa alikuwa *secured* kutoka katika Bodi ya Mapato, sasa hivi yuko mtu. Lakini najiuliza unaposema unafanya zoezi la uhakiki kuwatambuwa waliodhulumiwa na waliodhulumiwa wametajwa humu kuisaidia serikali mpaka mikataba yao ilivyokuwa na maelezo yake yameorodheshwa humu. Sasa ndio pale wanapopiga kelele wajumbe wako kwamba tunapoteza fedha za walipa kodi kwenda kufanya uchunguzi tunaleta hapa yanaridhiwa na Baraza halafu serikali inakwenda kufanya uchunguzi wake mpya. Yako maeneo nakubali kama alivyosema kuwa kuna maeneo ya hatua zai kisheria huwezi tu ukatoka Barazani ukasema unakwenda kushtaki Mahkamani lazima taratibu zake zifuatwe.

Lakini mambo ambayo tayari yameorodheshwa na vielelezo vyake vimo na vimeambatanishwa halafu bado serikali itwambie inafanya uhakiki wa waliodhulumiwa Mhe. Spika, tunajiuliza faida ya kazi hii ni nini? Mhe. Spika, hayo yako katika kila pendekezo ambalo lilitolewa na maelezo ya serikali ambayo imeyajibu hapa, ukitoa lile la ujenzi wa soko hivyo hivyo.

Pendekezo linasema ujenzi wa soko jipya serikali inaripoti matengenezo ya masoko yaliyokuwepo, ingeweza kutwambia kwamba sasa hivi inatengeneza au ingeatwambia kwamba sasa hivi serikali haina uwezo. Lakini haiwezekani pendekezo linasema ujenzi wa soko jipa serikali inajibu kwamba tunatengeneza yaliyokuwepo. Mhe. Spika, haioneshi kabisa *seriousness* ya suala hilo.

Vile vile Mhe. Spika, ukitizama hili pendekezo linalohusu kuwatafutia eneo mbadala wafanyabiashara ambao wametajwa kuwa wamejaa kwa mfano Mwanakwerekwe kule, walioko Darajani. Serikali imetwambia kwamba inafanya utaratibu wa kutengeneza soko la Mombasa. Moja kati ya mambo ambayo tumebainisha katika ripoti zetu ni kwamba ushirikiano ulikuwa unakosekana wa hawa ambao walitakiwa kuhama kutoka eneo moja kwenda katika maeneo mengine. Kwa sababu wanakopelekwa hakuna huduma na si huduma tu kwa maana ya huduma

zao lakini hata kuwafanya wateja kuweza kupita katika maeneo yao kufanya biashara na ndio maana wanashindwa kutekeleza matakwa ya serikali kwa sababu yule ni binadamu anatafuta riziki yake.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, sitokaa humu ndani tukalipwa posho wengine hawana posho hii inabidi akae juani kuanzia asubuhi mpaka usiku, unamkuta pale usiku anakaa anatafuta riziki yake. Sasa lazima tuwe na utaratibu wa kuwawekea mazingira kwamba atawapata wateja na mapendekezo ya serikali yamejibu kama vile basi inaondosha ondosha njiani tu.

Mhe. Spika, sitaki kuyasema moja moja kama nilivyosema lakini kwa jumla mimi kabisa sijaridhika na ripoti hii ya serikali waliyoileta hapa ya utekelezaji. Na nasema nikiwa Mjumbe wa Kamati kwamba kwa namna hii Mhe. Spika, Wajumbe wako tutavunjika moyo sana, kwamba serikali hii kweli ina nia ya kutekeleza kazi ya kuwatumikia wananchi kupitia chombo chao hiki.

Juzi nilisema Mhe. Spika, kwamba katiba yetu inasema serikali kwa maana ya mawaziri chini ya Makamu wa Pili wa Rais wanawajibika kwa pamoja katika Baraza hili, ibara ya 43(5). Na nikasema kwamba ikiwa kila siku tutaunda kamati ikiwa serikali haioneshi umakini tutafika pahala tutakuwa hatuna chaguo jengine Mhe. Spika. Kwa sababu kama Wawakilishi hatuna mamlaka ya kumuondoa waziri sisi aliyekuwa hawajibiki moja kwa moja, lakini katiba imetupa *power* ya kumpigia kura ya kutokuwa na imani Makamu wa Pili wa Rais maana yake serikali nzima iondoke na wenzetu Bungeni wametumia mamlaka hayo Mhe. Spika, hawakupiga kura ya kutokuwa na imani, lakini utekelezaji wa ripoti yao umepelekea kuondoka Waziri Mkuu na ikabidi serikali iunde upya Baraza la Mawaziri kupitia kwa Rais.

Hata karibuni kabisa katika Bunge hili linaloendelea Rais alilazimika alipoona Wabunge wamechachamaa kulivunja Baraza la Mawaziri akaliunda upya. Mhe. Spika, inaonekana sisi humu ndani kidogo ile heshima kwa Wajumbe inapungua kwa sababu labda Wajumbe hawajaamua kufanya kazi yao hasa na kutekeleza majukumu yao na nguvu zetu ambazo tumepewa kikatiba.

Sasa Mhe. Spika, kasema Mhe. Mwenyekiti alipokuwa akifanya *winding* ya ripoti yake na mimi naomba nimalizie hilo nikae kitako. Kwamba hiyo tunayomaliza kuipitisha asubuhi leo kuipokea ripoti ni ya tatu, kuna kamati Mhe. Spika, umeunda ya kuchunguza masuala ya ardhi, zinaendelea kudundulizika lakini ripoti za utekelezaji wa serikali ndio kama hizi tunazoletewa hapa. Kikao kilichopita ilikataliwa Ripoti ya Serikali ya Utekelezaji wa Kamati ya Kwanza kabisa na mimi nashawishika kuwaambia Wajumbe wenzangu na hii ya leo tuikatae ripoti hii mimi siwezi kuipitisha hata siku moja. Kwa sababu sioni umakini wake katika serikali. Sasa najiuliza na keshokutwa itapokuja ripoti ikaja katika mtindo huu huu tukija tukiikataa ya utekelezaji wa Ripoti ya PAC iliyochunguza ZECO mawaziri chini ya Makamu wa Pili wa Rais wana uhalali gani wa kuendelea kutumikia serikali hii Mhe. Spika.

Sasa mimi Mhe. Spika, naomba niseme tena kwa moyo safi kabisa nimuombe Mhe. Rais mimi nasema mawaziri chini ya Makamu wa Pili wa Rais wameshindwa kazi Mhe. Spika. Inaonekana hawana uwezo tena wala ubunifu wa kuweza kusimamia maamuzi ya Baraza hili na kuweza kuwapa matumaini mapya wananchi wa Zanzibar ambao walitarajia sana katika serikali hii ya

Awamu ya Saba. Sasa nimuombe sana Mhe. Rais kwamba ikiwa wanashindwa kuwajibika afike pahali achukue maamuzi alivunje Baraza la Mawaziri aunde Baraza jipya la mawaziri Mhe. Spika, lakini kwa majibu haya ya kuondoshwa ondoshwa njiani haturidhiki kabisa.

Mimi nadhani wakati umefika serikali izingatie hilo na kama Mhe. Rais atakuwa bado anawaonea huruma mawaziri wake basi wananchi watakujakuwa wanashindwa kumfahamu yeye mwenyewe, na tukija tukifika hapo Mhe. Spika, sisi Waheshimiwa wengi tutakuwa hatuna *choice* nyengine, isipokuwa sasa itabidi tuungane kufanya kazi ile aliyoisema Mzee Jumbe kwamba ni ngome ya wananchi tupige kura ya kutokuwa na imani kwa Makamu wa Pili wa Rais ili kuilazimisha serikali ifikirie upya juu ya utendaji wake wa kazi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema naikataa ripoti iliyoletwa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na naomba kuwashawishi Wajumbe wenzangu tuikatae ripoti hii na tuitake serikali iwe makini katika kutekeleza kazi zake. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru kunipa nafasi hii nataka nizungumze mambo machache sana. Mhe. Spika, katika maelezo au katika utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ambayo iliundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa ambapo kamati hiyo iliongozwa na Mhe. Salmin Awadh Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni. Katika maelezo ya Mhe. Waziri mimi nadhani kama itakuwa iko haja Mhe. Spika, ungelimruhusu tena Mhe. Waziri akakaa tena na ile kamati akajaribu tena kupitia yale mapendekezo.

Mimi nafikiri Mhe. Spika, umetumia busara sana kwa kujenga mashirikiano baina ya serikali na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na hasa pale ulipomruhusu Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye aliyekuja kuwasilisha maelezo ya serikali kuhusu Ripoti ya Kamati Teule iliyopita kwamba akae tena na ile kamati kujaribu kuangalia yale mambo ambayo hawakuridhika nayo.

Sasa mimi nadhani Mhe. Spika, ili kuondoa utata kwa sababu si vizuri kila siku kuzungumzwa kwamba ripoti zimekataliwa na Baraza kidogo haituletei picha nzuri. Mimi nadhani sisi katika ile kamati iliyopita tulikaa na Mhe. Waziri na kwa kiasi fulani mambo mengi yale ambayo Wajumbe hawakuridhika nayo sasa hivi nadhani tumekaa na Mhe. Waziri na yeye amekiri kwamba kweli kulikuwa na baadhi ya mapungufu na ameahidi kwamba serikali itaweza kuyafanyia kazi. Kwa sababu sisi haja yetu sio kuja kubishana sisi haja yetu kila palipokwenda upande basi tupanyooshe ili mambo yaende vizuri.

Mhe. Spika, kama tutafikia hatua hiyo basi ni vizuri ukamruhusu Mhe. Waziri akarudi tena na kamati yake na kwa bahati mbaya leo Mwenyekiti hayupo hapa basi ni vizuri sisi tuchangie kwa yale ambayo tunaona kuna mapungufu baadae Mhe. Waziri arudi kwenye kamati yake wakae wajaribu kukubaliana hili na lile mimi nafikiri tutakwenda vizuri, bado tuendelee na ile *spirit* yetu ya kujenga mashirikiano zaidi kuliko kuweza kukwazana sana. Sasa hilo lilikuwa ombi la mwanzo.

Mhe. Spika, katika haya maelezo aliyotoa Mhe. Waziri kama alivyosema sisi tulifikia yatakwenda kwa zile *issue* zenyewe mafungu kwa mafungu, lakini yeye moja kwa moja alikuja kijumla jumla. Hili suala la mwanzo kuhusu suala la Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa hatua zilizopangwa kutekelezwa, kuliwasilisha suala hilo kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa ngazi ya ukurugnezi. Kwa sababu kama tunavyojua kuna hatua mbali mbali kila daraja inachukuliwa hatua zake. Sasa hapa katika utekelezaji halisi unasema, "Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ameondolewa katika wadhifa huo kwa barua yenye kumbukumbu hiyo hapo iliyotajwa ya tarehe hiyo hapo iliyotajwa. Aidha, mhasibu mwengine ameshapelekwa kwa barua nambari hiyo hapo". Sawa.

Sasa mimi swali langu liko hapa, kwanza Baraza la Manispaa lilikuwa halina Mkurugenzi moja kwa moja isipokuwa lilikuwa lina Kaimu Mkurugenzi, na yule aliazimwa kutoka ZRB. Sasa sijui tupate ufafanuzi kwamba je hii barua yake ilisema kwamba unarejeshwa katika ile nafasi yako ya zamani kule ZRB au vipi. Kwa sababu barua ya kuachishwa ukurugenzi yeye si mkurugenzi sasa hiyo barua sijui ilikuwa imeandikwa vipi, pale alikuwa anakaimu tu ile nafasi kwa sababu ilikuwa bado haijatangazwa.

Lakini jengine Mhe. Spika, mimi ninavyojua kwamba mpaka ile Ripoti ya Kamati Teule inawasilishwa kama sikosei nafikiri Mhe. Waziri atakuja kuniweka sawa, Mkurugenzi huyu alikuwa tayari kuna nafasi aliomba katika ngazi za kichama na alikwishakuandika barua ya kuomba kuachia nafasi ile na kushiriki moja kwa moja katika ngazi ya chama. Sasa sijui lipi lilikuja mwanzo lipi lilikuja mara ya pili. Kwa hivyo, sasa hatujajua hii barua kwa sababu ni siri ya serikali labda wangelitupa tu maelezo Mhe. Waziri kama pale aliondolewa je amerejeshwa kule alikokuweko au ameondolewa moja kwa moja yuko nje ya serikali, nilikuwa hili nataka ufafanuzi.

Lakini jengine Mhe. Spika, hapa kulikuwa kuna suala la utata katika suala la ununuzi wa basi, lakini vile vile hatukuweza kupata ufafanuzi wake. Lakini ndio kama nilivyoshauri Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri atakuwa leo hakujiandaa katika hilo basi nadhani akija akikaa na hiyo kamati ili kujua zile taratibu ambazo kamati ilihisi kwamba zilikiukwa.

Jengine ambalo nategemea ndilo litakuwa la mwisho Mhe. Spika, naomba ninukuu Ripoti hii ya Taarifa ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi inayohusiana na Baraza la Manispaa. Naomba ninukuu ukurasa wa 33, kuna kifungu kinasema kwamba, "Aliendelea kutueleza kwamba baada ya Baraza kuamua kumpa maduka mawili alitaka kujua hatma ya fedha zake zilizosalia ambazo ni shilingi 38 milioni". Kwa hivyo, hapa kuna Ndugu Suleiman alikuwa analidai Baraza la Manispaa baada ya kujenga lakini baadae maduka akapewa mtu mwengine.

Mhe. Spika, anasema, aliendelea kutueleza kwamba, baada ya Baraza kuamua kumpa maduka mawili alitaka kujua hatma ya fedha zake zilizosalia ambazo ni shilingi 38 milioni. Ndugu Vuai alimtaka akachukue shilingi milioni kumi kama kianzio cha fidia cha gharama zake alizozitumia, ingawa baadae alijuilishwa kwamba fedha hizo zimeingia kimakosa kwenye *account* ya Ndugu Ramadhan Abdalla Songa ambaye kwa muda huo alikuwa Dar es Salaam siku chache baadae aliambiwa tena na Ndugu Vuai kuwa akachukua shilingi 20 milioni lakini majibu yalikuwa ni

yale yale kwamba fedha hizo zimeingia kimakosa tena kwenye account ya ndugu Ramadhan Abdalla Songa na amekwenda Dubai kuzifanyia biashara.

Sasa Mhe. Spika, hizi fedha inamaana ni fedha za Baraza la Manispaa, ni fedha za umma lakini zimeingia kimakosa katika *account* ya mtu binafsi Ndugu Ramadhan Abdalla Songa kama ilivyoelezwa humu tena zimeingia kimakosa mara mbili. Mhe. Spika, mimi ninavyojua mtu kweli hukosea lakini hukosea mara moja akaambiwa umekosea hakosei tena. Sasa lakini huyu *account* shilingi milioni kumi zimeingia kimakosa, halafu tena shilingi 20 milioni zimeingia tena kimakosa, tena mara ya mwanzo zimeingia kimakosa yeye mwenyewe hayupo yuko Dar es Salaam, mara ya pili zimeingia tena kimakosa anatafutwa huyu mtu anaambiwa amekwenda Dubai kufanya biashara.

Kwa hivyo, inaonesha kwamba watendaji wetu tuliowapa dhamana hasa ukusanyaji wa fedha basi wakishakusanya fedha kwanza wanapeana wanakwenda kufanyia biasara Dubai wakishapata faida tena baadae aidha kama wenyewe hatujalala wanazirejesha lakini kama tumelala ndio inakuwa zimetoka. Sasa Mhe. Spika, tunataka tujue hizi fedha zilizoingia kimakosa tena hii *account* ya Ndugu Ramadhan Abdalla Songa itabidi Mhe. Spika, ifanyiwe kazi, kwa sababu hata sisi katika ripoti ya mwanzo huyu Ndugu Ramadhan alihusika vile vile tena katika mambo haya haya ya fedha.

Mimi naomba Mhe. Spika, kwa nguvu za Baraza tulizokuwanazo ifuatiliwe *account* ya ndugu Ramadhan Abdalla Songa ijulikane, huyu inawezekana anatumiliwa sana katika kuiba fedha za umma. Sasa Mhe. Spika, hizi fedha hatukujua baada ya kukosewa na huyu baada ya kurudi Dubai zilirudi ndani ya Baraza la Manispaa au tena ndio zilielekea Dubai kwa ajili ya kwenda kufanya biashara.

Sasa Mhe. Spika, mambo kama haya yashawachosha wananchi, *account* za serikali tunazijua zimo na *account* za mtu binafsi. Kwanza huwezi ukaingiza fedha katika *account* ya mtu bila ya kumtaja jina lake na kujua *account number*, ndio maana nikasema hii *account* ya Ndugu Ramadhan Abdalla Songa hebu ifuatiliwe, hii inaonesha inatumiwa vibaya na watendaji wetu. Mimi nafikiri Mhe. Spika, kama kusema tumeshasema sana, serikali kama inasikia ndio isikie, kama haisikii basi tena, sitaki kurejea aliyoyazungumza Mhe. Ismail Jussa kwa sababu sisi wengine tukizungumza lugha nyengine tunaambiwa maneno mengine ya kiajabu ajabu.

Sasa baada ya haya machache Mhe. Spika, nakushukuru. Mimi nafikiri kama nilivyosema naamini haya Mhe. Waziri kwa ghafla jawabu atakuwa hana, lakini mimi nadhani kama akikaa na kamati tutaweza kuja kupata jawabu ambazo zitakazokuwa sahihi kabisa ili wajumbe kwa ile kazi kubwa na nzito waliyofanya waridhike kwamba wameifanya kwa niaba ya wananchi na fedha za wananchi hazikupotea bure. (Makofi)

Mhe. Spika, nakushukuru. (Makofi).

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, nikushukuru kwa dhati na mimi kupata nafasi hii kuchangia mapendekezo ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na uhai mchana huu kupata nguvu kuweza kuzungumza machache katika Baraza hili lako tukufu.

Mhe. Spika, nianze kwa pongezi za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule. Naanza kwa pongezi Mhe. Spika, kwa kupongeza zile hatua za awali ambazo serikali imeanza kuonesha nia ya kuzichukua baada ya taarifa ile ya Kamati Teule.

Nazo hatua ya mkurugenzi kama taarifa inavyoeleza kwenye kumbukumbu za barua zinavyoonesha na hatua ya mhasibu na yeye kama kumbukumbu zinavyoonesha. Hii ni imani kwamba serikali yetu inajali maamuzi ya Kamati zinazoundwa na wanakuwa tayari kuzifanyia kazi.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo lakini na mimi pia sitoacha kuzungumza yale machache au yale mapungufu ambayo yameonekana na hayakuweza kuchukuliwa hatua. Na kwa kweli Mhe. Spika, nakuwa napata kigugumizi cha kutosha sana. Mara nyingi huwa tunajifunza kutokana na matendo ya wenzetu na ndio hata maana Mhe. Spika, Baraza lako hufikia wakati likatoa wajumbe kwenda kujifunza maeneo mbali mbali ya nchi za wenzetu jinsi ya ufanisi ya utendaji wa kazi kwenye serikali zao.

Mhe. Spika, mara nyingi tunaunda Kamati Teule na kwa hesabu ambazo zinazotajwa mara kwa mara. Kamati Teule tatu tayari zimeshatoa taarifa na tunasubiri ya nne ile ya ardhi. Lakini cha kushangaza kwamba pamoja na hatua ambazo tunazichukua lakini bado uimara wa hatua unakuwa hauonekani katika yale mambo ambayo yamependekezwa.

Mhe. Spika, mwaka jana hapa mimi nilimsifu sana yule mkurugenzi wa vipodozi Ndugu yangu Burhan na nikawahi kumpa jina kwamba ni Magufuli wa Zanzibar. Mhe. Spika, wenzetu wamebadilika na zinapoundwa Kamati Teule, maamuzi yanapofanyika basi na wananchi huwa wanapata faraja kubwa sana.

Mimi ningetoa maombi kama inawezekana basi tukamsome mwenzetu Ndugu Mwakyembe. Mhe. Spika, yule ni waziri mahiri sana na kwa kweli kamati zote zinazoundwa kupitia wizara yake basi hatua zinazochukuliwa kila mtu anakuwa anaridhika na lile suala ambalo lililochukuliwa.

Mhe. Spika, sababu ya kusema hivyo kwamba pamoja na mazuri ambayo tayari yameanza kuchukuliwa hatua, lakini na mimi nataka kuzungumzia kwa yale ambayo sijayaona kwenye hii taarifa au mapendekezo ya utekelezaji.

Mhe. Spika, katika taarifa ya Kamati Teule walitajwa maafisa mbali mbali ambao walihusika katika mambo mbali mbali katika namna moja au nyengine. Sasa katika taarifa hii tunaelezwa kwamba kuna baadhi ya masuala yanahitaji kuwaslishwa kwa Katibu Kiongozi ya ngazi ya ukurugenzi.

Lakini kuna maafisa kwa mujibu wa sheria za Baraza la Manispaa hawa hawahusiki katika katika suala la ngazi ya ukurugenzi, lakini hadi sasa watu hawa hakuna hatua ambazo zimechukuliwa. Na hatukuona taarifa zao ndani ya haya mapendekezo.

Mhe. Spika, mule yalizungumzwa masuala ya mabango, mambo ya uajiri, kuna mkuu wa utumishi ambaye ndiye kwa mujibu wa sheria za Baraza la Manispaa anakuwa ndiye katibu wa kamati ya sheria ya Baraza la Manispaa. Sasa hii inakuwa ni mamlaka ya taasisi ya Manispaa pamoja na wizara.

Sasa Mhe. Spika, sijui sababu gani au ugumu ambao unaotupelekea na ile ndio imani ya wajumbe wako ndipo pale inapoanza kuondoka kutokana na hali halisi ya yale mambo ambayo hayakuweza kuchukuliwa hatua, mambo ambayo yamo ndani ya mamlaka yetu. Mimi nilitarajia leo hapa nione kwamba muhusika fulani na fulani, hawa angalau wamehamishwa kutoka eneo fulani kwenda eneo fulani.

Sasa hii Mhe. Spika, ndio kitu ambacho kinakuwa kinatupa mashaka katika maamuzi ya haraka kwenye hizi Kamati Teule ambazo zinazoundwa, Kamati ambazo zinatumia pesa nyingi za wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, jengine ambalo linakuwa linanipa kazi sana ambapo mimi kwa kweli katika mapendekezo haya, kidogo bado yananipa mashaka. Ningemuomba Mhe. Waziri labda atutafutie jawabu ambalo sisi tunaweza tukaridhika nalo.

Mhe. Spika, lilizungumzwa suala la Darajani na katika taarifa humu imeeleza namna ya hatua ya kutaka kuwapeleka Saateni. Lakini linalotupa taabu Mhe. Spika, kwamba suala la kwenda Saateni watu wa Darajani Mhe. Spika, suala hili limekuwa kama mchezo wa kuigiza. Serikali inakuwa inatumia nguvu kubwa, Baraza la Manispaa inashirikiana na vikosi katika kuondosha watu wale lakini huwa haichukui muda, ndani ya mwezi mmoja au miwili hatua zilizochukuliwa basi zinakuwa zinarudi pale pale.

Sasa labda Mhe. Waziri anaweza kuja kutueleza labda mbinu mbadala ambazo wameamua kuzichukua katika kuondosha watu wa Darajani kuelekea Saateni. Na tumejaribu kutoa mapendekezo mbali mbali wakati tangu tupo katika Baraza la Manispaa Mhe. Spika, kwamba basi kuna haja baadhi ya mambo kama soko la Darajani kupelekwa Saateni, basi baadhi ya mambo yapelekwe Saateni, otherwise Mhe. Spika, huu mchezo utakuwa ni wa kuigiza.

Mhe. Spika, tulitoa mapendekezo kwamba baadhi ya gari lazima *route* yake ielekee Saateni baada ya kuja kituo cha Darajani pamoja na zile huduma muhimu katika lile eneo. Lakini kama ninavyozungumza haya mambo yamekuwa yamezoeleka, operation huwa zinatumika lakini baadae gari hukatisha route zinakuja Darajani na wale wafanyabiashara nao wanaamua kurudi pale pale kufanya biashara zao. Sasa sijui Mhe. Waziri katika mapendekezo yake mikakati ambayo ameiandaa katika suala hili, maana yake hatujaliona kabisa.

Lakini chengine Mhe. Spika, ambacho ninataka kukizungumzia ni jinsi ya mapendekezo yalivyoelezewa katika masuala mazima ya masoko na hususan walivyozungumzia soko la Mwanakwerekwe na soko la Mombasa.

Mhe. Spika, mimi ninasema kwamba kama walivyozungumza wenzangu umakini katika utendaji wa kazi bado haujaonekana. Haya mambo Mhe. Spika, tunayaleta hapa leo wakati mambo haya tayari yalikuwa yameshafanyika katika siku za nyuma. Mhe. Spika, hakuna aliyekuwa hafahamu kwamba soko la Mombasa ambalo ndugu zetu za Kichina walilijenga kuwasaidia ndugu zetu wa Manispaa, lilikuwa ni soko la mboga mboga. Paliwahi kupelekwa mnada, mnada ukaondoshwa Mwanakwerekwe ukapelekwa soko la mboga mboga, lakini katika mazingira haya haya yasiyoeleweka lile soko liliachwa likawa tupu, soko likawa genge la wahuni, linatumika katika yale mambo ambayo hayajakubalika.

Sasa sijui Mhe. Waziri ile njia mbadala ambayo aliyoiona ya kuweza kulirejesha soko la Mombasa liweze kutumika katika haiba yake na kuondosha ule msongamano katika soko la Mwanakwerekwe ambapo hivi sasa linakuwa linapelekea ajali mara kwa mara.

Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba mapendekezo nimeyapokea lakini niseme kwamba kuna haja kama walivyozungumza wenzangu ya kukaa na kuona zile kasoro ambazo basi hazikuingizwa katika haya mapendekezo ili yafanyiwe kazi kwa haraka sana, ili kuweza kujenga imani ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru. Ahsante sana. (Makofi).

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuamka kwa hali ya uzima na usalama.

Lakini Mhe. Spika, kwa kweli nimesimama nimenyong'onyea. Maana yake hata hii, hata sijui niseme nini jamani. Mhe. Spika, mimi wengine munatuweka kwenye kona kwa sababu sisi dhamira yetu ni kuwatumikia wananchi na kuwatetea yale ambayo yanawakwaza, ndio tulimoletewa humu kwenye Baraza. Hatukuletwa humu Mhe. Spika, kuja kuchukua posho na kukaa nyumbani tukala na familia yetu. Mhe. Spika, tumeletwa kwenye Baraza hili tukufu kwa imani ya wananchi kwamba tutawatetea haki zao. Lakini leo Mhe. Spika, nimebogonyoka kuona kwamba buku hili mapendekezo yaliomo humu tumejibiwa kwa karatasi nne au tano hizi au saba na hamna kinachofahamika humu. (Makofi).

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesoma kule sisi tumekaa hatujui tufanye nini. Amesoma karatasi yake, mapendekezo yake yeye mwenyewe na hayo hatujui kitu gani kimo ndani. Lakini baadae kasoma karatasi hii na hii haifahamiki Mhe. Spika. Hii si ripoti Mhe. Spika, na tunasema kwamba haya ni mapendekezo ya kamati, kama kukiwa na warsha, kukiwa na nini, mapendekezo ni maazimio na haya ni maazimio ya Baraza. (Makofi).

Kwa hivyo leo tunaletewa kitu kama hiki Mhe. Spika, jamani munatuweka kwenye kona wenzenu wengine. Tunatafsiriwa vibaya na baadhi ya wenzetu, kweli lakini sisi tutasema. Mhe.

Spika, niseme kwamba serikali ni lazima ipime, itafakari, iwe na ufanisi, kusimamia mambo ambayo ni ya umma na sisi ndio wasaidizi wa serikali.

Lakini leo Mhe. Spika, mimi ninashangaa. Kipindi kilichopita utumbo mtupu wa Baraza la Manispaa, ninathubutu kusema hivyo. Leo tunaletewa mengine yale yale, mimi sielewi. Mhe. Spika, kwa sababu na mimi nilikuwa ni mwana kamati wa Kamati hii ya Manispaa, jamani kwa kweli kazi tuliyoifanya wengine Mhe. Jussa shahidi, Mhe. Mwanaidi kwa sababu mimi nilitaka kupigwa pale soko la Mwanakwerekwe.

Sasa inafika hali kama hiyo kwa kuwatetea wananchi, halafu watu wanakuja hapa wanatusomea mambo ambayo hayaeleweki. Mhe. Spika, sitokuwa tayari, nasema kwa kinywa kipana sito kuwa tayari. Tuchukue juhudi, serikali ithamini yale mambo ambayo kwa kweli tunaifanyia serikali ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi).

La mwisho Mhe. Spika, na mimi nasema tukae na Mhe. Waziri ili tujadili moja baada ya moja tukubaliane. Kwa sababu kwanza mimi nilikuwa na wasi wasi, mimi nilifikiri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio itakuja kutuwasilishia kwa sababu na yeye Mhe. Waziri humu ameguswa.

Lakini nashangaa ndio tumeshaipokea hii. Lakini bado turudi na Mhe. Waziri tuhakikishe tunapitia moja baada ya moja ili pale ambapo panahitajika kuchukuliwa hatua za kisheria zichukuliwe, pale ambapo panahitajika kuna marekebisho tuyarekebishe kwa pamoja Mhe. Spika. Mhe. Spika, ninaiomba sana serikali.

Baada ya kusema hayo, niseme ahsante sana Mhe. Spika. (Makofi).

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kuchangia hoja hii iliyoopo mbele yetu.

Mhe. Spika, jana tulikuwa na ripoti ya Kamati Teule kuhusu Shirika la Umeme lakini sisi tupo karibu sana na wananchi, kwa sababu wananchi wanatuona. Baraza letu lilikuwa wananchi wa Zanzibar hawataki kulisikiliza na kuliangalia. Tumefika mahali wananchi wanatusikiliza sana na wanatuangalia sana na kufuatilia kwa makini.

Mhe. Spika, wakati ukisomwa ripoti hii ya Shirika la Umeme imefika hadi wananchi kutwambia kama aah! sisi tumeshazoea munakwenda mukikaa pale mukihubiri tu, mukisema na mukishasema ni basi, ndio yameshamalizika hivyo.

Sasa Mhe. Spika, kila tukija tunasema kama hiki ni chombo ambacho kinaangalia na wananchi na matumaini yao yote wanaangalia hiki chombo. Sasa Mhe. Spika, tunapounda Kamati Teule ya kuchunguza kitu chochote kile mpaka ukifika muda wa kuwa wewe mwenyewe Mhe. Spika, ukubali kuunda Kamati Teule, huwa suala hilo lina matatizo na matatizo hayo huwa yamemshaonekana kuna shaka.

Sasa kama kuna shaka inaundwa kamati ili waende wakaangalie kujiridhisha na kuona jee kweli kuna matatizo? Sasa Mhe. Spika, ilipoundwa Kamati ya Kuchunguza ripoti hii ya Baraza la

Manispaa, watu walikwenda wakaangalia kwa umakini mkubwa na wakaleta vielelezo, si kwamba ripoti imekuja tu hivi hivi, kila panapochunguzwa kuna na vielelezo.

Sasa Mhe. Spika, mukija mukitupa ripoti kama hii ndio pale watu wanaposema kuwa serikali bado haijawa tayari inakigugumizi. Jana hata kuna mtu alisema kama serikali ina kigugumizi utekelezaji wa mambo haya. Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais akasema serikali haina kigugumizi.

Leo Mhe. Spika, tunapokuja tukapewa ripoti kama hizi, tunaambiwa kuwa mkurugenzi tayari keshaondolewa lakini mhasibu mkuu kahamishwa hapa kapelekwa eneo jengine. Sasa mtu afanye makosa huku apelekwe sehemu nyengine ndio itakuwa ameondolewa, hao watendaji watakuwa na wasi wasi kwa sababu akifanya makosa huku anaondolewa anapelekwa sehemu nyengine, hana wasi wasi.

Mhe. Spika, kwa utekelezaji huu wa serikali unavyokwenda basi watendaji wataona kama tunakuja tukiimba hapa tukipiga ngoma tukicheza ikisha tukiondoka. Mhe. Spika, ripoti ilivyokuja kwa kweli haija kidhi haja hatujaona hasa utekelezaji wa serikali, pamoja na kuwa imesema kwamba inatakiwa yafuatiliwe na kuchunguzwa, lakini kuna mambo mengine yana vielelezo kamili na hivi sasa ni miezi mitatu zaidi tangu kusomwa ripoti hii, hivyo uchunguzi wa serikali tangu siku hiyo mpaka leo haijafuatilia kunangojwa nini, na wakati kuna vielelezo kamili, kama mfano wa hawa watu wa maduka kuna vielelezo vyote. Kwa hivyo serikali tayari ilikuwa imeshapita na kuangalia.

Lakini leo munakuja kutupa ripoti kama hii, sitowashangaa kwa kusema ukweli na bado tunaona kama mimi nasema vile vile kama serikali haijawa tayari na huruma na watu wake, kumuondoa mtu kwa sababu ya uharibifu wa mali ya umma inamuonea haya. Kwa kweli kusema ukweli basi tuna haja gani ya kuunda Kamati Teule, hatuna haja ya kuunda Mhe. Spika, fedha za serikali zinazotumika ni nyingi kwa sababi Kamati Teule inapofanya kazi inatakiwa ifanye kazi kwa ufuatiliaji na inafuata kwa sababu ya kuwezeshwa kwa fedha za serikali za umma.

Leo ripoti zinaletwa kamili, vielelezo vipo serikali haijawa tayari kufuatilia na kumuondoa mtu kwa sababu ya ubadhirifu wa mali ya umma. Juzi tu tumepitisha sheria ya rushwa hapa katika Baraza hili. Sasa watu hawa wakaonekana, bado munawalinda munawaonea haya, basi yamefanywa makosa. Kwenye ripoti hii ni huyu mkurugezi wa Baraza la Manispaa hakuna watu wengine waliofanya ubadhirifu na ubaya. Jamani munatupeleka wapi.

Tunaposema hapa jamani tunasema sisi serikali tunawasaidia, kwa sababu kamati inapofanya kazi inaisaidia serikali, inaisafisha serikali. Leo bado munawalinda watu, munaona taabu munawahifadhi watu, kumuwajibisha watu munawaonea haya katika kufanya ubadhirifu, yeye hakuona haya kula mali ya umma, nyinyi munamuonea haya.
“Ukimuacha mwana kulia mara waja lia wewe”. Kwa maana hiyo serikali munawaogopa watu munapakwa matope nyinyi, maana yake wananchi watakosa imani na nyinyi.

Sisi tunasema hapa na watu wanaona tunanawa, tunanawa kwa wananchi mpaka kwa Mwenyezi Mungu. Mtu amekwishafanya makosa munamlinda. Ripoti kama hii aliyokuja kutupa Mhe. Waziri ni ripoti gani, hii kweli inakidhi haja hii. Hatuoni uwajibikaji mtu anayewajibisha.

Jengine Mhe. Spika, naomba nimuombe Mhe. Waziri, nakuomba tushapiga kelele sana ndani ya Baraza hili, tushasema sana, kama uso wa mji huu Zanzibar pale Darajani ni mso mmoja wa mji wa Zanzibar. Mhe. Spika, jaa liliopo pale lenye harufu mbaya inasababisha mji mzima unanuka ni aibu. Mhe. Spika, lile jaa lifanyiwe shauri lihame, tushakwambia sana humu mara kumi. (Makofi).

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. (Makofi).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusiana na huu utekelezaji wa serikali kuhusiana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Teule.

Mhe. Spika, ripoti hii kwa kweli imenifanya hivi sasa nisifu sana hii hawa backbeachers waliopo katika Baraza hili. Ni kwamba wana uwezo mkubwa sana na wapo makini katika kuhakikisha kwamba wanawapatia utumishi ulio makini na wenye kukumbukwa wananchi wa nchi.

Kwa sababu Mhe. Spika, unapoteuwa Kamati Teule kwenda kuchunguza mambo huko, kupitia huku backbeachers, kwa kweli wapo makini sana katika kufanya kazi uliowakabidhi. Inaletwa ripoti hapa ikiwa na supporting evidence. Leo tunaletewa yaani hii taarifa ya Kamati Teule utekelezaji wake vijikaratasi hivi Mhe. Spika. Taarifa yetu ilikuwa ni kubwa na mafaili ya *supporting evidence*, leo tunaletewa hivi, mimi naita kama *verbal statement* ni kauli za mdomo tu basi bababa!.

Kwa kweli Mhe. Spika, serikali yetu hii ya GNU haipo *serious* na inafanya mzaha na fedha za walipa kodi wa nchi hii. Sisi tunaipenda sana serikali hii Mhe. Spika, kweli kweli, sisi *backbeachers* tunaipenda sana GNU kuliko hawa mawaziri, nataka ufahamu hilo Mhe. Spika. Na mimi huwa naumia sana Mhe. Spika, pale mjumbe anaposimama akasema serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, huwa naumia sana kwa sababu serikali ya Chama cha Mapinduzi hii, ni hizo zilizopita, hivi sasa ni serikali ya GNU ambayo ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa; Chama cha Mapinduzi wapo na CUF wamo. Kwa hivyo ni yetu sote pamoja na sio ya Chama cha Mapinduzi. Naomba sana Mhe. Spika, wajumbe wakichangia waseme kwamba serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu sote tumo. (Makofi).

Sasa niende moja kwa moja Mhe. Spika, hii ripoti siiungi mkono na kama ingelikuwa si kuvunja sheria ningeliichana lakini naogopa kwamba nitakiuka Kanuni. Mhe. Spika, huwezi kuleta ripoti hii kwa watu intellectual kama sisi *backbeachers* tuliopo huku.

Mhe. Spika, hivi juzi tuliambia kwamba tunataka kuingia kwenye *e-Government*, tukapewa semina kule Hoteli ya Zanzibar Beach Resort kwamba tunataka kuingia kwenye *e-Government*.

Sasa ripoti kama hii kama tumeshaingia kwenye *e-Government* yupo jamaa yangu wa Kizanzibari yupo London Uingereza nampelekea ripoti kama hii, si atatutia aibu serikali yetu. Ninadhani Mhe. Spika, katika hili arudi Mhe. Waziri na karatasi zake tano hizi, wakae watuletee ripoti ambayo ina mashiko, ina mashiko.

Kwa mfano tumebabaishwa tu hapa, hebu niende kwenye *item number one.* "Pendekezo au shauri ilikuwa ni mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine kutokufuata sheria na Kanuni mbali mbali kuchukuliwa hatua". Lakini utekelezaji anakwambia kwamba mkurugenzi wa Baraza ameshaondolewa katika wadhifa huo kwa barua yenye kumbukumbu namba, angetwambia kiambatanisho cha barua hii nimekiweka nyuma ni kiambatanisho namba fulani, yeye kasema mkurugenzi tu wakati huku taarifa imesema na watendaji wengine.

Sasa hii ni kutudharau Mhe. Spika, ina maana aliyekuwa hakufuata sheria ni huyo mkurugenzi tu. Tumedhalilishwa sana katika hili. Mimi nadhani kwa mujibu wa kumbukumbu tuliyonayo ni kwamba huyu mkurugenzi aliomba nafasi kubwa sana katika chama kimoja kikubwa sana katika nchi hii na akashinda nafasi ile. Aliposhinda nafasi ile inaonekana sheria hazimruhusu tena kuwa mtumishi wa serikali, kakaa pembeni tu, kwa hivyo mimi ninataka Waziri huyu atuletee barua hiyo yenye kumbukumbu namba hii ili tujiridhishe na sisi na tuwaridhishe wananchi.

Mhe. Spika, *item number 3,* naomba kidogo niinukuu inasema kwamba "Baraza la Manispaa lifanyie matengenezo masoko yake kwa kulinda dhana ya soko na sio kujenga maduka ya kudumu ambayo yataondosha dhana. Hatua ya utekelezaji ni kwamba hatua ya kuwasilishwa imefanyika kwa barua nambari hiyo iliyoainishwa hapo".

Mhe. Spika, mimi nadhani Baraza tunababaishwa vile vile kwa hapa. Sasa barua imepelekwa, jambo hawajawa na uwezo wangetuambia *cost estimate* tunayotaka kutumia ni hii. Lakini hata makisio ya ujenzi huu hatukuwekewa ni barua tu, hili ni tatizo Mhe. Spika. Uwezo kama haujakuwepo, basi wangetuletea *cost estimate* ya hizo gharama atakazotumia huyu Mhe. Waziri katika kutengeneza hayo masoko, asitubabaishe kiasi hiki na kama angetuletea *cost estimate,* hata hili Baraza pengine lingemsaidia kufanikisha huu utekelezaji. Hilo jengine.

Mhe. Spika, *item number 5* lijengwe soko kubwa litakalokidhi haya. Majibu ni ya kubabaisha mno na ni ya dharau, kwa sababu hayakukidhi hili pendekezo lenyewe. Kwa mfano agizo lilisema serikali ijenge soko kubwa ambalo litakidhi haja kwa wafanyabiashara wetu. Lakini baada ya kuzungumzia soko kubwa, utekelezaji amejibu vipi. Anasema tayari soko la Mombasa limesharejeshewa huduma za maji. Hakuambiwa arejeshe huduma za maji huyu bwana, ajenge soko kubwa, hivi ni kutubabaisha.

Mhe. Spika, mara nyingi tunasema kuwa hiki ni chombo kikubwa sana cha nchi na hata asubuhi hapa, ndio ikabidi nikamueleza Mhe. Waziri ndugu yangu Mohamed Aboud, kwamba hiki ni chombo kikubwa mno, mtu anatakiwa awe na uhakika na anachokisema. Sasa sisi tumemueleza ajenge soko, yeye anataka kurudisha huduma za maji, huu ni ubabaishaji Mhe. Spika.

Mimi nadhani Mhe. Spika, kuna mengi sana, lakini nimetaja haya machache. Kwa hivyo, naomba kuwa hii taarifa haifai, irudi serikalini wakakae watuletee taarifa ya utekelezaji huku ikiwa imeegemezwa kwenye viambatanisho vya *supporting evidencies* na sio katika kutuletea hii *verbal statement.*

Baada ya maelezo haya Mhe. Spika, siiungi mkono hii ripoti na naiomba irudi serikalini, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu kidogo juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar.

Kwanza Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa na pia nikushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi. Halafu nimpongeze kidogo Mhe. Waziri angalau kwa kumuondoa huyu Mkurugenzi kwenye hili Baraza la Manispaa. Kwa hivyo, ningeomba tu nimuulize swali je, baada ya kumuondoa hapa ndio kasimamishwa kazi, kafukuzwa kazi au kapangiwa kazi pahala pengine kwenye taasisi za serikali.

Mhe. Spika, chombo kinapoundiwa kamati teule, maana yake kuna matatizo ambayo chombo hicho kinahitaji kuchunguzwa. Yule aliyebainika kuwa ana kosa fulani ndio anachukuliwa hatua za kinidhamu au za kisheria. Kwa hivyo, hapa nadhani mkurugenzi kachukuliwa hatua hiyo nadhani ya kinidhamu. Lakini nikipongeze sana Chama cha Mapinduzi, kuwa baada ya kadhia zote hizo alizofanya mkurugenzi katika Baraza la Manispaa, imempa nafasi ya juu ya katika Chama cha Mapinduzi kawa ni mjumbe wa NEC, kwa hivyo kwa hili nawapongeza.

Mhe. Spika, nitazame *item* nyengine kuwa baada mkurugenzi pale, ikifuatia chini kuna majukumu yanayochunguzwa. Sasa hii ripoti tokea wakati ilipowasilishwa hadi leo hivyo kweli wizara hii haina watendaji makini wa kuweza kuchunguza na leo kuweza kuletewa ripoti ambayo ni kamilifu. Ina maana baada ya huo uchunguzi ripoti hii inarudi tena hapa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi siridhiki kuwa bado uchunguzi unaendelea. Uchunguzi kuendelea ni sawa sawa na ile tuliyozoea wenyewe kusema mipango iko mbioni. Mara nyingi mimi husema mipango ina mbio kuliko sisi na huenda mipango tusiikamate. Kwa sababu kazi inaendelea basi maendeleo haya yanakuwa hayana mwisho. Mhe. Waziri angetuambia hasa ni lini ataweza kutupa ripoti inayokidhi haja na kazi ya kamati iliyofanywa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, mimi naomba nikushukuru na niseme tu kwamba nadhani kwa mujibu wa kanuni ni kosa sana kupoteza wakati. Kanuni inawakataza Wajumbe kwamba wakiwa hawana sababu ya msingi wasipoteze wakati.

Kwa hivyo Mhe. Spika, niwaombe Wawakilishi wenzangu baada ya mimi wanikubalie tusipoteze wakati. Kwa sababu kuijadili ripoti hii madamu Mhe. Waziri ametudharau, maana yake anakusudia kupoteza wakati.

Mhe. Spika, mimi ni mwaka wa saba na nusu huu kuwa Mwakilishi, tangu tuko Kikwajuni mpaka hii leo, nina historia ya waziri huyu kutuchezea sisi. Nadhani kwa sababu yeye ni *PhD holder*. Sasa mtu mwenye *PhD* na mimi mwenye digrii ya Mwambe na Mhe. Hamza Hassan ya Kwamtipura, sio saizi yetu kusema ukweli.

Mhe. Spika: Rudi kwenye hoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Ahsante Mhe. Spika. Kwa hivyo, hoja yangu ni kwamba kwa sababu pengine ya udhaifu wetu ndio mara zote akatuletea ripoti ambazo hazina mantiki, na kwa kweli ni aibu ya serikali na sisi wengine hatuko tayari serikali hii ikaaibishwa kwa makusudi. Sasa majibu ya Mhe. Waziri kipindi cha kwanza mpaka mwisho ni mzaha. Anaonesha kana kwamba wale watendaji waliotajwa humu hawajui. Anawajua lakini anaona aah! Niwaambie nini. Mhe. Spika, nikuombe umwambie ageuke huko juu aangalie. Yeye kama Waziri atuambie huko juu kuna mtendaji gani wake yeye anayemsaidia hizi hoja, hakuna. Waziri maana yake anafanya kazi kwa mujibu wa watendaji. Nina hakika leo akitoka hapo nje hanayo haya tuliyomwambia. Sasa kama nchi inapelekwa hivyo, tena ni waziri ambaye yuko katika Ofisi ya Rais tutafika wapi.

Mhe. Spika, kuna kila sababu ya kuwaomba Wawakilishi wenzangu, baada ya mimi wanikubalie tukuruhusu tupige kura na kura yenyewe ni kwamba arudi nayo, akitaka awaambie wamsaidie hakutaka basi asije nayo. Kwa mujibu wa kifungu cha 5(a) cha katiba, serikali inawajibika kwa pamoja, kama hakuweza peke yake basi kuna wataalamu huku kina kaka yangu Mhe. Haroun wangemsaidia majibu mazuri. Lakini kama pengine amekumbuka jana kwamba aah! Kunatakiwa jambo fulani, ndio matatizo yake haya Mhe. Spika,

Mimi nikuambie Mhe. Spika, kwamba wenzetu hawa wamefanya kazi mwezi mzima, wamepoteza pesa nyingi za wanyonge, ndio majibu yake haya hapa. Mtoto wangu wa darasa la 4 anayejifunza kompyuta basi anaweza akayaandika haya, ukimwambia tu andika hivi atayaandika haya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Waziri ama kakusudia kutudanganya na kwa mujibu wa kinga na fursa za wajumbe kwa mujibu wa sheria nambari 4 ya mwaka 2007 ni kosa kubwa kudanganya. Mimi namuomba sana kwa heshima kubwa kwamba tumeshakoma atuachie, ama atuambie siwezi kuwachukulia hatua ama atuambie kwamba musinikere. Lakini kila siku mambo yanazuka huko mitaani sasa hivi ni wizara hii hii kuna shutma ya ajira kwa pesa.

Lilikuwa ni jambo dogo tu la mtu ametajwa kuwa ni mbadhirifu Songa ametajwa humu, Songa katajwa katika ripoti iliyopita, Songa kesho kutwa anatarajiwa kutajwa kwenye ripoti ya ardhi inayokuja. Hawezi kuchukua hatua yoyote, tafsiri yake ni nini. Tafsiri yake itakuwa kuna jambo linalindwa. Sasa atuambie tunalinda nini, tusihangaishwe Mhe. Spika.

Mimi mara nyingi huwaambia wenzangu hapa yule mzee anakaa pale masaa 7, hendi hata chooni. Ni lazima tukufanyie haki na wewe, asije mtu hapa na hadithi zake za kitoto toto, wewe ndio unayeumia hapo ulipo, maana yake umekaa kutwa nzima unasikiliza maneno ya maana hayapo. Waheshimwia Wajumbe tumfanyieni haki yule mzee wa watu, tusimuweke pale kwa masaa 7 bila ya hoja ya msingi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba Mhe. Waziri kwa heshima kubwa hii karatasi yake achukue mwenyewe na ikiwezekana zote zikunjwe apewe mwenyewe, akitaka aje nayo tena hakutaka basi. Wazanzibari wanaona kwamba huyu hana dhamira ya kweli.

Mhe. Spika, juzi Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hapa alipoona kwamba ameteleza alituita na mambo ameyarekebisha, huo ndio ustaarabu. Alituita tukamuelimisha, akasema kweli hapa kidogo serikali imegonga mwamba na naamini anarekebisha mambo. Kwa hivyo, na yeye akitaka na arudi nayo na aje nayo tena na asipotaka basi. Wazanzibari wanaona na kwa kweli hatuwafanyii haki na kwa *speed* hii, licha ya China hata twende mbinguni hatufanikiwi. Kwa mawaziri kama hawa wanaodharau licha ya China, hata tupelekwe mbinguni tukajifunze hatufanikiwi.

Mhe. Spika, nawaunga mkono wenzangu kwamba hii ripoti irudi na siungi mkono hoja ya Mhe. Waziri. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Hija Hassan Hija nakushukuru na tumemaliza michango ya jumla, sijui kama kuna upande wa mawaziri, kuna mjumbe yeyote ama niende moja kwa moja kwa mwenyewe. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa wasaa huu wa kufanya majumuisho baada ya michango ya Waheshimiwa niliyopata wanane. Kwa kweli nawashukuru sana. Hii ni nyumba yetu ya ukweli na uwazi, hii ndio nyumba yetu ya kuelekezana, ya kukosoana, ya kuambizana.

Kwa hivyo, hii ndio demokrasia Mhe. Spika, unayoisimamia ndani ya nyumba hii. Mhe. Spika, mimi nayachukua haya kama wanavyosema wazungu ni *constructive criticism.* Yaani ni maoni ya kutukosoa kwa nia ya kuelekeza kwa kujenga.

Mhe. Spika, ningeomba sana ikiyumkini tujitahidi *hansard* yangu ya leo pale nilipotoa utangulizi, hebu ningeomba isambazwe kesho kabla hatujatawanyika. Kwa sababu maneno niliyoeleza ni maneno ya kujenga, ya kujirekebisha ndani ya taasisi yetu. Nawashukuru Wajumbe wame-*echo* yale yale yangu. Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kauli kali, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Subeit Khamis Faki na wengine. Sasa ndio yale yale niliyoyasema mimi. Tujirekebishe kwa kuleta tija katika utendaji wetu. Nilianza hivyo, nakumbuka nilisema kabisa hivyo, wala sikupotea kwa hilo.

Mhe. Spika, wale waliozungumza Mhe. Asha kwamba mawaziri hawafai. Sio kweli. Mhe. Ismail Jussa Ladhu anavyosema kwani si Mhe. Rais anajua yuko, utendaji wako si unaonekana, michango yako si inaonekana, sasa una wasi wasi wa nini wewe, wewe ngojea rizki tu, rizki itakuja. Siku moja rizki itaanguka tu, unafahamika LLB.

Kwa hivyo, mimi nataka kusema Mhe. Spika, tusiende huko, mimi sipendi ku-*respond* yale ambayo nimegongwa moja kwa moja mimi kama Mwinyihaji, naona mengine kama Mwinyihaji ambapo kwa kweli sio jambo zuri. Mpaka mtu anafika kusema PhD *holder* wanatudharau. Mimi

hakuna ninayemdharau ndani ya Baraza hili, ninamnyenyekea kila mtu, yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe namtania kila siku hapa. Aah! Mhe. Mjumbe jana hivi na hivi. Sasa dharau hiyo ya kuwa nina PhD, sasa labda ningekutania nikakuambia kwa nini na wewe umeogopa umande, ndio lakini hatufiki huko.

Kwa hivyo, mimi nafikiri Mhe. Spika, tusiende huko tuzungumze hoja. Hoja tunazipokea na nilisema mwanzo kwamba tunazipokea na tunazifanyia kazi, hatukukataa hata kidogo, tumekubali kwa uwazi kabisa na mapungufu tukasema tumeyaona. Lakini jamani miezi mitatu kutoa maamuzi ya utekelezaji. Manispaa pale kuna watu 810 kama sikosei, tunakubali kuna mapungufu makubwa sana, panahitaji *complete over rall* pale mahala. Mimi mwenyewe kama waziri napita mwenyewe na kufuatilia mikutano, ndio ile niliyosema tubadilike. Kwa hivyo, haya hatukatai Mhe. Spika, lakini sasa nafikiri tusiende huko Mhe. Spika.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe waliyoyasema tumeyasikia, tumeyachukua na kwenye *presentation* ya ripoti jamani kuna njia nyingi. Siku zote unapoweka njia ya bango kitita ya *matrix* ndio njia fupi sana ya kuonesha lile ulilotaka au pendekezo lililotoka au ushauri, hatua zilizotekelezwa au ulizopanga kutekeleza na utekelezaji halisi na maelezo. Mimi nataka mtu aniambie katika hii *summary* ambayo tumetoa kama kuna kitu ambacho hakikuguswa hapa. Haya ndio mapendekezo yaliyotoka humu ya jumla, haya ndio tuliyoya-*refer*, sasa hatuwezi tena kwenda kwenye moja moja, tuandike tutoe ripoti hii wenyewe wamefanya kama karatasi 65, halafu sisi tutoe ripoti nyengine ya karatasi 60 nafikiri sio sahihi. Sisi tumetoa hii ni *road map* yetu, narudia tena *road map* yetu, yaani mpango wetu wa kazi wa kuyatekeleza haya Waheshimiwa mliyoyasema. Hatukatai hata moja hapa, lakini ni lazima tuwe makini twende kitaalamu na mengi haya mambo ni ya kisheria.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la Mkurugenzi. Mkurugenzi keshaondolewa, kulikuwa na utata mwanzo kabla ya kuondoka kwake, lakini kwa ufupi tunasema keshaondoka, hayupo tena kwenye nafasi. Sasa tumesema kwenye *column* ile kwamba unatizamwa utaratibu wa kisheria, sisi hatuwezi kumshtaki. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kasema tufungue *file* sisi, aah! Jamani hatuna *mandate* hiyo, wanasheria wapo. Sasa lile limeshapelekwa ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Mkurugenzi wa Mashtaka kule tutafika, ili tuone ni makosa gani aliyofanya. Sio yeye tu, hata hao wengine, kwa hivyo hatuku-*rule out* wao kushtakiwa lalala eeh dada yangu Mhe. Asha anasema wanalindwa. Hapana, hatuwalindi, lakini ninachosema Mhe. Spika, zifuatwe taratibu, miezi mitatu kwa utekelezaji wa kitu kama hiki sio mingi hata kidogo, ile kujipanga wenyewe tu kuwa twende vipi, basi hiyo peke yake inachukua miezi mitatu na ndio hiyo tunayoifanya sasa hivi.

Kwa hivyo, mimi ningewaombeni Waheshimiwa msione hivyo. Mhe. Saleh Nassor rafiki yangu angeichana. Mimi nafikiri *matrix,* unajua *mode of presentation* kila mmoja ana yake, lakini kwa kweli kama unataka kitu uki-*condense,* sisi tume-*condense,* tumeibana, lakini kila kitu kimo humu, wewe ukitizama pengine itagusa mkataba, itagusa masuala ya wafanyakazi, itagusa labda hadidu rejea nyengine, lakini kila kitu kimo. Kwa hivyo, sisi tutakiweka tena, nini mkataba, basi unapitiwa mkataba, haki za wafanyakazi basi wafanyakazi. Kwa hivyo, humu hakuna kisichopo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, naomba niwashukuru sana kama nilivyosema Waheshimiwa Wajumbe waliopata wasaa wa kuchangia. Kwanza naomba niwataje;

- Mhe. Ismail Jussa Ladhu
- Mhe. Hamza Hassan Juma
- Mhe. Ali Salim Haji
- Mhe. Asha Bakari Makame
- Mhe. Saleh Nassor Juma
- Mhe. Mohamed Haji Khalid
- Mhe. Hija Hassan Hija

Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa lengo letu na sisi ni hivyo hivyo tutengeneze, wala penye uovu hatutomficha mtu uovu wake. Kwa sababu ndio hayo ninayosema sasa, ikiwa samaki mmoja kaoza basi tutaambiwa sote tumeoza. Hapana sio hivyo, inategemea lile kontena unavyomuweka yule samaki.

Kwa hivyo, mimi ninachowashauri Waheshimiwa ninawaombeni sana kuwa tupeni muda, huu tunasema ndio mpango wetu wa kutekeleza hayo mambo, hatukwenda kwenye *specific item* kama nilivyojaribu kuzungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu, labda twende moja moja, hapana. Lakini mambo yote humu yamo na hiyo tutajipanga na muhimu sana kwanza tuanzie na kubadilisha ule muundo wenyewe na mtizamo wenyewe wa lile Baraza la Manispaa, ili tupate wataalamu watusaidie, ilikuwa hatujui tuanze vipi na nyinyi wenyewe mmeona mapungufu yaliopo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nisingependa niwajibu mmoja mmoja, lakini yale mambo ambayo sikuyataja kama Songa na mengineyo, yote tumeyaona yale. Lakini ndio ninasema yote hayo ndio yanaingia kwenye mapitio ya mikataba, tutaona anayedaiwa na anayedai, tunakwenda huko Waheshimiwa, lakini huko kunahitaji ujuzi wa wanasheria, wao wanasheria watatuelekeza, tufanye hivi kuna kosa gani. Mambo mengi tumeshafanya na tumeshaunda kamati kadhaa.

Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe kazungumza soko jipya, kasema sisi tunataka soko jipya nyinyi mnatuambia mnakarabati. Mhe. Spika, soko jipya nilizungumza na nikasema kwamba kwa sasa serikali haina mpango wa kujenga soko jipya, lakini haya yaliopo tuyatengeneze. Nyinyi nyote mnasikitika na kutuambia hapa kwamba masoko mabovu yanavuja, hakuna usafi. Kwa hivyo, kwanza tumeona tushike hapo, lakini kwa serikali kushughulikia habari ya masoko, yameshakuja maombi tayari ya *private sector*, pale Darajani wanataka wajenge *mall* moja kubwa sana. Lakini sasa tunataka tuone kwamba kweli *is it practicable* pale, patafaa pale. Sasa hayo tuwaachie *private sector* tutashirikiana nao. Sasa hiyo mipango ya kujenga soko kwa upande wa serikali hamna, lakini tuboreshe haya yaliopo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kulikuwa na maneno kidogo sio mazuri kuyarejea, lakini yamezungumzwa kwamba ripoti ni utumbo mtupu, haifai. Mimi nasema kweli hivi sisi watu wazima, wizara nzima tukae tufanye utumbo, sisi watu tuna heshima zetu bwana, tunajua nini tunafanya, hivi kweli ripoti ukaiite utumbo mtupu. Mhe. Spika, nafikiri kidogo tuheshimiane, lugha hiyo kidogo sio nzuri wala haipendezi hata kidogo.

Mhe. Spika, labda mimi nafikiri mtu mwenyewe hajui kutafsiri maneno, kwa sababu ujuzi wake mdogo ndio maana akaita utumbo, lakini kama hujui ujuzi wako mdogo waachie wengine watafsiri. Mhe. Spika, nafikiri lugha kama hii sio nzuri. Sisi baada ya kuitayarisha Mhe. Spika. Mimi sio mwanasheria na tunao wanasheria wizarani kwetu, tulikuja Baraza la Wawakilishi tukaomba ushauri wa Katibu, tukamwambia katibu wewe ni mwanasheria, tunataka *presentation* hebu tushauri. Akatuambia chukueni haya haya ya jumla muyaelezee utekelezaji wenu, na hivyo ndivyo tulivyofanya, tungechambua moja moja yale basi tungeandika buku jengine la nini, halina haja.

Kwa hivyo, mimi ninachotaka kusema Mhe. Spika, nawaombeni sana, natumia hili neno sana, na bado naliomba tena tuaminiane, hatukupewa dhamana hizi kwa kubahatisha. *Alhamdulillah*, tumekwenda kisha tukapata mapumziko kidogo, tukarudi ulingoni na mpaka leo tuko kwenye *system*. Kwa hivyo, sio watu na sisi wa kudharauliwa kiasi hicho, kutuambia hufai, siamini kabisa. Kuna wengine wameondoka wakarudi, kuna wengine wako kwenye *cabinet* ya Muungano wamekwenda wakarudi. Leo mnawaambia mawaziri hawafai, nafikiri hiyo sio sahihi hata kidogo, lazima kidogo ile heshima yetu ya mtu na mtu iwepo, kama tunavyoheshimiana basi lazima tuheshimiane.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tutunze nidhamu. Uzingatie muda Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Namaliza sasa hivi Mhe. Spika. Mhe. Subeit Khamis Faki alizungumzia suala la jaa lile la Darajani. Nakubaliana na yeye kabisa, tatizo tulilonalo jamani kwa majaa kweli tuna tatizo la magari, tunapata tabu sana. Sisi mji unatuuma sana kwamba taka hazichukuliwi, magari yaliopo yale ni spana mkononi, kwa hivyo hapa akili yetu yote ni hivyo vitu vipya vinavyokuja kwa mradi wa *ZUSP*, kuna magari 4 yatakuja kwa mji na Pemba yanapelekwa mawili mawili, kwa kweli wanasafisha sana jamaa, lakini zinarundikana pale kwa matatizo. Bado jaa la kutupia taka tuna tatizo nalo, sasa tunalizungumza. Pale Jumbi tumefurushwa, tukenda Ndijani nako huko tunatumia mafuta mengi tumefurushwa, lakini sasa hivi tunatafuta *technology* tumeshauriwa nyengine ya kufanya *compost* kutokana na taka, lakini pia wameshajitokeza wafadhili wengine wameleta mazingatio yao tutizame vipi hizo taka tutazigeuza umeme, linazingatiwa nalo hilo, hatusemi tayari linazingatiwa.

Mhe. Spika, kusema kweli suala la usafi kama linavyowakera nyinyi basi na sisi linatukera hivyo hivyo na tunahitaji mji wetu uwe safi kabisa. Kwa hivyo, rai iliyotolewa Mhe. Spika, ya kukaa na kamati sisi hatukatai tunaikubali, tunaikubali lakini tena upande huo wa mengine nakuachia wewe mwenyewe Mhe. Spika, sisi tutazidi kuchukua ushauri wao, lakini ninachosema mimi tupeni nafasi ndani ya miezi mitatu mingine hii, naamini kabla ya bajeti mtaona hatua ambazo tumekuja nazo na tutakazowasilisha utekelezaji wetu kwenye bajeti. Kwa sababu mipango mingi sana iko njiani. Ndio hiyo inakubalika hilo neno la kizungu kabisa, *pipe line*, sio unapanga leo na kutengeneza leo, haiwezekani Mhe. Subeit na Mhe. Mohamed ni lazima mambo mengi yawepo kwenye *pipe line* yanatengenezwa kidogo kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kweli mimi sina zaidi, nawaomba Waheshimiwa mtuamini, mtuamini na mtuamini.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hii ni *road map*, huu ni mpango wetu na tume-*condense*, hatukutaka kuirejea ripoti yote, hapana hayo mmeshatuambia na sisi tumeona, tunataka tutengeneze.

Mhe. Spika, mimi nimalizie niseme ninayakubali yote mliyotuelekeza, mliyotushauri na tumo kuyafanyia kazi kisheria sasa. Maana yake ni lazima tupate *element* ya kisheria, wanaoingia hatiani watiwe hatiani, sio Mkurugenzi tu kuna na wengine pia, sio kama wamesameheka hapana, kumuhamisha mtu kwanza tumeona tuchukue ile haraka sana, ili angalau aondoke pale, akishaondoka kuna mengine yanakuja na sheria itachukua mkondo wake.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi nawashukuru sana Waheshimiwa na ninawaomba mtuachie tukaifanyie kazi, na naamini nakuahidini matunda yake mtayaona. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe, anachoomba Mhe. Waziri kwamba tumuachie aendelee kuifanyia kazi, niwahoji basi wale wanaokubali ombi la Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kushirikiana vyema kutekeleza shughuli zetu na niwaombe tu tuendelee na utaratibu wa ushirikiano kwa ajili ya kufanya shughuli zetu ziwe bora zaidi kwa manufaa ya wananchi wetu. Katika taarifa hii iliyowasilishwa na kuamua tumuachie Mhe. Waziri akaifanyie kazi, imeombwa kwamba kamati na yeye Mhe. Waziri hakuwa na tatizo hilo, lakini akasema anaachia kiti kuamua.

Sasa mimi nataka niwakumbushe tu Waheshimiwa Wajumbe, katika vikao vyetu vya kamati ya uongozi nadhani na *briefing*, juu ya masuala haya tulielekezana kwamba kamati iwe inafikia mwisho wa shughuli zake. Kwamba kamati ikishawasilisha taarifa yake hapa, kilichobaki sasa ni juu ya serikali kutekeleza. Sasa kamati iliyopita ambayo ilishauriwa kwamba wakae pamoja na Mhe. Waziri, ilikuwa sababu yake moja maalum. Kwanza ile ripoti ilikuwa ni kubwa sana na mambo ni mengi mno. Sasa ilikuwa ieleweke ni lipi na lipi halijatekelezwa. Baraza la Wawakilishi likaamua kwamba *ok* basi Waziri kakae na kamati ili tuone hayo maeneo ambayo hayajatekelezwa.

Lakini hayo mapendekezo 13 yaliyotajwa yameguswa, kilichoelezwa Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba utekelezaji wake haujatimia vyema, kuna baadhi ya maeneo na kimsingi ukizingatia Waheshimiwa Wajumbe hapa ni baadhi ya maeneo ndio tumetaja fulani kwa nini hajachukuliwa hatua. Waziri ameeleza kwamba hatua za kisheria zinachukuliwa.

Mimi nataka nielekeze kwamba tukubaliane na hili, kuchukua kama vile tunachukua moja kwa moja bila ya kuzingatia taratibu za kisheria na hiyo itakuwa ni kinyume cha sheria. Sasa chombo

chetu hiki kufika pahala kuelekeza utekelezaji wa jambo, halafu ukawa kinyume na sheria basi heshima ya chombo hiki itashuka.

Kwa hivyo, tuwe makini sana tunapotoa maelekezo na maagizo kwamba maagizo hayo yatekelezwe kwa mujibu wa sheria, ili hatimaye chombo hiki kisije ikawa ndio sababu ya kuingia katika matatizo ya kushtakiwa serikali, maana inaweza ikashtakiwa, kwa sababu umekiuka sheria. Kama tulivyoelekeza katika ripoti iliyopita kwamba ni vizuri, tena Mhe. Ismail Jussa Ladhu alikuwa makini sana katika hilo, kwamba yale maeneo ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua za kisheria, basi tuhakikishe kwamba tunafuata taratibu za kisheria. Lile jambo ambalo linahusu kwenda labda kwa DPP lifanyiwe kazi kwa utaratibu huo. Yale mambo ambayo yanahitaji taratibu za utumishi zitumike basi ifanyike hivyo. Vyenginevyo watakaoathirika na hayo maamuzi wanaweza kuchukua hatua ya kuishtaki serikali na hiyo itakuwa ni hasara.

Jambo jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe, nataka niwaambie ni kwamba tumekuwa na kamati teule nyingi sana, ukweli wa mambo katika utekelezaji wa bajeti ya Baraza la Wawakilishi tumekuwa na nakisi kubwa. Sasa tusiwe sisi Baraza la Wawakilishi ni wa kwanza kuvunja taratibu za bajeti, kwamba tunatumia bajeti kubwa zaidi kuliko ile ambayo imepitishwa humu ndani.

Kwa hivyo, na hii naunga mkono pale ambapo tumesema kwamba kamati ikimaliza kazi ndio imeshamaliza kazi, ili tusiendelee kutumia pesa nyengine zaidi kwa ajili ya kamati ile kuendelea kufanya kazi ambayo kimsingi wajibu wake imekwisha kutimiza baada ya kuwasilisha ripoti yake katika Baraza hili la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba tuzingatie sana hayo, juu ya taratibu za kisheria, taratibu za matumizi, ili tuhakikishe kwamba Baraza letu liwe ni mfano wa matumizi bora, lakini pia ni mfano wa kusimama juu ya taratibu za sheria.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo basi. Muongozo wa Spika Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, maelezo yako mwenyewe uliyokuwa ukiyatoa yalikuwa ni muongozo, kwa hivyo sina nia ya kutaka kuweka utaratibu. Lakini umesema kitu kimoja, cha msingi nilikuwa naomba utuwekee sawa ili kiwe muongozo kwetu, kwa Spika na kwa serikali na vile vile kuepusha hayo ambayo umeyazungumza ya kuingiza gharama ambazo hazihitajiki.

Mhe. Spika, ni *trend* sasa kwamba takriban ukitizama kamati zote zilizokuwa zimeundwa za teule, zina pendekezo moja ambalo linajirejea la kutaka kuchukuliwa hatua za kisheria kwa watu mbali mbali. Kama ulivyosema mimi nilikuwa mmoja niliyesisitiza kwamba utaratibu uliokuwa kikatiba wa kwamba chombo kinachohusika na kupeleka mashtaka na kuridhika kwamba hayo mashtaka yanatimiza sifa ni Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Waziri, naogopa tusijetukaondoka na ufahamu huo, ni kwamba serikali kwa ujumla wake, sio yule Waziri ambaye ile ripoti inamgusa tu. Kwa hivyo, kunapokuwa na mapendekezo ya kuchukuliwa hatua za kisheria, ufahamu wangu mimi ni

kwamba serikali kwa jumla yake ndio inayochukua dhamana ya utekelezaji, inachukua ile ripoti na vielelezo vyake inapeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, na ndivyo inavyofanyika katika nchi zote, hata hapo Bara ndio inavyofanyika hivyo, tumeshuhudia Uingereza ikifanyika.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka hilo liwekwe wazi kwamba tunapotoa pendekezo kama hilo Mhe. Spika, nafikiri muongozo wako unahitajika kwamba je, inakuwa ndio mwamvuli kwamba kuna hatua za kisheria haziruhusu Baraza la Wawakilishi au ni kwamba serikali inapochukua ripoti kwa utekelezaji maana yake ni pamoja na kuchukua dhima ya kufikisha ripoti ile kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa yale maeneo ambayo yatachukuliwa hatua za kisheria. Nilikuwa naomba muongozo wako katika hilo Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maelezo ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu yanajieleza wenyewe. Ripoti kama hii inakuwa na mambo mbali mbali, kama vile ripoti zilizopita ambazo kamati imewasilisha hapa na mapendekezo yake. Kuna baadhi ya mambo ambayo moja kwa moja kuna tuhuma kwamba kumefanyika makosa, ambayo pengine hatua za kisheria zinahitajika. Itabidi iwe imechambuliwa tujue haya yamekwenda kwa mkondo wa DPP au kwa kadiri itakavyokua, lakini kuna mambo mengine ya kiutumishi itabidi iende kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi. Maana yake hata ukimpelekea DPP hana la kufanya sio sehemu ya kazi yake.

Kwa hivyo, nadhani sehemu fulani inakuwa ni Baraza la Wawakilishi, inategemea namna mapendekezo yalivyokuja, kama yamekuwa *itemised* vizuri, basi mengine moja kwa moja yanaonekana kwamba haya mkondo wake ni kwa *DPP*. Lakini kama ni ya jumla jumla, itabidi sasa wizara ambayo imetumwa ikafanye kazi hiyo iyachambue yale yanayohusu hatua za kinidhamu, hiyo sio ya *DPP*. Yale mambo ya kiutumishi hayo sio ya *DPP*. Lakini kama kuna tuhuma za wizi na ubadhirifu, hayo ni *DPP*. Kwa hivyo, inategemea na wizara na namna Baraza hili la Wawakilishi lilivyotoa yale maelekezo juu ya mapendekezo ya kamati, ndio yatakayosema kwamba sasa serikali ikae iyachambue ijue yepi yanakwenda kwa *DPP* na mambo gani ya kwenda kwa utumishi na masuala gani yanabakia ndani ya wizara kwa ajili ya hatua za kinidhamu.

Nafikiri huo uwe ndio muongozo juu ya suala ambalo Mhe. Mjumbe umelisema. Basi niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe na sasa niakhirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kunzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Kuweka Utekelezaji wa Majukumu na Uwezo wa mambo yanayohusiana na hayo naomba usomwe kwa mara ya kwanza.

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo naomba usomwe kwa mara ya kwanza.

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari na mambo yanayohusiana na hayo naomba usomwe kwa mara ya kwanza.

Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati na mambo yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mahkama ya Biashara Zanzibar

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mahkama ya Biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo naomba usomwe kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe Katibu anatuarifu kwamba shughuli zetu zimemalizika. Kwa kuwa shughuli zimekwisha basi mimi niseme maneno mawili tu, nayo ni maneno ya shukurani.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa ambayo mmetupa katika kuendesha shughuli zetu za mkutano huu wa kumi, ambapo miswada minne ya sheria pamoja na maswali mbali mbali na ripoti ziliwasilishwa na shughuli zote hizo zimekwenda kama zilivyopangwa. Kwa hivyo, sina budi kuwashukuru kwanza nyinyi Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Mawaziri wote, lakini nisiwasahau watendaji wetu kwamba shughuli hiyo isingekwenda vizuri kama si wao kujipanga vizuri na shughuli zetu zikawa zimekwenda kama vile ambavyo imekusudiwa.

Lakini pia wenzetu hawa ambao wanatumurika humu ndani pamoja na waandishi wa habari nao nichukue nafasi hii kwa niaba yenu kuwashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo tumekuwa tunashirikiana, kuanzia tarehe 16/01/2013 tulipoanza mkutano huu wa kumi. Sasa basi, Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo nichukue nafasi hii kwa heshima na taadhima nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nianze hotuba yangu hii kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa Kumi wa Baraza la Wawakilishi, mkutano ambao umefanyika kwa maelewano makubwa sana. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, usalama na utulivu na kutuwezesha kupiga hatua kubwa za kimaendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mhe. Spika, nakupongeza kwa dhati wewe mwenyewe pamoja na wasaidizi wako wakuu, ambao ni Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuendelea kuliongoza Baraza letu kwa busara, hekima, umakini na ufanisi mkubwa na kufuata vyema misingi ya kidemokrasia na Kanuni za Baraza. Nachukua fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali za kudumu za Baraza kwa kutekeleza majukumu yao kwa hekima kubwa, na kwa haki na uadilifu, lengo likiwa kuliwezesha Baraza lako tukufu kutekeleza majukumu yake ya kusimamia shughuli za serikali na kuona kwamba shughuli hizo zinaendeshwa vizuri na kwa uadilifu.

Mhe. Spika, kwa aina ya kipekee, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Spika, Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umakini mkubwa, hekima, busara na uadilifu. Uongozi wa Mhe. Rais ndio chachu ya maendeleo tunayoendelea kuyapata katika nyanja za kijamii na kiuchumi. Sote ni mashahidi jinsi Rais Shein anavyoonesha kwa vitendo utendaji bora katika serikali na kuhimiza watendaji kubadilika na kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea, ingawa bado kwa baadhi ya watendaji wetu tabia hii inawapa tabu kuiacha. Nawaomba sana waiache tabia hiyo. Tunamshukuru sana Mhe. Rais na tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima, afya njema na uwezo wa kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, pia nampongeza sana Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Spika, Maalim Seif Sharif Hamad kwa kumsaidia vizuri Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mashirikiano makubwa anayompa katika kuiendesha nchi yetu. Natoa shukrani

nyingi kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao ya msingi ya kuwasilisha mawazo ya wananchi waliowachagua na pia kwa kusimamia vyema utendaji wa serikali yetu ili kuona utendaji bora wa serikali katika kukuza uchumi wa nchi na kutoa huduma kwa jamii ya Wazanzibari. Vile vile, nawapongeza sana Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Watendaji wote wa Serikali kwa kuendelea kuchapa kazi na kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mhe. Spika, nina kila sababu ya kuvipongeza na kuvishukuru Vyombo vya Habari vyote hapa Zanzibar, hasa Shirika la Habari la Zanzibar (*ZBC*) kupitia Redio na Televisheni ambavyo viliendelea kurusha moja kwa moja maendeleo ya shughuli za Baraza yalivyokuwa yanakwenda na kuwawezesha wananchi wetu kufuatilia kwa makini hoja, michango na mijadala iliyoendeshwa Barazani. Kwa furaha kubwa nawapongeza na kuwashukuru wakalimani wa lugha ya alama kwa kazi zao nzuri walizozifanya; kutafsiri mijadala kwa ishara ili wananchi wetu wenye ulemavu wa kutokusikia nao waweze kufuatilia mijadala ya Baraza.

MASUALA MUHIMU YALIYOJIRI NCHINI:

Mhe. Spika, kama sote tunavyoelewa nchi yetu imo katika harakati za mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume ya Maoni ya Mabadiliko ya Katiba tayari imemaliza kazi yake ya kukusanya maoni kutoka kwa wananchi na Taasisi mbali mbali hapa Zanzibar na Tanzania Bara, na pia imeshakamilisha zoezi hilo kwa upande wa Viongozi. Nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wote Unguja na Pemba kwa kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao.

Sasa ni kazi ya Tume kufanya uchambuzi wa maoni ya wananchi na naamini kabisa kwa uwezo wa Wajumbe wa Tume hiyo nchi yetu itapata Katiba mpya yenye kukidhi matakwa ya wananchi walio wengi na ambayo itaendeleza umoja na mshikamano wetu na kudumisha muungano wa nchi yetu. Wakati Tume inaendelea na kazi zake za kuandaa rasimu ya Katiba, nawasihi wananchi wote tuwe wastahamilivu na tuwe na subira na tuendelee kuchapa kazi ili tuweze kuiletea nchi yetu maendeleo kwa faida ya wananchi wetu na kwa faida ya vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Spika, katika mwezi wa Agosti, 2012 nchi yetu ilikuwa katika zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi, zoezi ambalo limefanyika kwa mafanikio makubwa licha ya kujitokeza changamoto katika baadhi ya maeneo. Matokeo ya Awali ya Sensa hiyo yalitangazwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 31 Disemba, 2012 katika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam. Matokeo hayo yanaonesha kwamba Tanzania hivi sasa tupo watu 44,929,012 na Zanzibar tumefikia watu 1,303,560.

Kwa upande wa Zanzibar, idadi hii ya watu ni kubwa na kwa kweli tunahitaji kuwa na mipango madhubuti ya kudhibiti ongezeko la kasi la idadi ya watu. Sasa inatulazimu kuongeza bidii katika kufanya kazi na kuzalisha kwa wingi bidhaa zitakazokidhi mahitaji yetu ya ndani na kupata ziada ya kuuza nje. Vile vile tutahitajika kuimarisha huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama na makaazi. Nawasihi viongozi wote katika ngazi zote na wananchi kwa ujumla tuzidishe mashirikiano na tuzidishe ari ya kujituma na kuwajibika zaidi katika maeneo yetu ya kazi katika sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sensa ya 2002, Zanzibar ilikuwa na watu wapatao 980,000. Katika Sensa ya 2012, miaka kumi baadae, Zanzibar inayo watu 1,303,560. Ongezeko la watu 323,560, hili ni ongezeko kubwa sana. Hatuna budi sasa tufanye maarifa ya kupunguza kasi ya kuzaliana ili watoto wetu tuwalee vizuri zaidi.

Mhe. Spika, tarehe 12 Januari, 2013, nchi yetu iliadhimisha miaka 49 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Katika maadhimisho hayo, miradi 53 ya maendeleo iliwekewa mawe ya msingi na kuzinduliwa. Miradi hiyo ina thamani ya wastani wa Shilingi bilioni 97 na ilikuwa katika sekta ya elimu, maji safi na salama, afya, kilimo, uvuvi na miundombinu ya habari, mawasiliano na barabara. Hii ni hatua kubwa ya maendeleo ambayo nchi yetu imepiga katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati viongozi katika ngazi zote na wananchi wote kwa kushirikiana katika kufanikisha sherehe zetu hizi adhimu ambazo zilifana sana.

Vile vile nawashukuru makamanda na askari wa vikosi vyetu vya ulinzi, Wajumbe wa Kamati ya Halmashauri ya Sherehe na Maadhimisho na Wanafunzi walioshiriki katika halaiki na maandamano na Wanahabari, kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo imetuletea mafanikio makubwa katika maadhimisho ya Mapinduzi yetu. Hivi sasa tunakabiliwa na maandalizi ya maadhimisho ya Mapinduzi ya kutimiza miaka 50 (nusu karne) ifikapo tarehe 12 Januari, 2014. Ni imani yangu viongozi sote na wananchi tutaendelea kushirikiana ili kuzifanya sherehe zetu hizo kuwa za mfano na za hadhi ya juu kulingana na umuhimu na hadhi ya Mapinduzi yetu.
Mhe. Spika, hivi karibuni nilipata fursa ya kuzindua utekelezaji wa Mradi wa *TASAF* Awamu ya Tatu hapa Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar na una jumla ya Shilingi Bilioni 470 ambazo zitatumika kusaidia kaya masikini kwa kipindi cha miaka mitano (5) ijayo. Naomba niwaelekeze watendaji wote watakaohusika na utekelezaji wa mradi huu kufanya kazi kwa umakini, bidii na uadilifu ili kuhakikisha malengo na matarajio ya mradi huu yanafikiwa. Viongozi kwa upande wao hawana budi kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi huu ikiwa ni pamoja na kubuni miradi mbali mbali itakayokuwa na manufaa kwao.

Mhe. Spika, lengo la Serikali zetu kuandaa mradi huu ni kutekeleza kwa vitendo ahadi zake kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupunguza makali ya umasikini. Nachukua nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Unguja na Pemba na viongozi na watendaji wote walioshiriki katika utekelezaji wa *TASAF* Awamu ya Pili kwa kazi nzuri walizofanya na kupelekea kupata mafanikio makubwa ya mradi huu ambayo yamewafurahisha Wahisani wetu ambao ni Benki ya Dunia, Shirika la Misaada la Uingereza (*DFID*) na *USAID* na kufikia maamuzi ya kutusaidia tena katika awamu hii ya tatu. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nawashukuru kwa dhati Wahisani hao kwa misaada yao mikubwa kwa Tanzania na kwa Zanzibar.

MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA BARAZANI:
Mhe. Spika, katika mkutano huu wa 10 wa Baraza lako Tukufu, Waheshimiwa Mawaziri wamewasilisha miswada minne (4) ya sheria ambayo ina umuhimu mkubwa kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu. Miswada iliyowasilishwa na kupitishwa na Baraza lako tukufu ni:

- Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997.

- Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usafiri Nam. 5 ya mwaka 2006.

- Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar Kazi, Majukumu na Utawala wake pamoja na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

- Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Shirika la Meli Zanzibar Kazi, Uwezo na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, Mswada wa kwanza uliojadiliwa ni Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo Nam. 6 ya mwaka 1997. Marekebisho ya Sheria hii yana lengo la kuimarisha demokrasia nchini mwetu pamoja na kuviongezea uwezo vyama vya siasa kushiriki katika chaguzi zote zinazoendeshwa nchini. Mgawanyo wa ruzuku hiyo kwa vyama vya siasa utafanywa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa baada ya Mhe. Rais kuweka saini sheria hiyo.

Mhe. Spika, Mswada wa Pili uliojadiliwa na Baraza lako Tukufu ni Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya mwaka 2006. Mswada huu unakusudia kuweka mazingira bora ya udhibiti wa masuala ya usafiri wa baharini na kuhakikisha kuwa yanatekelezwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria hii. Marekebisho ya Sheria hii yamezingatia maeneo mbali mbali ikiwemo suala la umri wa meli kutumika kwake tangu ilipoundwa ambayo itaruhusiwa kuingia nchini.

Aidha, suala jengine lililozingatiwa ni kutobadilisha uasili wa meli, kutoka kwenye uasili wa meli ya kubeba mizigo na kuwa meli ya abiria. Lengo hasa la Mswada huu ni kuwalinda wananchi kutopoteza maisha yao kutokana na ajali zisizo na sababu.

Mhe. Spika, pia marekebisho ya sheria hii yana lengo la kuweka uwiano na mashirikiano mazuri kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuhakikisha usalama wa usafiri baharini kutokana na kwamba meli zinasafiri pande zote mbili za Muungano. Haya yote ni maudhui yaliyozingatiwa kwenye marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini.

Mhe. Spika, marekebisho ya sheria hii pia yanalenga kuweka utaratibu mzuri wa usafiri wa abiria na mizigo kwa vyombo vya baharini na hivyo kuondoa sababu za kibinadamu zinazosababisha ajali.

Mhe. Spika, Mswada mwengine uliowasilishwa na kujadiliwa kwenye Baraza lako Tukufu ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar, Kazi, Majukumu na Utawala wake pamoja na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mswada huu unakusudia kufuta Tangazo la Sheria Nam. 111/2011 la kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar pamoja na kazi na majukumu yake.

Umuhimu wa kuanzisha upya Shirika hilo umekuja kutokana na haja ya kuwa na chombo kimoja tu, kitakachosimamiwa na kuendeshwa na uongozi wa aina moja tu ambao ni Mkurugenzi Mkuu mmoja, Mhariri Mkuu mmoja, Mhandisi Mkuu mmoja na Meneja wa Vipindi. Utaratibu huu wa sheria hii utaliimarisha Shirika pamoja na kuleta ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako wakati wakijadili mswada huu walisisitiza sana umuhimu wa kuwepo na wataalamu wa fani mbali mbali watakaoweza kuliendesha Shirika letu la Utangazaji kwenye mazingira yaliopo sasa ya kiushindani kwa lengo la kuwavutia wananchi.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi kwamba serikali imejipanga vyema katika kuliimarisha shirika kimajengo, vifaa na wataalamu, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu hao.

Mhe. Spika, serikali imo kwenye hatua zake za mwisho za kuondoka kwenye matumizi ya analogia na kwenda kwenye dijitali. Ni dhahiri kwamba matumizi ya mfumo wa dijitali yanahitaji utaalamu wa hali ya juu unaoendana na ubunifu ili Shirika hili liweze kusonga mbele kwa kutoa habari za kisiasa, kiuchumi na kijamii za ndani na nje ya nchi.

Serikali itayazingatia sana maslahi na marupurupu ya wafanyakazi wa Shirika hilo ili kuwajengea mazingira mazuri ya kuweza kuwajibika ipasavyo na kuweza kulibadilisha kwa kuimarisha huduma zake ili ziwe nzuri na za haraka zaidi. Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla wana mategemeo makubwa ya kuona Shirika hili linabadilika sana na kuondokana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea. Huu sasa ni wakati wa kutoa huduma za kiushindani, kutafuta wateja na kubuni mambo mbali mbali ili kuweza kukidhi mahitaji ya walengwa.

Mhe. Spika, tunakusudia Shirika hili lijiendeshe kibiashara, hivyo kila atakayetumia huduma zake, ikiwa ni pamoja na Baraza la Wawakilishi, itawalazimu kuzilipia huduma hizo.

Mhe. Spika, Mswada wa Nne uliojadiliwa katika Mkutano huu wa 10 wa Baraza lako ni Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Shirika la Meli Zanzibar, Kazi, Uwezo na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, Shirika la Meli hapo awali liliundwa kwa mujibu wa Amri ya Rais iliyotolewa mwaka 1983 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Nam. 4 ya mwaka 1978 ambayo imeshafutwa na kwa sasa Mashirika yote ya Umma yanasimamiwa na Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2004. Mswada uliopitishwa na Baraza lako unakusudia kutekeleza Sera ya Usafiri ya Zanzibar pamoja na Mpango Mkuu wa Usafiri wa mwaka 2008 na kuliwezesha Shirika jipya la Meli kutoa huduma za usafiri zilizo bora na zinazoendana na matwaka ya viwango vya ushindani wa Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, serikali ina lengo la kuwa na usafiri wa baharini ulio bora zaidi na endelevu hapa Zanzibar. Sote tunaelewa jinsi nchi yetu ilivyokumbwa na misiba mikubwa kutokana na kukosa usafiri wa baharini wa uhakika. Nchi yetu ni ya visiwa ambapo usafiri mkubwa unaotumiwa na wananchi walio wengi ni kwa njia ya bahari.

Serikali yetu imeanza kuchukua jitihada za hali na mali za kuweza kuagiza meli kubwa, ya uhakika na itakayoweza kuchukua abiria wengi na mizigo kwa usalama. Kwa mantiki hiyo, serikali imekusudia kuanzisha Shirika la Meli litakaloimarisha huduma za meli kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi na kibiashara.

Aidha, Shirika litasimamia uendeshaji wa meli zetu kitaalamu na kibiashara ili ipatikane tija na faida ya kuliimarisha shirika hilo. Serikali itachukua hatua za kuhakikisha kwamba Shirika hili linapatiwa wataalamu na kuendeshwa kwa ufanis, tija na kibiashara.

Mhe. Spika, Sheria hizi zote zimetungwa na Baraza lako tukufu kwa nia ya kuwatumikia wananchi. Ningependa kuwasihi watekelezaji wa sheria hizo wazisimamie na kuhakikisha kuwa zinatekelezwa ipasavyo, bila ya kumuonea haya au aibu mtu yoyote atakayezikiuka sheria hizi.

Mhe Spika, mara nyingi Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wamekuwa wakilalamika kuwa sheria nyingi zimetungwa lakini kumekuwa na udhaifu wa kusimamia utekelezaji wake. Nakubaliana na malalamiko hayo. Hii ni kwa sababu wasimamizi wa sheria zinazotungwa hawawajibiki ipasavyo.

Kwa mfano, tuangalie, usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani. Hausimamiwi vizuri na wahusika. Utaona waendesha baiskeli wakiendesha baiskeli zao usiku bila taa, magari yanaendeshwa usiku bila namba *(Number plates)*, hatujui madhumuni yake ni nini, wapanda mapiki piki hawavai kofia za kinga *(helmet)*. Wanaosimamia sheria hizi wapo, lakini wanaangalia tu. Nawaomba sasa watekelezaji na wasimamizi wa sheria hizi watimize wajibu wao. Huu ni mfano mmoja tu lakini ipo mifano mingi.

Mhe Spika, katika jitihada za kuimarisha uchumi na kuimarisha shughuli za uwakala, serikali inaendelea na juhudi zake za kutafuta washirika wa maendeleo na wawekezaji watakaochangia ujenzi wa bandari mpya ya kibiashara ya Mpiga Duri, ili serikali iweze kuongeza mapato yake kutokana na meli kubwa zitakazotumia bandari hiyo.

Mhe Spika, Baraza lako Tukufu liliunda Kamati Teule ya Kuchunguza utendaji wa Shirika la Umeme na Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa. Nawapongeza kwa dhati Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizi kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kufuatilia kwa kina masuala mbali mbali kwa mujibu wa hadidu rejea walizopewa na kuwasilisha ripoti zao katika Baraza hili. Nawashukuru Wenyeviti wa Kamati hizo kwa umakini wao na kufanya uchunguzi wa kina kuhusu utendaji katika Taasisi hizo.

Mhe Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba serikali imepokea ripoti hizo za Kamati Teule zilizowasilishwa katika Baraza na itazifanyia kazi taarifa hizo pamoja na mapendekezo yake yote kwa umakini mkubwa na kuchukua hatua kadri itakavyoonekana inafaa. Nirudie kuwapongeza Viongozi na Wajumbe wote wa Kamati hizi kwa kazi kubwa waliyoifanya, ambayo serikali inathamini sana kazi yao hiyo yenye lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji serikalini. Ningependa kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, kwamba wale wote waliotajwa kwenye ripoti hiyo watashughulikiwa ipasavyo kwa kuzingatia haki na utawala bora. Kama baadhi ya Wajumbe walivyosema, aliyekuwemo hatoki na asiyekuwamo hataingia.

Mhe Spika, katika Mkutano huu, jumla ya maswali 72 ya msingi na maswali 130 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wawakilishi na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri husika. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuja na maswali mazuri yenye lengo la kujenga zaidi na kuimarisha uwajibikaji wa watendaji wa serikali. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa majibu yao ya kina ambayo hatimaye yaliwaridhisha Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe Spika, nachukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako na wananchi wote wa Zanzibar kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa, inayoongozwa na kiongozi makini, Dkt. Ali Mohamed Shein inafanya kazi kubwa ya kuiletea nchi yetu maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha huduma za jamii. Katika kufanikisha hayo, serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha sekta za uzalishaji, zikiwemo za kilimo, mifugo na uvuvi, kuimarisha sekta ya viwanda, utalii na biashara na kuendeleza sekta ya miundombinu nchini.

Vile vile, serikali itaendelea kuimarisha sekta ya elimu, afya na kuhakikisha wananchi wote wa mijini na mashamba wanapata maji safi na salama kwa kuimarisha afya zao na kuwa na nguvu kazi bora itakayoshiriki katika kukuza uchumi wetu. Lengo kuu la jitihada hizi ni kukuza uchumi na kupunguza umasikini katika nchi yetu.

Mhe Spika, ili tuweze kufanikiwa katika jitihada zetu hizi, ni lazima sote tuwajibike katika kutunza mazingira yetu. Hatuna budi sote kwa pamoja kushiriki kikamilifu katika upandaji wa miti, utuzanji wa misitu yetu ya asili na kuachana na tabia ya kuchimba mawe na mchanga ovyo bila ya vibali na kutupa taka ovyo. Aidha, nawataka wafanya biashara ambao bado wanaendelea na tabia ya kuingiza mifuko ya plastiki nchini waachane na tabia hiyo mara moja, kwani kuendelea kufanya hivyo ni kuhatarisha afya zetu na vizazi vyetu. Uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu, hivyo kila mwananchi ana wajibu wa kutunza mazingira kwa manufaa ya nchi yetu.

UNUNUZI WA MELI:

Mhe Spika, kama nilivyoeleza hapo awali na katika hotuba yangu wakati wa kufunga Mkutano wa Nane wa Baraza lako Tukufu nilieleza juhudi inayofanywa na serikali za kununua meli mpya, kubwa ya abiri itakayokidhi mahitaji ya usafiri wa baharini katika Visiwa vyetu na katika maeneo ya mwambao wa nchi jirani. Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba serikali imekwisha chukua hatua hizo na hivi karibuni serikali itatiliana saini mkataba na Kampuni ya Damen ya Uholanzi itakayotengeneza meli hiyo.

Mhe Spika, meli hiyo itakuwa na uwezo wa kuchukua abiria wapatao 1,200 na mizigo yenye uzito wa tani 200. Meli hiyo itachukua miezi 18 kutengenezwa baada ya mkataba kuwekwa saini na pande mbili hizo husika. Hivyo, wananchi wa Zanzibar wategemee, kama mambo yote yatakwenda sawa, kupata meli mpya mnamo robo ya mwisho ya 2014, ingawa inawezekana ikawa zaidi kabla ya hapo.

Mhe Spika, kwa mara nyengine tena naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, Wajumbe wa Baraza lako, Waandishi wa Habari na wananchi wote kwa mashirikiano makubwa katika kuliendesha Baraza letu kwa mafanikio. Kadri siku zinavyoendelea mbele, wananchi

wanazidi kujenga matumaini makubwa na Baraza hili na serikali yao na hii ndio ishara ya kukua kwa utawala wa demokrasia nchini.

Mhe Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako Tukufu hadi siku ya Jumatano, tarehe 3 April, 2013 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kumpigia makofi mengi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Hiyo ina maana yakumpongeza kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa hivi punde katika kufunga Mkutano wetu huu wa kumi. Na mimi kwa niaba yenu naomba nimshukuru sana kwa hotuba hii ambayo imejaa miongozo tele ya kuendesha nchi yetu.

Waheshimiwa Wajumbe hapo ndio mwisho wa shughuli zetu, hoja imetolewa na sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Mimi sina zaidi isipokuwa sasa nichukue nafasi hii kuakhirisha Mkutano huu wa Kumi hadi siku ya Jumatano tarehe 03/4/2013, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 11:40 jioni Baraza liliakhirishwa hadi

tarehe 3/4/2013 saa 3:00 asubuhi)